

ELIMU YA UKUAJI: Ubora wa Neno la Mungu.



Mtayarishaji wa Nakala halisi (Toleo la Kingereza)

® RANDOLPH BARNWELL

Tovuti: www.Randolphbarnwell.com

Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili (Toleo la Kiswahili)

na

Mchungaji Jackson Lyimo, S.L.P 47, Mlandizi, Pwani- TANZANIA

Tel: +255 752 421 500, Barua pepe: ndosariolimo141@gmail.com

Kimehaririwa na..

Askofu Samwel Meena, S.L.P 47, Mlandizi, Pwani- TANZANIA

Tel: +255 782 304 916, Barua pepe: meenasamwel1@gmail.com

Na

Kimepigwa chapa na..

Mission to Unreached Areas Church

S.L.P 47, Mlandizi, Pwani- TANZANIA

Tel: +255 657 348 464, Tovuti: tounreached@yahoo.com

**Mafundisho haya yameandaliwa na
RANDOLPH BARNWELL kwa kushirikiana na Mission to Unreached Areas Church**

Unaruhusiwa na unatiwa moyo kuzalisha na kusambaza mafundisho haya kwa muundo wowote ambao:

- 1. Utamtambua mwandishi wa nakala hii.**
- 2. Utaonyesha marekebisho yoyote katika nakala hii.**
- 3. Na kwamba hutaweka gharama zaidi ya zile ulizotumia(hutafanya biashara)**
- 4. Hutaruhusiwa kutengeneza nakala zaidi ya 200.**

Kama utahitaji kuweka mafundisho haya katika mitandao ya kijamii au kuwa na matumizi tofauti na hayo yaliyotajwa hapo juu, tafadhali wasiliana na

**Mission to Unreached Areas Church
S.L.P 47, Mlandizi, Pwani- TANZANIA
Tel: +255 753 304 306, Tovuti: tounreached@yahoo.com**

Yaliyomo

MADA YA KWANZA	Uk. 5
i. Neno la Mungu ndiyo asili ya Mungu	Uk. 5
i.i Mungu na Neno lake ni wamoja.....	Uk. 5
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 11
MADA YA PILI	Uk.12
i. Neno linatubadilisha sisi tufanane na asili ya Mungu.....	Uk. 12
i.i Mbegu ya Neno inafanyika kuwa mwana wa Ufalme	Uk. 12
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 19
MADA YA TATU	Uk. 20
i. Kuishi kwa kila Neno linaloendelea.....	Uk. 20
i.i Tii yote anayosema Mungu na hivyo jifunze njia zake.....	Uk. 20
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 31
MADA YA NNE	Uk. 32
i. Kumfunua Kristo kutoka katika Maandiko	Uk. 32
i.i Ufunuaji wa Ki-uungu kwa kumwonyesha Kristo kutokana na Neno la Mungu.....	Uk. 32
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 42
MADA YA TANO	Uk. 43
i. Kioo cha Neno	Uk. 43
i.i Jione wewe mwenyewe katika Kristo katika Neno.....	Uk. 43
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 54
MADA YA SITA	Uk. 55
i. Kuchanganya Imani na Usikiaji wa Neno	Uk. 55
i.i Imani kama kiini kuelekea asili ya Mungu.....	Uk. 55
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 67
MADA YA SABA	Uk. 68
i. Sauti ndani ya sauti	Uk. 68
i.i Mungu hunena kupitia Baba yako wa Kiroho	Uk. 68
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 80
MADA YA NANE	Uk.81
i. Neno la Mungu katika nyumba ya Mungu	Uk. 81
i.i Nyumba ya Mungu – Familia ya Mungu hulipa kipaumbele Neno la Mungu	Uk. 81
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 93

MADA YA TISA.....	Uk. 94
i. Neno la Mungu ndiyo nyumbaYa Mungu.....	Uk. 94
i.i Yakobo anavyoiona nyumba ya Mungu na mvuto kwa mataifa kuiendea Nuru.....	Uk. 94
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk.104
MADA YA KUMI	Uk. 105
i. Wito wa kuangaza kama mianga duniani	Uk. 105
i.i Wito wa kuwa Nuru.....	Uk. 105
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 115
MADA YA KUMI NA MOJA: 1.....	Uk. 116
i. Upendo wa kwanza	Uk. 116
i.i Kumpenda Mungu kuna akisiwa kwa upendo.....	Uk. 116
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 125
MADA YA KUMI NA MOJA: 2.....	Uk. 126
i. Upendo wa kwanza	Uk. 126
i.i Uchunguzi kifani kuhusu Waefeso.....	Uk. 126
i.ii Maswali ya rejea na majadiliano katika kikundi.....	Uk. 139

NENO LA MUNGU NDIYO ASILI YA MUNGU.

Lengo: Mungu na Neno lake ni wamoja.

DABAR, LOGOS, RHEMA

Agano la Kale liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania. Agano Jipya liliandikwa kwa Kiyunani (baadhi ya sehemu kwa Kiaramu)

Tafsiri ya neno “NENO” katika Agano la Kale ni Dabar kwa Kiebrania.

Neno **Dabar** au **daba’r** lina maanisha: **-kauli** au **maandishi, maneno yaliyokwisha tamkwa** mahali ambapo kutimbia kwa kilichotamkwa, kimetungwa mimba ndani ya neno lililokwisha tamkwa. Wakati mwingine neno hili linatafsiriwa kama **kazi**. Ni kama vile wakati wa kutamka, kuna kukumbuka kitendo kinacho ambatana na neno hilo kwamba tayari kimesha *timia* au *kukamilishwa*.

Maneno mawili ya Kiyunani yanayo tafsiri neno “NENO” ni logos na rhema

Logos maana yake = Intelijensia (Uwezo wa akili/kufikiri). Neno linalo elezea intelijensia hiyo (uwezo huo wa akili) ni **kuhutubu/kuhubiri, kauli, kitu; kubainisha mawazo.**

Rhema maana yake = **Kile kilichokwisha semwa/nenwa, tamkwa, maelezo au neno, tamko (binafsi, kwa pamoja au mahsus) kwa kuhusisha jambo au maandishi.**

LOGOS

Logos ingeweza kuwakilisha ukweli wote wa Biblia nzima – yaani maandiko kwa ujumla wake.

2Timoteo 2:14-16

14. *Uwakumbushe mambo hayo, ukiwaonya machoni pa Mungu, wasiwe na mashindani ya maneno, ambayo hayana faida, bali huwaharibu wasikiao.*
15. *Jitahidini kujionyesha kuwa mmekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno (logos) la kweli.*
16. *Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu.*

Ile logos ya Neno la Mungu ni lazima itumiwe kwa halali au itafsiriwe kwa usahihi (KJV) hasa kwa viongozi na kwa wale wote wanaohubiri na kufundisha.

Istilahi, **litumiwe kwa halali (NASB) au litafsiriwe kwa usahihi” (KJV)** ni neno la Kiyunani linaloitwa:- “Orthotomeo”

Maana ya Orthotomeo= kufanya mkato mnyoofu, kuchangua (kuelezea kwa usahihi kabisa, kukata bila kupindisha, kukata kwa njia zilizo nyooka, kuendelea na njia zilizonyooka, kushikilia mwendo ulionyooka, sawa na kutenda kwa usahihi, kufanya kwa unyoofu na kwa ulaini, kudhibiti sawa, kufundisha ukweli moja kwa moja na kwa usahihi, kudhibiti kwa usahihi, kwa ustadi.

2Timoteo 2:15: *Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli kwa usahihi (ISV)*

Angalizo: Katika fundisho letu kuhusu ‘Logos’ tunalazimika kila wakati kutafuta kufahamu Nafsi ya Kristo ni nani. Kwa Roho Mtakatifu, yeye ndiye mwandishi wa maandiko. Kadri tunavyojifunza ukweli, kujifunza kwetu hakulazimiki kuwa kwa kitaaluma sana na kuwa na mazoezi mengi ambayo ni sawa na kupata ubaridi na kupima joto. Kadri tunapojihusisha na ukweli wa Neno la Mungu kwa kulisoma na kwa kujifunza, lazima litufikishe katika upeo wa kumfahamu Kristo, nafsi ya UKWELI. Yesu ndiye KWELI (Yoh 14:6). Ukweli siyo mafundisho mengi sana au kanuni nyingi sana kama ilivyo katika ufunuo wa nafsi yaani Kristo.

Rejea Yeremia 2:8. *Makuhani hawakusema, Yuko wapi Bwana? wala wana - sheria hawakunijua wachungaji nao waliniasi, nao manabii walitoa unabii kwa Baali, wakafuata mambo yasiyo faidia kitu.*

‘Tunza’ au tapas maana yake = kamata, shikilia, teka, twaa kwa ustadi/ujuzi.

Kadri tunavyo LISHIKA Neno la Mungu, iwezekane katika kusoma kwetu, kujifunza na kusikiliza, lituvute na kutuingiza katika uhusiano wa ndani zaidi na Kristo.

Yohana 5:39. *“Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake, na hayo ndiyo yanayonishuhudia*

1Yohana 1:1-4

1. *Lile lililokuwepo tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima;*
2. *(na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu.)*
3. *hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.*
4. *Na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe.*

RHEMA

Rhema ya Neno kadri inavyo tofautiana na Logos, ni mfano katika agizo la twaeni upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu, “Waefeso 6:17. Rejea hapa, siyo katika Biblia nzima kama ilivyo katika logos, lakini ni katika andiko moja ambalo Roho hulileta katika kumbukumbu zetu ili tulitumie wakati wa mahitaji, kwa sharti kwamba tunaendelea kuhifadhi maandiko katika fahamu zetu mara kwa mara.(Vines)

Ikiwa ‘logos’ ingewakilishwa na kisima basi ‘rhema’ ingewakilishwa na ndoo ya maji yaliyochotwa kutoka katika kisima husika. Rhema ni neno ambalo Roho Mtakatifu huvuvia kwa wakati muafaka kutoka logos,- ni neno maalumu linalofaa katika hali maalumu kwa ajili ya mtu maalumu au kundi la watu maalumu.

Baadhi ya ulinganifu unaoweza kuuzingatia.

LOGOS

RHEMA

Chungwa	-	Vitamini zilizomo ndani ya juisi ya chungwa husika.
Kinanda chote/Piano yote	-	Sauti ya ufunguo au noteni.
Mwili wote wa mwanadamu	-	Kiungo kimoja hutenda tendo maalum.

Wakati wote Rhema humtegemea logos. Rhema hutokana na logos. Bila ya logos, huwezi ukapata rhema. Mmoja anaweza akanena kutoka logos ya Mungu na kwa wasikiaji ikasikika kama Neno la rhema kutoka kwa Mungu.

1Petro 4:11. *Mtu akisema, na aseme kama mausia (logion) ya Mungu; (KTV)*

1Petro 4. *Yeyote anaye nena, afanye hivyo kama mmoja anenaye matamshi (logion) ya Mungu; (NASB)*

Warumi 10:17. *Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno (rhema) la Kristo.*

Tunaweza tukatumia neno la rhema kwa kile ambacho wengi wanakiita MAHUBIRI YA KINABII. Siyo kila uwasilishaji wa Neno la Mungu uwe na umuhimu wa asili ya unabii. *Kuhubiri* hapa linatumiwa kwa mtu ambaye *ametengwa* na Mungu *kunena kwa niaba* Yake. Unenaji huu unaweza mara nyingine ukawasilishwa kwa wasikilizaji kama ukweli wa Kibiblia ulio fanyiwa utafiti, kujifunzwa na kuandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa. Kwa sababu unabii una kipimo cha uvuvio na ‘ufunuo’ mahubiri ya kinabii, hata kama hilo neno limefanyiwa utafiti na kuandaliwa kwa mpangilio, linakuwa na sura zifuatazo:

- Neno linalohubiriwa huwa ‘rhema kwa kusanyiko hilo maalum kwa wakati huo. Neno hilo kwa ujumla linaweza kutumika na waaminio wote, lakini ni kwa hadhira maalum ambayo liliandaliwa kwa ajili yake. Linakuwa la kipekee na lenye uhusiano wa kiroho na lenye kufaa kwa wakati huo.
- Maneno halisi, maandiko, fafanuzi, mawazo, kutamka kwa sauti, na hata viashiria vya mwili vinaweza vikawa vimevuviwa Ki-Uungu.
- LOGOS ni ufafanuzi uliotolewa kwa ajili ya Yesu Kristo, ambaye ni mwana.

Yohana 1:1-4

1. *Hapo mwanzo kulikuwepo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
2. *Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.*
3. *Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilicho fanyika.*
4. *Ndani yake ndimo ulimokuwapo uzima, nao uzima ulikuwa nuru ya watu.*

Ufunuo 19:13 *Naye amevikwa vazi lililo chovywa katika damu, na jina lake anaitwa, Neno la Mungu.*

NENO LA MUNGU NDILO JINA LA MWANA KONDOO

Neno la Bwana ni Mungu mwenyewe.

Yohana 1:1-2

1. *Hapo mwanzo kulikuwepo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
2. *Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.*

Mungu hawezi kuwa Mungu nje ya Neno lake.

Mwana alikuja katika muktadha wa mwelekeo wa dunia kufunua uzuri na asili ya vyote vilivyomo ndani ya Mungu. Uwana ni bomba au chombo tu ambacho kinaweza kumwelezea Mungu kwa usahihi na kwa ukamilifu. Huyu Mwana aliye mfano, Yesu Kristo, alikuja kama “Neno lililofanyika mwili”. Kufanana na Neno ndiyo njia pekee tunayoweza kuwa kielelezo cha asili ya Mungu. Tunaiweka asili ya Mungu katika matendo kwa upendo na utii wetu kwa Neno la Mungu. Mungu hawezi kujulikana, kuelezewa au kutathiminiwa nje ya Neno lake. Mungu na Neno lake ni wamoja haiwezekani kutengua.

Sisi, tulio jamii ya kitume, tunasimama na Mwana kondoo juu ya Mlima Sayuni (mahali pa ukamilisho na ung’arisho). Mwanga ni kiwakilishi cha kanisa. TUNALO JINA LA Mwana kondoo na jina la Baba yake katika paji la nyuso zetu.

Ufunuo 14:1

1. *Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana - Kondo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao.*

Hii 144,000 siyo namba ya kawaida ila ni alama inayo wakilisha jamii ya kitume iliyotengenezwa ili ifanane na Kristo, mwana kondoo katika heshima zote na tukitenda kazi tukiwa na ufahamu wake katika vipaji vya nyuso zetu. Mwana wa Mungu anafafanuliwa hapa kama mwana kondoo. Sisi tulio wana wake, tunalo jina lake na jina la Baba yake katika vipaji vya nyuso zetu.

Ililahi ‘jina’ inaelezea mambo mawili

- 1) asili
- 2) kusudi au hatima ya kinabii.

Jina = Onomazo maana yake =*toa jina, teua jina*; kwa kufafanua hadi kutamka, kutaja, kutangaza, ita jina, mpa jina.

Ililahi *jina* ina maana kubwa zaidi kuliko inavyotumika kumtambulisha mtu na hivyo kutofautisha mtu mmoja na mwingine. Inaonesha ile asili, tabia na hali ya huyo mtu ikiwa ni pamoja na kuonesha utendaji na hatima yake.

Mifano: Jina Yakobo lililokuwa na maana ya (kubadili au mdanganyifu) lilibadilishwa kuwa Israel (mtu aliyeshindana na Mungu) likiashiria mabadiliko katika tabia na utambulisho.

Yusufu (“Mungu ameongeza”) aliitwa Barnaba (mwana wa kutia moyo) likisisitiza asili ya utendaji wake wa kitume. Hivyo basi, jina la mtu lina beba kumbukumbu kuelekea utambulisho na hatima ya mhusika. Utambulisho ni wa maana katika kukamilisha hatima au matokeo.

Ufunuo 19 inaashiria lile jina la mwana Kondoo ndilo NENO LA MUNGU

Ufunuo 19:7-13

7. Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana -Kondoo imekuja, na mkewe amejitweka tayari.
8. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing’arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.
9. *Naye akaniambia Andika, Heri walio alikwa karamu ya arusi ya Mwana –Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu.*
10. *Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndiyo roho ya unabii.*
11. *Kisha nikazona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda, aitwae Mwaminifu na Wa-kweli, naye kwa haki ahukumu na kufanya vita.*
12. *Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi; naye anajina lililoandikwa, asilolijua mtu ila yeye mwenyewe.*
13. *Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake anaitwa, Neno la Mungu. Jina [linabeba asili na kusudi] la mwana na Baba huja kwetu kupitia kushikamana nao na kwa neno la Mungu. Ni kupitia Neno la Mungu tu kwamba Baba na mwana wanadhihirishwa [soma Yoh. 14 hapa chini]*

Jina (yaani asili na kusudi) la Mwana na Baba huja kwetu kupitia ujihusishaji na utii kwa Neno la Mungu. Ni kwa kupitia tu, Neno la Mungu kwamba, Baba na Mwana wanafunuliwa. (Soma Yohana 14 hapo chini)

Yohana 14:19-26

19. *Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakua hai.*
20. *Siku ile ninyi mtatambua kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.*
21. *Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye nimpandaye; naye anipandaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*
22. *Yuda [siye Iskariote], akamwambia, Bwana, imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu?*
23. *Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*

‘Kuwa’ na ‘Kuzishika’ amri za Mungu kunakuweka wewe katika nafasi ya kufikia dhihirisho za kipekee za upendo wa Baba na mwana [mst 21], ikiwa ni pamoja na kushiriki katika baadhi ya siri za Mungu za mafunuo yake Mwenyewe kwako.

Funua= emphanizo maana yake = dhihirisha, onsha ionekane, mtu kujionesha mwenyewe, toka uonekane, tokeza, kaa uonekane, jifunue, ashiria, tangaza, fanya kujulikana.

Tia maanani jinsi Mungu alivyo jifunua mwenyewe kwa Abrahamu kama ‘Yehova Yire’ kwa sababu ya utu wake kwa amri ya Mungu kwake ya kumtoa mwanawe Isaka [Mwanzo 22]. Kila tendo la utii lina uwezo wa kukufungulia sura nyingi za nafsi ya Mungu na nguvu zake kwako. Upendo wako kwa Mungu unapimwa kwa utii wako kwa Neno lake na unavyo endelea kumtii Yeye, Yeye ataji hudhurisha mwenyewe kwa mamlaka katika maisha yako [mst 23] na ataendelea kujiachia na kujifunua zaidi na zaidi Yeye Mwenyewe kwako.

NENO LA MUNGU NDIYO ASILI YA MUNGU.

Zaburi 138:2. *Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote[NASB]*

Ona hapa kwamba, Mungu amelikuza Neno lake SAWA NA JINA LAKE.

Biblia ya (KJV) inaelezea (Zaburi ya 138:26) kama ifuatavyo:

“kwa kuwa umelikuza Neno lako juu zaidi kuliko jina lako”.

Neno ‘**juu**’ kwa kiasi fulani **linapotosha linapo wasilisha** lile wazo kwamba Neno limewekwa juu ya Jina la Mungu. Hakuna sehemu ya Mungu iliyo dhaifu au yenye stahili, uthamani na uzito pungufu kuliko sehemu nyingine ya Mungu. Kwa kweli wazo kuwa zipo ‘sehemu’ za Mungu na kwamba zinaonekana kutengana ni upotofu. Mungu ni wa kushikamana ndani yake mwenyewe. Yeye ni mkamilifu. Hivyo NASB ilivyo unda mstari huu inaonekana kuwa sahihi zaidi: Neno la Mungu linakuzwa KUFUATANA na Jina lake lote. Jina lake linaelezea asili na tabia yake. Neno lake haliko juu ya hili, lakini ni kwa kufuatana nalo. Hivyo basi, Neno Lake ndilo Jina, asili na tabia yake.

Zingatia tafsiri hizi :-

ESV: [Kuwa umelitukuza juu ya vitu vyote jina lako na neno lako](#)

NIRV: [Umeliheshimu jina lako na neno lako kuliko kitu kingine chochote.](#)

NIV: [Umeliinua juu kuliko vitu vyote jina na neno lako.](#)

NLT: [Kwa kuwa ahadi zako zinafadhiliwa kwa ukamilifu wa heshima ya jina lako.](#)

Wakati neno la Kiebrania ‘Al’ lilitafsiri kama ‘kufuatana’ [NASB] au ‘juu’ [KJV] inashauri kitu kama kuwa na umaarufu kuliko kingine, lakini ni muktadha wa aina fulani ambapo maneno haya yanavyo tumika utafunua msisitizo huu. Katika Zaburi 138:2, ufahamu wa jumla ni ‘kufuatana ‘na’ na siyo ‘juu’. Brown, Driver na Briggs-[wasomi wa Kiebrania] wanatoa visawe [synonyms] kwa neno la Kiebrania ‘al’ (vinavyo weza kutumiwa katika Zaburi 138:2)’ kwa mashiko ya matumizi ya:- “kufuatana na, kwa maelezo kuwa, kuhusu, karibu ya, kuyaongezea kwa, pamoja na”.

**MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA
KIKUNDI.**

1. Fafanua maana ya neno ‘Dabar’ katika Agano la kale.
2. Unaelewa nini kuhusu maneno haya ya Kiyunani ‘Logos’ na ‘rhema’? Eleza jinsi mahusiano yalivyo baina yake.
3. Imani huja kwa kusikia Neno la Mungu. Elezea.
4. Mtu anaweza kunena kutoka ‘Logos’ lakini wasikilizaji wakasikia kama ‘rhema’. Onesha hili kwa kutumia maandiko.
5. Katika kujifunza kweli za ‘logos’ inanipasa kwa hali zote kuzingatia ufahamu ulio wazi wa Kristo aliye nafsi ya kweli : [jadili maelezo haya]
6. Hili ‘jina’ la Mwana-kondoo ndilo “Neno la Mungu”.Istilahi ‘jina’ ina maanisha nini katika Maandiko na ni kwa namna gani inaweka sawa uelewa wetu kuhusu jina la Mwana kondoo kama Neno la Mungu?
7. Sisi kama wana wa Mungu ni jina la nani limeshika fahamu na mawazo yetu [vipaji vya nyuso]? Jadili hili na onesha ukitumia mifano kwa vitendo.
8. Kufuatana na Yoh 14. Ni njia gani za msingi ambazo kwa hizo Baba na mwana wanajidhihirisha na kujifunua wenyewe kwetu hatua kwa hatua?
9. Fafanua jibu lako la swali la 8 kwa kuonesha mchakato katika maisha ya Abrahamu katika Mwanzo 22.

NENO LINATUBADILISHA SISI TUFANANE NA ASILI YA MUNGU.

Lengo: Mbegu ya Neno inafanyika kuwa Mwana wa Ufalme.

NENO LA MUNGU-NDIYO MBEGU YA UZIMA WA MUNGU NDANI MWETU
INAYOTUBADILISHA TUFANANE NA SURA YAKE KILA WAKATI.

Neno la Mungu ni hai na lina nguvu - (Waebrania 4:120) Neno la Mungu ni roho na uzima (Yohana 6:63)

Waebrania 4:11-12

11. *Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano huo huo wa kuasi.*
12. *Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena la choma hata kuzigawa nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

Waebrania 4:12a. *Kwa maana Neno analo litamka Mungu ni hai na limejaa nguvu [analifanya kuwa hai, tendaji, hutia nguvu, na lenye kufaa]; [AMP]*

Yohana 6:63. *Roho ndiyo itiyayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyo waambia ni roho, tena ni uzima.*

Wakati tulipo yasikia maneno haya ya ukweli – tuliyatoa maisha yetu kwa Kristo, kumtegemea na kuwa na imani Naye.

Waefeso 1:13. *Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena, mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho Yule wa ahadi aliye Mtakatifu. [NKJ]*

Waefeso 1:13. *Ndani yake, ninyi pia, baada ya kuusikia ujumbe ule wa kweli, injili ya wokovu wenu tena mkamwamini yeye, mkatiwa muhuri ndani yake na Roho Yule wa ahadi.*

Tumezaliwa mara ya pili kupitia Neno la Mungu.

Yohana 3:5. *Yesu akajibu, Amin, Amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingia Ufalme wa Mungu.*

Maneno, ‘zaliwa kwa maji’ Linaelezea kule kuzaliwa kwa Neno la Mungu, ikiwa maji ni aina ya alama ya Neno la Mungu.

Waefeso 5:25-27

25. *Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake;*
26. *ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno;*
27. *apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*

Katika kumkubali Kristo aingie ndani ya mioyo yetu, Neno la Mungu ndilo lililokuwa ufunguo na tendaji katika mwanzo huu wa ujuzi wa kuzaliwa upya. Neno la Mungu ni kama MBEGU iliyo pandwa- soma Marko 4. Mbegu hii inabeba uwezo wa kukua na kuwa mti mkubwa wenye uwezo wa kuzaa matunda mengi. Neno la Mungu ndani yetu ni mbegu, inayotupa fursa ya kukua ndani ya yote aliyo nayo Mungu. Kama vile mbegu ilivyo wekewa kuficha pamoja na uwezekano wa kukua sana, Neno la Mungu ndicho chombo pekee ambacho uwezo wote na uwezekano wa asili pamoja na asili na nguvu za Mungu vinaachiliwa na kupata kujidhihirisha ndani mwetu. Katika kuingia kwetu katika Ufalme wa Mungu, uwana wetu uliamshwa tulipo lipokea na kuliamini Neno la Mungu lililonenwa kwetu. Kutoka hapo na kuendelea, ukuaji wetu hadi kufikia ukamilifu wa uwana katika Mungu hadi ukomavu, unategemea kujihusisha kwetu kuendelea na Neno, ambalo ni mbegu ya Ki-uungu.

Yakobo 1:18-21

18. *Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake.*
19. *Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu awe mwepasi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika;*
20. *kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu.*
21. *Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zetu.*

Zingatia- alituzaa sisi kwa Neno la kweli.

Alituzaa- apokueuo maana yake = *kuzaa kwa kubadilishwa; kuleta kwa kuzaa*

Mungu alituzaa sisi kupitia Neno Lake. Neno lake ndiyo njia pekee ya kupitia ambayo VINASABA vyake, mfanano wake, sura na tabia- vinaweza kuambukizwa kwetu. Mungu alituingizia mbegu isiyo haribika ya Neno lake lenye nguvu ndani yetu katika hatua za awali za ujuzi wa wokovu wetu. Mbegu hii ya Neno la Mungu ina uwezo wa kubadilisha asili yetu. Inapaswa kupokelewa mara kwa mara ili iongezeke kikamilifu ndani ya ukamilifu wa sura ya Mungu. Ni kupitia katika Neno Lake tunaweza kuwa na asili na tabia yake

1Petro 1:22-25

- 22 *Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.*
- 23 *Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyo haribik;, kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.*
- 24 *Maana, “MWILI WOTE NI KAMA MAJANI, NA FAHARI YAKE YOTE NI KAMA UA LA MAJANI. MAJANI HUKAUKA NA UA HUPUKUTIKA;*
25. *BALI NENO LA BWANA HUDUMU HATA MILELE. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.*

1Yohana 3:9.*Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutoka kwa Mungu.*

Neno – wakati ‘linapo hubiriwa kwenu’ –linaingia lenyewe ndani yako kama mbegu ambayo tayari ina uwezo wa kubadilisha asili yako. Hii ni mbegu isiyoharibika – na nguvu yake inaingia ndani mwetu wakati tunapolitii. Nguvu ya Neno la Mungu ndani yetu hutufanya tuishinde dhambi.

Hatutaendelea kutenda dhambi- siyo kwamba hutatenda dhambi mara kwa mara- lakini ni kwamba hutatenda kama ndiyo mtindo wako au tabia yako ya maisha – ukitenda dhambi inakuwa una pingana kabisa na asili ya Mungu ndani yako, na kwa haraka utajirekebisha, utatubu na kutafuta ushindi imara katika eneo husika- soma 1Yohana 1:8-10 [zaidi ni hapo baadaye]

Utii wetu kwa Neno la kweli HUTAKASA nafsi zetu ili kwamba tuweze kuanza kuonesha viwango vya Ki-Uungu vya upendo kwa mtu na mwingine. Upendo ukiwa ndicho kiashiria cha hali ya juu cha asili ya Ki Uungu.

KUKUA KATIKA UKAMILIFU WA MSINGI NA ASILI YA MUNGU KUPITIA NENO LAKE.

Utukufu wa Mungu ndio rejea ya asili kamili ya Mungu. Ni mwana wa Mungu tu, mwenye uwezo uliokamilika wa kuwakilisha ile asili kamilifu ya Mungu.

Waebrania 1:1-5

- 1. Mungu ambaye alisema zamani za baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,*
- 2. Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliye mweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*
- 3. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu,*
- 4. Amefanyika bora kupita malaika, kwa kadri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao.*
- 5. Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wowote NDIWE MWANANGU MIMI LEO NIMEKUZAA? Na tena MIMI NITAKUWA KWAKE BABA NA YEYE ATAKUWA KWANGU MWANA?*

Uwakilishi =Charakter=Neno hilo kwa asili lilimaanisha kerezo au kifaa cha kutia nakshi; kifaa kinacho tumika kuchonga, kukata nakshi au kukereza. Baadaye kinatoa maono ya jinsi kilivyo, kwa kawaida ni **kitu kilicho kerezwa, kilichotiwa mkato au chapa, tabia, herufi, alama, ishara.**Utambulisho huu pamoja na maumbile yake ya kipekee yalitambuliwa kama kiwakilishi kamili cha kile kitu mbacho taswira yake ilinakshiwa/chongwa.

Asili= hupo'stasis maana yake = Kile ambacho ni msingi dhahiri, tangu sasa, *ukweli, kiini, uumbikaji/dutu, kile ambacho ndicho chanzo* cha kitu fulani, uhakikisho uliohibitishwa, kujiamini, uumbikaji/dutu, chochote kilichopo katika muonekano wowote, ukweli, asili muhimu.

2Petro 1:4 *Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*

Uungu = theios maana yake= Uungu, kilicho cha kipekee cha Mungu na kilichotoka kwake. Linatuonesha tabia ya Mungu kama vile nguvu zake na siyo tabia Yake katika asili na ujumla wake.

Asili = phusis = Kwa mfano wa silika za wazawa, umbile. Inatokana na ‘phuo’lenye maana ya ukuaji kwa kuchanua au kutanuka, kutokeza, kupasuka au kuvimba.

[Ukuaji ndani ya asili yake hakuna kutulia bali ni endelevu].

Mshiriki=koininos maana yake = mwana hisa ambaye ni mshiriki:-mwenz, ushirika, mshiriki, mbia.

Uharibifu = pthora= Uharibifu, maangamizi, kupotea, haribu, kile ambacho ni matokeo ya uharibifu, kinacho haribika, katika ufahamu wa kimaadili, uharibifu, k.v. uozo wa kiuadilifu.

Hapa asili ya kiuungu [phusis] inatukumbusha tabia na uthamani wa kiuungu wa Mungu na siyo asili/kitovu chake. Asili yake siyo uumbikaji ambao upo chini ya tabia zake. Sisi ni wawakilishi sahihi wa ASILI yake (Hupostasis). Huwezi ukapata picha ya ‘phusis’ bila ya ‘hupostasis’ yake. Asili ya Mungu ni neema na kweli-[**Yohana 1:14.**]

Hii Huja kupitia Neno. Pia katika [**2Petro,**] tunaungana na kuanza kushiriki katika asili ya kiuungu kwa njia ya Ahadi kubwa mno za thamani katika Neno. Uti na kujihusisha kikamilifu na Neno utaanzisha kuturudisha kwenye asili.

Asili na kusudi la Mungu Baba ndiyo, URITHI wetu [**Warumi 8:16, 17.**] Tumeupata kwa sababu, sisi ndio wana wazaliwa wake wa kwanza.Tumerithi JINA LILILO KAMILI ZAIDI YAANI MWANA/MZALIWA WA KWANZA [**Waebrania 1:18.**] Tunaingia katika urithi huu kupitia kuipokea Neema kwa njia ya NENO LA MUNGU [**Mdo 20:32**]

MWANA ANAFANYIKA KUWA MBEGU - MTU ANAFANYIKA KUWA NENO

Matayo 13:1-23

1. *Siku ile Yesu akatoka nyumbani, akaketi kando ya bahari.*
2. *Wakamkusanyikia makutano mengi, hata akapanda chomboni, akaketi; na ule mkutano wote ukasimama pwani.*
3. *Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda.*
4. *Hata alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila;*
5. *nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina;*
6. *na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka.*
7. *Nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga;*
8. *nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja thelathini.*
9. *Mwenye masikio na asikie.*

10. *Wakaja wanafunzi, wakamwambia, Kwanini wasema nao kwa mifano?*
11. *Akajibu, akwaambia, Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa.*
12. *Kwa maana yeyote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini yeyote asiye na kitu, hata kile alichona nacho atanyang'anywa.*
13. *Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.*
14. *Na neno la Nabii Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa; Kutazama mtatazama wala hamtaona.*
15. *Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na Macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya.*
16. *Lakini, heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia.*
17. *Kwa maana, amin, nawaambia, Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayo yaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayo yasikia ninyi, wasiyasikie.*
18. *Basi ninyi sikilizeni mfano wa mpanzi.*
19. *Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja Yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyu ndiye aliyepandwa karibu na njia.*
20. *Naye aliye pandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha;*
21. *lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa.*
22. *Naye aliye pandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno; likawa halizai.*
23. *Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyo ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo; yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu sitini, na huyu thelathini.*

Maana za alama katika mfano huu:

Mpanzi = ni mhubiri

Mbegu = ni Neno

Aina ya udongo = Namna neno lilivyosikiwa ndani ya hali ya mazingira ya moyo wa mtu fulani ita athiri kwa haraka ule uwezo wa Neno kuwa na matokeo yake kamili. Suala halisi hata hivyo ni namna mtu atakavyo kuwa na utayari na shauku ya kulitii Neno.

Chunguza: [Zab 111:10](#) *Kumcha Bwana ndiyo mwanzo wa hekima, wote wafanyao hayo wana akili njema, Sifa zake zaka milele.*

Kando ya njia = Husikia Neno; hushindwa kulielewa = hushindwa kulitii.

Juu ya mwamba = Husikia Neno, mateso yanatumwa kukujaribu wewe yakilenga neno ulilolisikia; unashindwa (Mungu hakujaribu wewe katika ulimwengu wa utii ili akuoneshe ni wapi umekosa kutii-Hapana-badala yake anafanya hivyo [KUKUONGEZA])

Linganisha: [chunguza mwamba ulio hapa chini sawa na mwamba katika mfano]

Matayo 7:24-27

24. *Basi kila asikiaye haya maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba;*

25 *mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba ile, isianguke kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.*

26 *“Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu mchanga;*

27 *mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga yumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.*

Katika miiba: Husikia Neno, hofu wasiwasi na kufukuzia utajiri kwa njia za udanganyifu hulisonga.

Udongo mzuri= Husikia Neno, hulielewa kwa kulitii.

Kila wakati tunapojiweka wenyewe chini ya usikivu wa Neno na tukaamua kuazimia kuchukua hatua za utii, tutaendelea kubadilika na kuingia katika asili au utukufu wa Mungu. Utukufu wa Mungu ndio asili ya Mungu. Utukufu huu ni lazima uambatane na “neema” na “kweli” kama ndizo sehemu zake muhimu. Neema ya Mungu kupitia Neno la Mungu. Utukufu wa Mungu unaonekana ndani na kwa kupitia sisi wakati neno la Mungu linapofanyika mwili ndani yetu k.v. wakati tunapo tii- huo ndio wakati ambapo neema inafanywa kuwa hai/ina amshwa. Kisha sisi pia kama wana wa Mungu na Yesu akiwa ndiye mwana wa kuigwa, tutajawa na neema na kweli ambavyo vitajitangaza vyenyewe kama utukufu- na hivyo tutakuwa tunaiweka ile asili ya Mungu katika maonesho machoni pa wanadamu.

ONA: Hata kuhusu udongo mzuri, kuna viwango vitatu tofauti vya uzaaji matunda (30, 60,100 yote haya yalitegemea kiwango cha utii). Hata hivyo kuna changamoto zaidi ya kuupeleka utii wetu kwenye kukamilishwa katika kila maeneo yote ya maisha yetu- soma **2Wakorinto 10:16, Filemon1:21,Waebrania 5:8.**

Matokeo ya hatima ya utii kamili kwa Neno ni kuzaa asili ya MWANA wa MUNGU ndani yetu.

Matayo 13:24-30

24. *Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyependa mbegu njema katika konde lake;*

25. *lakini watu walipo lala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.*

26. *Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu.*

27. *Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda kumwambia,Bwana, hukupanda mbegu njema katika shamba lako? Limepata wapi basi magugu?*

28. *Akawaambia, adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi wataka twende tukayakusanye?*

29. *Akasema, La; msije msije mkakusanya magugu, na kuzing’oa ngano pamoja nayo.*

30. *Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu.*

Ngano = Fundisho zuri la kitume;

Magugu=fundisho bovu/potofu. Neno zuri au fundisho [ngano] ni lazima liwe limeshikamana ndani yetu. Hivyo tufanyike kuwa Neno.

Matayo 13:36: *Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni.*

Yesu alifafanua tu lile fumbo akiwa ndani ya NYUMBA- ndani tu ya ‘nyumba’ mahali ambapo kanuni za kiroho za ubaba na uwana zinatenda kazi na ufunuo unaoeleweka unaweza kuzalishwa.

Angalia maana ya alama ya ngano na magugu zinavyo tupeleka katika maana halisi zaidi.

Matayo 13:37-43

37. *Aakajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni mwana wa Adamu;*

38. *Lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wale wana wa yule mwovu;*

39. *yule adui aliyepanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika.*

40. *Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia.*

41. *Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wakemachukizo yote, na hao watendao maasi,*

42. *na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*

43. *Ndipo wenye haki watapong’aa kama jua katika ufalme wa baba yao. Mwenye masikio, na asikie.*

Katika mfano wa kwanza mbegu ni Neno, katika mfano wa pili mbegu ni MWANA= Neno limefanyika mwili. NENO lifanyike MWANA.

Neno la Kiyunani linalotafsiri istilahi, mbegu katika Matayo 13:37 ni ‘sperma’ likiashiria mbegu, kwa pamoja kilichopandwa kina kichipukizi cha zao jipya na kinacho mea kutoka katika ile mbegu iliyo pandwa kinazaa (zodhiates). Wakati unapolisikia neno – ni kama vile mbegu za uzazi – sperma zina achiliwa kuingia katika tumbo la uzazi la roho yako na utungwaji hufanyika; upatanisho endelevu na tii huhakikisha kuwepo kwa uharakishwaji wa ukuaji kwa kile kilichozaliwa katika roho yako kikijidhihirisha kwa nje katika maisha yako yote.

Neno hili mbegu – sperma –lina uwezekano wote wa kiuungu kwa ajili yako kuongezeka hadi kufikia kuwa Mwana aliyekua /komaa wa Mungu.Yale magugu ni wana wa yule mwovu. Fundisho sahihi ni lazima lifanyike kuwa ndio mtindo wa maisha. Hatimaye ni kuzaa wana wanaofanana na Neno walilosikia.

Wana wa ufalme watatenganishwa na wana wa yule mwovu (**soma Yohana 8:44**) kwa kuzingatia neno kufanyika mwili au ushikamanaji wa kanuni katika mtindo wa maisha na tabia. Wana wa ufalme watang’aa kama JUA- wakiwa na uwezo na mng’ao wenye kutoa uzima.

Malaki 4:2 *Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza cheza kama ndama mazizini.*

2Wakorinto 3:1-3

1. *Je! Tunaanza tena kujisifu wenyewe? au tunahitaji, kama wengine, barua zenye sifa kuja kwenu, au kutoka kwetu?*
2. *Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote.*
3. *Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tulioikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.*

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI

1. Umezaliwa “mara ya pili” kwa Neno la Mungu. Fafanua usemi huu.
2. Neno la Mungu lina nafasi gani katika kutuwezesha kuwa na fursa ya kuwa washiriki wa ile asili ya Mungu?
3. Zingatia na kwa kifupi jadili kufanana kote kati ya “Neno la Mungu” na mbegu.
4. Kwa kile kinacho itwa mfano wa mpanzi (a) mpanzi (b) mbegu (c)aina mbali mbali za udongo. Vitu hivi vinawakilisha nini kwa kila kimoja?
5. Usikiaji na utii sahihi wa Neno la Mungu vina umuhimu gani?
6. Ule mfano wa ngano na magugu, mbegu njema (yaani ngano) vinaelezwa kama WANA wa ufalme waliopandwa katika muktadha wa wa ulimwengu. Katika mfano uliotangulia, mbegu ilikuwa ni Neno; sasa mbegu ni mwana. Hii ina maanisha nini?
7. Zingatia tofauti zote kati ya ngano na magugu na uzitumie kiroho kwa rejea ya kupambanua wana halisi katika ufalme wa Mungu na Wana wa Yule mwovu.
8. Kuna umuhimu gani wa kutenganishwa hivi viwili wakati wa kuvuna na siyo kabla ya kuvuna?
9. Zingatia kwamba Yesu alielezea ufalme kama ufalme wa BABA yake (Matayo 13:43) na kwamba ufafanuzi huo ulitolewa ndani ya “nyumba” [Math 13:36] Kuna jambo gani muhimu tunaloweza kupata hapa?

KUISHI KWA KILA NENO LINALOENDELEA.

Lengo : Tii yote anayosema Mungu na hivyo jifunze na jifunze njia zake.

Kumbu kumbu la Torati 8:1-20

1. *Amri hii ninayo kuamuru leo mtaishika kuitenda, mpate kuishi na kuongezeka, na kuingia katika nchi ile ambayo BWANA aliwaapia baba zenu; nanyi mtaimiliki.*
2. *Nawe utaikumbuka njia ile yote Bwana, Mungu wako, aliyo kuongoza miaka hii arobaini katika jangwa, ili akutweze, kukujaribu, kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri zake, au sivyo.*
3. *Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiojua wewe wala baba zako hawakujua; apate kukujulisha yakuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA.*
4. *Mavazi yako hayakuchakaa, wala mguu wako haukuvimba, miaka hiyo arobaini.*
5. *Nawe fikiri moyoni mwako, ya kuwa kama vile baba amrudivyo mwanawe, ndivyo BWANA, Mungu wako, akurudivyo.*
6. *Nawe uzishike amri za BWANA, Mungu wako, upate kwenda katika njia zake, na kumcha.*
7. *Kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yuakingiza katika nchi nzuri, nchi yenye vijito vya maji, na chemchemi, na visima, vibubujikavyo katika mabonde na vilima;*
8. *nchi ya ngano na shayiri, na mizabibu, na mitini, na mikomanga; nchi ya mizeituni yenye mafuta, na asali;*
9. *nchi utakayokula mikate humo, pasina shida, hutapungukiwa na kitu ndani yake; nchi ambayo mawe yake ni chuma, na milima yake yafukuka shaba.*
10. *Nawe utakula ushibe, utamshukuru BWANA, Mungu wako, kwa nchi nzuri aliyokupa.*
11. *Jihadhari, usije ukamsahau BWANA, Mungu wako, kwa kutozishika amri zake, na hukumu zake, na sheria zake, ninazokuamuru leo.*
12. *Angalia, utakapokuwa umekula na kushiba, na kujenga nyumba nzuri, na kukaa ndani yake;*
13. *na makundi yako ya ng'ombe na kondoo yatakapo ongezeka, na fedha yako na dhahabu yako itakapo ongezeka, na kila kitu ulicho nacho kitakapo ongezeka;*
14. *basi hapo moyo wako usiinuke, ukamsahau BWANA, Mungu wako, aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa;*
15. *aliye kuongoza katika jangwa lile kubwa lenye kitisho, lenye nyoka za moto na nge, nchi ya kiu isiyokuwa na maji; aliyekutolea maji katika mwamba mgumu,*
16. *aliye kulisha jangwani kwa mana, wasiojua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako.*
17. *Hapo usiseme moyoni mwako, Nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio ulionipatia utajiri huo.*
18. *Bali utamkumbuka BWANA, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo.*
19. *Lakini itakuwa, kama ukimsahau BWANA, Mungu wako, na kuiandama miungu mingine, na kuitumikia na kuiabudu, nawashuhudia leo ya kuwa mtaangamia bila shaka.*
20. *Kama vile mataifa yale ambayo BWANA, anawaangamiza mbele yenu, ndivyo mtakavyo angamia; kwa sababu hamkutaka kuisikilza sauti ya BWANA, Mungu wenu.*

ANGALIA TAFITI ZIFUATAZO KUTOKA KWENYE AYA HII.

Mstari wa 3: Kama huna njia ya kufikia unenaji wa sasa wa Mungu kupitia Neno lake basi unaishi kati ya ulimwengu wa kuoza na kufa- kiroho. Mtu anaishi kwa kila neno linalotoka kwa Mungu. Kushindwa kusikia na kutii Neno hili kunaleta kifo cha kiroho.

Mstari wa 2. Kwa kweli Mungu ‘anasahaulika’ wakati kanuni zake hazifuatwi tena. Matokeo ya kutotii kanuni zake kwa sehemu hutokana na kushusha heshima ya kutokuwa na kupuuzwa na uzito wa kunena kwake. Kama huzitii amri za Mungu, basi humpendi Yeye vya kutosha.

Tilia maanani maneno haya: ‘**MSIMKATAE YEYE ANENAYE**’

Waebrania 12:25-29

25. *Angalieni msimkataye yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale walio mkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni;*

26. *ambaye sauti yake iliitetemesha nchi wakati ule, lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia.*

27. *Lakini neno lile, mara moja tena, ladhihirisha kuhamishwa vile viwezavyo kutetemesha, kama vitu vilivyoubwa, ili vitu visivyoweza kutetemesha vikae.*

28. *Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemesha, na tuwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho.*

29. *maana Mungu wetu ni moto ulao.*

Kataa=paraiteomai=kana, epuka, jitenga, kataa

Matendo ya mitume 7:30-32

30 *Hata miaka arobaini ilipotimia, malaika wa Bwana akamtokea katika jangwa la mlima Sinai katika mwali wa moto, kijitini*

31 *Musa alipoona akastaajabia maono yale, na alipokaribia ili atazame, sauti ya Bwana ikamjia,*

32 *Mimi ni Mungu wa baba zako Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akatetemeke, asithubutu kutazama.*

Musa alikuwa na heshima kuu na uchaji wa ki –Mungu kwa SAUTI ya Bwana. Alitetemeke Neno la Mungu.

Isay 66:1-2

1. *Bwana asema hivi, mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; mtanijenge nyumba ya namna gani? na mahali pangu pa kupumzikia ni mahali gani?*

2. *Maana mkono wangu ndio uliofanya hivi vyote, vitu hivi vyote vikapata kutokea, asema BWANA; lakini mtu huyu ndiye nitakaye mwangalia, mtu aliyemnyonge, mwenye roho iliyo pondeka, atetemekaye asikiapo neno langu.*

Mbingu au nyumba yoyote iliyojengwa na mwanadamu haiwezi kuenea ukamilifu wote wa Mungu. Ni mtu tu, mwenye moyo uliopondeka na ulio mnyenyekevu na ambaye analitetemeke Neno Lake.

Waebrania 3:7-11

6. *bali Kristo, kama mwana juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.*
7. *Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, LEO, kama mtaisikia sauti yake,*
8. *Msiifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha, Siku ya kujaribiwa katika jangwa.*
9. *Hapo baba zetu waliponijaribu, wakanipima, Wakaona matendo yangu miaka arobaini.*
10. *Kwa hiyo nalichukizwa na kizazi hiki, Nikasema, Siku zote ni watu walio potoka mioyo hawa, Hawakujizua njia zangu.*
11. *Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia rahani mwangu.*
12. *Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai.*

“Leo” linaashiria umuhimu wa kuitikia kwa haraka na kwa kuona unenaji wa Mungu unafaa.

Ki-muktadha wale wasioitikia kwa utiifu unenaji wa Mungu, kwa kificho wanaonesha dharau Kwake na kwa sauti Yake kwa sababu.....

- Walikuwa wanatazama mno kazi zake (utendaji) mst 8 hadi kufikia kupuuza njia zake (kanuni) na hivyo hawakuhama kutoka kutegemea miujiza ya Mungu, kuelekea kutafuta na kutawaliwa na kanuni za Mungu.
- Waliendelea na kwa kurudia rudia “walipotoka ndani ya mioyo yao” [mst.10]
- “kupertoka” au planao maana yake ni = **“kusababisha kutanga tanga, kupotosha, kudanganya, kukosesha”**
- Inatukumbusha wale ambao kwa kupitia hila na ushawishi, waliacha njia iliyowekwa wakfu na kutanga tanga kweye upotofu. Yeye anayeonesha dharau kwa unenaji wa Mungu, anajifungulia mlango kwa ‘sauti nyingine’ na kwa ushauri wa kishetani wenye lengo la kumtoa ili atoke katika mapenzi ya Mungu.
- Wanastawisha mioyo migumu kwa kujitoa kwa asili danganyifu za dhambi [2:8,12].
Skleros linatokana na *skello*, likiwa na maana ya kufanya iwe ngumu “*kuwa kavu*” lilitumiwa kwa kitu kisichokuwa na *unyevu*, na hivyo kina *kwaruza* na *hakikubaliani na mguso*, na kwa hivyo kinaonesha “*ukali*, bila huruma au ugumu”. Mara zote inatumiwa kama istilahi ya *kushutumumu* na inaashiria *ukali*, hata *katika tabia ya mwanadamu*.
- Inazungumzia *ugumu wa shingo* na kule *kukataa kurekebika*. Kuto toa makubaliano ya haki na utii kuitikia unenaji na kutasababisha ‘kuteleza’ au ‘kwenda mrama’ yaani *kuiacha njia* (2:1).

Waebrania 2:1-3

1. *Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.*
2. *Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki,*
3. *Sisi je! tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia;*

Pararheo = kutiririka kupitia, kuteleza kwa karibu au kwenda mrama.

La muhimu hapa ni mtu kujiona mwenyewe kama “anatiririka” au “anapita karibu bila ya kutilia maanani yale aliyoyasikia”

Mst 12. Kutotambua Neno la Mungu humfanya mtu aathiriwe na kiburi na kutumainia utoshelevu binafsi na maarifa aliyo nayo, na kufikia kutomtambua Mungu. Mtu wa namna hiyo anaanza kutumika kwa kujitumainia bila ya Mungu. Staha kwa Mungu na utii kwa Neno lake ndio utaratibu unao tuhakikishia tunadumu kumtambua Yeye kwa mafanikio yetu na hivyo kutufanya tuwe wanyenyekevu kwa kadri tunavyo endelea kumtegemea Yeye kabisa kwa kila kitu.

Mst 19-20. *Matokeo ya mwisho ni kumuacha Mungu wa kweli na kukimbilia miungu ya kigeni na kuishia katika kifo cha kiroho ('kupotea'). Siri iliyo fichika inayosababisha hayo na matokeo yake kwa mara nyingine ni kwamba. "Kwa sababu hukuisikiliza sauti ya BWANA Mungu wako"*

Ni dhahiri kuwa katika mistari hiyo hapo juu ndani yake kuna uwezekano wa kufikia kufanikiwa kwa ukarimu na kwa utoshelevu katika kupata mahitaji yote ya mwili kwa sababu ya neema ya utoaji ya Mungu, na bado kwa sababu ya ukweli huu, unashawishika kukaa mbali na Mungu. Hili ni tatizo ikiwa mtu hajatoa kipaumbele kwa Neno la Mungu kuwa ndiyo kanuni ya msingi katika maisha yake.

Kutafuta kuishi kwa kujitenga katika ulimwengu wa kuwa na kila kitu kwa ajili ya mahitaji ya mwilini na kutaka kujiridhisha, bila ya kuwa na shauku ya kina ya ndani ya kusikia na kulitii Neno la Mungu, ni kuanguka kifudi fudi kuelekea uongo na hatima yake ni kutoka katika njia sahihi na ya utimilifu wa kinabii.

Njia dhidi ya matendo: Kama inavyooneshwa hapo juu, Israel alizijua **kazi za Mungu, lakini sio njia zake.** Neno lake linafunua njia zake. Usitamani sana matendo yake kiasi cha kushindwa kumjua Yeye [kanuni zake]. Tafuta kujua nafsi ya Mungu iliyoko nyuma ya utendaji Wake. Zijue njia zake zaidi ya kutafuta tu kuvutiwa na kazi Zake. Ujue mfumo wake wa utendaji kazi kabla ya 'kazi' za Mungu.

Zaburi 103:7. *Alimjulisha Musa njia zake, wana wa Israel matendo yake.*

Zaburi 86:10-11. *Kwa kuwa ndiwe uliye mkuu, wewe ndiwe mfanya miujiza ndiwe Mungu peke yako, Ee BWANA, unifundishe njia zako nitakwenda katika kweli yako; moyo wangu na ufurahi kulicha jina lako.*

Kukamilishwa kwa mahitaji yetu binafsi siyo lengo la kibibilia la kufukuzia. Mahitaji yote yanapatikana yenyewe kwa kadri Ufalme wa Mungu na haki yake vinatafutwa kwa shauku na kwa kupewa kipaumbele. Lengo la kweli au kusudi la mwisho ni kufikia katika ukamilifu wa taswira ya Kristo katika ulimwengu wetu na katika uwakilishi, tutende kwa niaba yake na kufikisha katika utimilifu kila agizo linalo husu makusudi Yake ya ki-ulimwengu.

Katika kufikia hili, kujiweka wenyewe chini ya unenaji endelevu wa Bwana ni jambo muhimu sana. Mtu haishi kwa mkate tu yaani siyo kuwa na tamaa kuhusu kupata mahitaji binafsi kwa ajili ya kuishi, lakini ni kwa KILA NENO LINALOTOKA katika KINYWA cha MUNGU na ni kupitia utii haina endelevu kwa maneno haya, kwamba tunashiriki na kufananishwa na asili ya Kristo ndani yetu na kwa hivyo tutakuwa tunamwakilisha Yeye ulimwenguni.

Mstari wa 1 na 2. Kumbuka kwamba amri zile walipewa Waisrael ili ‘**kuwajaribu au kuwapima**’. Katika Mwanzo 22, Mungu alimwagiza Ibrahimu amtoe dhabihu mwanawe pekee, Isaka “Wakati Ibrahimu alipoonesha utayari halisi wa kufanya hivyo, Mungu alimwambia “... sasa ninajua kwamba unamcha Mungu” [Mwanzo 22:12] Mungu anajua vitu vyote. Hakugundua kwamba Ibrahimu anamcha Yeye kwa sababu ya tendo lake la utii-Tayari alikuwa analijua - mapema katika –Mw.18:19-Mungu alishuhudia kwamba *Alimjua Ibrahimu*.

Mwanzo 18:19. *Kwa maana nimejua ya kwamba atawaamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana wafanye haki na hukumu, ili kwamba Bwana naye antimizie Ibrahimu ahadi zake.*

Pia hapa, Mungu anasisitiza kwamba ahadi alizompa Ibrahimu na familia yake zilikuwa na masharti kuhusu utii. Kwa hiyo nini lilikuwa kusudi la Mungu kwa kusema “**sasa najua unamcha Mungu**” Mungu alitaka Ibrahimu ajue mambo yanayomhusu yeye mwenyewe kwamba Mungu aliyajua kutoka kabla ya mwanzo wa nyakati. Mungu alimtaka aoneshe kwa vitendo ule ukweli kwamba, amesha fikia kiwango cha kuwa kama Mungu – Ibrahimu alitakiwa aoneshe hili. Kila mara unapo kabiliwa na jaribu linalohusu utii kwa Neno, huwi tu na fursa ya kipekee ya kulifanya hili kuwa halisi kwa kufanya kitu sahihi, lakini pia unafikia kujua vitu ambavyo tayari Mungu alikuwa anavijua kukuhusu wewe. Utii ni fursa ya kufikisha katika udhihirisho ukweli wa umilele kukuhusu wewe mwenyewe. Lakini bila ‘jaribio’ la wewe kuwekwa wazi kuhusu amri za Mungu, itakuwa vigumu kuondoka mwilini katika maisha yako na kuwa na asili ya Mungu.

Kwa mfano. Kuna watu wanakuchukia na wanaeneza uwongo kukuhusu wewe; unao uchaguzi wa kuwachukia au kuwapenda; usishawishike kuwachukia wakati Mungu anasema wapende adui zako; wakati unapowapenda unaweka asili yako ya Kimbingu katika maonesho; hivyo kimatendo unajaza katika maisha yako asili halisi ya Mungu.

[Kando] Vivyo hivyo wakati Mungu alipo muuliza Adamu baada ya kutenda dhambi “uko wapi?”- haimaanishi kwamba Mungu hakujua alikokuwa. Hakika Mungu alikuwa anajaribu kumfanya Adamu atambue pale alipo kuwa amewekwa ndani ya mahusiano na Yeye mwenyewe kipekee sasa baada ya kutenda dhambi.

Utii wa mwana kwa neno utajaribiwa /utapimwa:

Yesu alijaribiwa:

Waebrania 5:7-9

- 7. Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwoko na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu;*
- 8. na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata*
- 9. naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanamtii;*

Yusufu alijaribiwa:

Zaburi 105:19. *Hata wakati wa kuwadia neno lake, ahadi ya Bwana ilimjaribu.*

Utii kwa neno ni fursa ya kushiriki na kuonesha asili ya Mungu.

Mungu aliweza siku moja kumtoa dhabihu mwana wake wa pekee kama vile Ibrahimu alivyo mtoa dhabihu wa kwake. Utii kwa Neno huturuhusu sisi kuwa washiriki katika asili ya Mungu-tunafanyika kuwa kama Yeye - Neno lilifanyika mwili. Ibrahimu kupitia utii wake, alionyesha tu kitu kilichokuwa tayari kipo ndani ya mfumo wa asili ya Mungu na ndicho kiini kwa makusudi yake ya milele - uwezo wa kutomzuilia mwanawe wa pakee.

Linganisha mistari hii miwili ifuatayo:-

Ibrahimu Mwanzo 22:12. *Akasema Usimnyooshee kijana mkono wako, wala usimtende neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee” [NASB]*

Mungu Warumi 8:32. *Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?*

Kila tendo la utii hufungua ndani yetu vipengele ambavyo tayari ni vya asili ya Mungu. Tunavyo tayari. Utii ndio unaoviweka wazi kwetu. Mungu anavijua tayari. Anataka kuufanya ukweli ujulikane kwetu ambao kwa huo tayari ameutungisha mimba kwetu, kupitia kuachiliwa kwa amri yake [Neno] kwetu.

Moja kwa moja kupitia unenaji wa Mungu kwa Ibrahimu, ‘aliitikia kwa kusema ‘niko hapa’. Mungu ndiye “**NIKO**”. Wakati Ibrahimu alipoitika “**NIKO Hapa**” anaonesha uthamani uliyo ndani Yake, kwamba ndivyo alivyo kama Mungu. Uendelevu katika hili ulimwezesha yeye kujihusisha na kutii amri ngumu ya Mungu – ya kumtoa mwanawe wa pekee.

Kwa namna yoyote huu ulikuwa ni upeo wa kitu fulani ndani ya Ibrahimu kwamba alifanyika mfano, na hapo alisogea karibu zaidi kuwa kama Mungu, tena kwa Neno la Mungu na amri zake huipalilia ile asili ya Mungu ndani yetu.

Kwa kiasi, huu ulikuwa upeo wa kitu fulani ndani ya Ibrahimu ambacho kilimtengeneza, kiasi kwamba alisogea karibu zaidi ili awe kama Mungu. Tena – utii kwa Neno na amri za Mungu hupalilia asili ya Mungu ndani yetu.

Kama inavyo oneshwa katika somo lililopita Ibrahimu alimtambua Mungu kama Yehova Yire. Kipengele kipya kabisa cha asili ya Mungu kinafunuliwa kwake kwa sababu ya utii wake, na pia aliingia katika kumfahamu Mungu kama ‘Mpaji’- Kumfahamu Mungu kulikuwa muhimu kwa ajili ya muhula mrefu wa utimilifu wa ahadi ya awali ambayo Mungu alimpa *kuwa ‘Baba wa mataifa’*.

Tendo hili la utii sasa linamfanya Mungu kufanya ahadi isiyotenguka kwa Ibrahimu.

Mwanzo 22:16-18

16. *akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,*

17. *katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zako;*

18. *Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.*

Baraka, ruzuku, utoaji n.k. ni matokeo ya asili ya utii kwa Neno la Mungu linalo tumwa kwetu. Tunajilisha kwa Neno hili kwa kulitii. Tunaishi kwa amri za Mungu. Hili linatustawisha na kutuchochea tusonge mbele katika Mungu na katika hatima yake ya kinabii inayo ambatana na maisha yetu.

'KILA' NENO

Neno la Mungu linawakilisha ufunuo wa Mungu na makusudi yake kwa mwanadamu, ikiwa ni pamoja na Agano la Kale na Agano Jipya. MAANDIKO YOTE yamevuviwa na Mungu Mwenyewe.

2Timoteo 3:16: *Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki;*

Vuviwa yaani theopneustos likiwa na maana yapulizia ndani Ki-Uungu, vuviwa na Mungu.

Yohana 6:63. *Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu, maneno hayo niliyo waambia ni roho, tena ni uzima.*

Roho au **pneuma** likiwa na maana ya *mkondo wa hewa*, hiyo ni, *pumzi [mlipuko] au upepo mwanana.*

Neno la Mungu lina uzima wa Mungu ndani yake. Maneno yake ni Roho na uzima. Yamevuviwa na Mungu Mwenyewe. Mtu hawezi kuwa na uumbikaji wowote wa upeo wa 'Roho' bila ya kuwa na sehemu ya utajiri wa Neno. Hili linafafanuliwa kwa nguvu sana katika kitabu cha Mwanzo kuhusu uumbaji.

Mwanzo 1:1-3

1. *Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi,*
2. *Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, Roho ya Mungu ikatulua juu ya uso wa maji*
3. *Mungu AKASEMA, Iwe nuru, ikawa nuru.*

Agano la Kale limevuviwa na Mungu.

2Petro 1:20-21

- 20 *Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.*
21. *Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*

[Soma pia. **Kutoka 4:12; 2Samweli 23:2, Yereimia 1:7 na 9]**

Uthamani wa Agano la Kale

Mara nyingi imesemwa kwamba Agano la Kale ndio Agano Jipya lililofichwa; na Agano Jipya ndio Agano la Kale lililofunuliwa. Wakati Paulo alipo andika 2Timoteo 3:16, kuwa "KILA ANDIKO LENYE PUMZI YA MUNGU"Maandiko halisi aliyorejea hapa, yalikuwa ni Agano la Kale, ingawa mengi tunayotilia maanani kama ndio Agano Jipya lilikuwa halijaandikwa.

Katika Luka 24 kwa wanafunzi wake wawili walio kuwa njiani kwenda Emau, Yesu alijielezea mwenyewe, yaani alijionesha mwenyewe kutoka katika Torati, Manabii na Zaburi, istilahi ambazo ni muhimu kwa rejea ya Agano la Kale lote. Kwa kufanya hivyo, Yesu alionesha umuhimu na uhusiano wa Agano la Kale.

Luka 24:27. *Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyo mhusu yeye mwenyewe.*

Luka 24:44-47

44. *Kisha akawaaambia, haya ndiyo maneno yangu niliyo waambia nilipo kuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyo andikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii, na Zaburi.*

45. *Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.*

46. *Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*

47. *na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

Mengi ya Agano la kale yanashughulika na mwingiliano wa Mungu na taifa la Israeli ambalo lilikuwa na mpangilio wa makabila. Maingiliano haya yanawasilisha mafunzo muhimu na yenye nguvu kwetu leo. Paulo alitoa hoja kwamba, nyaraka zote za historia ya kiroho ya Israel kama ilivyo andikwa kwa ajili yetu katika Agano la Kale; zinapaswa zijifunzwe kwa makini kwa sababu kila kitu kilichotokea kwao kilikuwa kabisa ni mpango ulioratibiwa wa Ki-Uungu na kwamba matukio na mwitikio wake vilitokea kama mfano kwetu.

Warumi 15:4. *Kwa kuwa yote yaliyo tangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi, ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.*

1Wakorinto 10:1-11 [NJV]

1. *Kwa maana, ndugu zangu, sipendi mkose kufahamu ya kuwa baba zetu walikuwa wote chini ya wingu; wote wakapita kati ya bahari;*
2. *wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari;*
3. *wote wakala chakula kile kile cha roho;*
4. *wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo.*
5. *Lakini wengi sana katika wao, Mungu hakupendezwa nao; maana waliangamizwa jangwani.*
6. *Basi mambo hayo yalikuwa mfano kwetu, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyo tamani.*
7. *Wala msiwe waabudu sanamu, kama wengine wao walivyokuwa; kama ilivyo andikwa, watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama wacheze.*
8. *Wala msifanye uasherati, kama wengine wao walivyofanya, wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu.*
9. *Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyo mjaribu, wakaharibiwa na nyoka.*
10. *Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyoning'unika, waka hairibiwa na mharibu.*
11. *Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani.*

1Kor 10:11 [NASB] Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani.

[AMP] Basi mambo hayo yaliwaangukia wao kwa jinsi ya [mifano na maonyo kwetu] yaliandikwa kuturudi na yanatufaa sisi kwa hatua njema kwa maelekezo sahihi, sisi katika siku zetumiisho yetu imefikia kilele chake [kilele chake na kipindi cha kukamilisha]

Mfano au tupos maana yake ni:-

- (i) Alama, chapa, wazo
- (ii) Umbo, sura
- (iii) Mfano wa awali, mwelekeo, mpangilio.

Kitamathali (kiumbo) ni kielelezo, mfano wa kuigwa, kufuatwa [Wafilipi 3:17, 1Watesal. 1:7, 2Watesal. 3:9, 1Timo 4:12; Tit 2:7; 1Pet 5:3] kwa ajili hiyo pia ni kuasa, kuonya, onyo [1Wakor. 10:6na 11] **Zodhiates:** mafunzo ya maneno kwa ukamilifu. [Ukisoma kamusi iitwayo:-**The complete word study Dictionary- Kamusi ya kujifunza maneno kwa ukamilifu**] utaona inatupa ufafanuzi wa ziada wa neno ‘**tupos**’

Tupos maana yake ni **aina** kama mfano wa baadhi ya **kweli** ambazo bado zilikuwa **hazijajitokeza au sampuli** ya kitu ambacho kilikuwa **bado kuendelezwa na kukua**. Kwa mfano, amri na sheria katika Agano la Kale zilivyokuwa katika asili yake ya ndani. Aina za Agano Jipya. Zama za kwanza zinatumika kama aina ya zama za pili. Hata hivyo mpaka au umbo asili au kifani cha baadhi ya kweli ambazo bado kujitokeza ziliitwa **tupos**.

Hata hivyo Agano la Kale lina miongozo, aina, vifani n.k ambayo vinatupa picha ya uhalisia muhimu zaidi ambao unapaswa kutambuliwa na Kanisa, katika Agano Jipya.

Hivyo katika kutafuta kufanyika yote ambayo Mungu ameandaa kwa ajili yetu na kuelewa asili ya njia zake na ufalme wake, tunapaswa kujifunza Agano la Kale kwa uangalifu sambamba na Agano Jipya.

1Wakor.10:11. Unadokeza kwamba ‘**Ule mwisho wa wakati**’ umeshalijia kanisa, yaani, wewe na mimi. Maingiliano ya Mungu na wanadamu katika Agano la Kale yalikuwa ni ‘**tupos**’- ni mfano ulioandikwa kwa makusudi na faida yetu.

Shughuli na mabadiliko haya ya binadamu ya Ki-Uungu yalisanifiwa kwa makusudi kwa ajili ya maonyo na maelekezo kwetu, ili yatumike kutuonya sisi. Ni juu yetu, katika wakati wetu, mapenzi ya Mungu yapate wakati wa kufikia upeo wa kilele cha juu kabisa au ukomavu kamili. Ikiwa hivi ndivyo, basi, hatutawezi kulidharau Agano la Kale.

Katika fikra za Mungu, ikiwa sisi ndio tunaotaka kuwa watu watakao fikisha mapenzi yake yote kufikia ukamilifu katika wakati wetu, basi tunapaswa kuwa kizazi tendaji, chenye ufahamu na kwa msimamo, kuruhusu kanuni za Kibiblia za Ki-Uungu zilizomo ndani ya Agano la Kale zitengeneze mawazo na tabia zetu. Kwa kweli, kwa pamoja Agano la Kale na Agano Jipya- **MAANDIKO YOTE**- yana uhai na yana husika kwa ajili ya kutu harakisha tuingie katika ukomavu binafsi na wa pamoja, na katika hitimisho la kusudi lote la Mungu kwa dunia yote.

Ukomavu wetu ndani ya ukamilifu wa sura ya Kristo kupitia mtindo wa kupokea maonyo na maelekezo kwa kujifunza kwa Israel kama mfano, pia ilikuwa ni sehemu ngumu ya

kukamilisha makusudi ya Mungu kwa kila mmoja wa watakatifu wa Agano la Kale. Maandiko yana tufundisha wazi wazi kwamba, bila ya sisi kuyatii, hayata weza kukamilishwa kwetu.

Waebrania 11:39-40. *Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; 40. kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.*

Zingatia mst 40 (b) ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

Waandishi wengi wa Agano Jipya walitumia **kumbukumbu za kimaandiko** na au /**tafiti** kutoka **Agano la Kale** ili kufafanua jambo au kanuni.

Kwa mfano. Mtume Paulo alifundisha kanuni za utii na imani akitumia mfano wa Ibrahimu-soma Warumi 4. Hapa pia ‘anatumia sisi tufuate hatua za imani za baba yetu Ibrahimu’ (Warumi 4:12) -yaani tufuate mfano wake. Hili kwa asili litatumia kuchunguza maisha ya Ibrahimu kama yalivyoandikwa katika kitabu cha Mwanzo.

Ninashawishika kusema kwamba, kamwe mtu hatafikia utimilifu wa kiroho ikiwa atadharau Agano la Kale.

Zaburi 119:160. *Jumla ya neno lako ni kweli, na kila hukumu ya haki yako ni ya milele.*

Yesu aliongezea uthamani katika Agano la Kale kwa kueleza kwamba, Yeye hakuja kuitangua Torati na manabii ila kuitendea kazi katika mtindo wake wa maisha ili watu waone ni kwa namna gani wanavyoweza kuikamilisha.

Matayo 5:17-20

17. *Msidhani kuwa nilikuja kuitangua torati au manabii; la, si kutangua, bali kutimiliza.*

18. *Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapo ondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.*

19. *Basi mtu yeyote atakaye vunja amri moja kati ya hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakaye zitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.*

20. *Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.*

Yohana 5:46-47

46. *Kwa maana kama mngali mwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu.*

47. *Lakini msipo yaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?*

Petro anatutahadharisha tukumbuke maneno yaliyonenwa na manabii wa Agano la Kale.

2Pet 3:1-2

1. *Wapenzi, waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi; katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa kuwakumbusha,*

2. *mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na ile amri ya Bwana na mwokozi iliyoletwa na mitume wenu.*

‘NENO LITOKALO’

Kumb 8:3b. *apate kukujulisha yakuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA.*

Litokalo’= motsa’/motsa’= *kwenda mbele, hilo ni (tendo), haki ya kutoka [mahali penyewe] au pa kutokea, tendo au mahali pa kutokea nje au mbele, toa, safirisha, chanzo, tokeza.*

Neno litokalo ni neno ambalo **linalotujia sasa**. Likiwa linatujia au kuruka kuchupa kuelekea mbele kutoka kinywa cha Mungu. *Mtu hataishi kwa mkate tu ila kwa neno ambalo ni jipya linalokuja [chupa, ruka] kutoka katika kinywa cha Mungu likiwa linaelekezwa kwenye kanisa lenye mshikamano au kwako kama mtu binafsi.* Wengi wanaita neno hili kama, ‘ukweli’ wa sasa. Hitaji la Ki-Uungu kila wakati siyo tu **KUUJUA** ukweli wa sasa, ila ni **kujengwa** katika ukweli wa sasa yaani ukweli unaokuja kwetu kutoka kwa Mungu.

2Pet 1:12. *Kwa hiyo, nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo siku zote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo.*

Matayo 4:3-4

3.Mjaribu akamjia akamwambia, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate”

4.Naye akajibu akasema, Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.

Yesu alihamishia mtazamo hapa kutoka njaa ya kawaida hadi njaa ya kiroho. Mtu haishi kwa mkate peke yake ila kwa kila Neno la RHEMA lililotoka katika kinywa cha Mungu. Ni muhimu kabisa mtu awe na njia ya kufikia unenaji wa Mungu wa sasa. Ili kuwa mhusika kamili wa kiroho, na uanze kikamilifu kuwa mtendaji kama mtu mwakilishi wa Mungu na katika utekelezaji wa mapenzi yake, unapaswa kujiunganisha na baba mwenye neema ya kitume iliyo imara na halisi; ili kutoka kwake uwe unapokea neema kupitia ukweli uliopo na neno bichi (jipya) la sasa.

**MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA
KIKUNDI.**

1. Ni nini kiashiria au ushahidi kwamba Mungu amesahauliwa? [kumb 8:11]
2. Jadili namna ya kujishughulisha na kumpatia mtu mwenye shida mahitaji yake bila ya kuanzisha upendo kwake na utii kwa neno la Mungu na namna inayoweza kuwa sababu ya kifo cha kiroho.
3. Ni kwa kuzingatia nini kuwa, Neno la Mungu au amri zake zina TUPIMA? Kwa upande wako tilia maanani pia namna Mungu alivyompima [jaribu] Ibrahimu kwa kumpa amri ngumu.
4. Hatupaswi kujifunza Agano la Kale, ni Agano Jipya tu. Kanusha usemi huu kwa ushahidi wa kibiblia. (Kanusha=kuthibitisha kitu kuwa na makosa)
5. Ni nini maana muhimu ya LITOKALO katika usemi :- “Mtu hataishi kwa mkate tu ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu”
6. Katika mistari 176, mwandishi wa Zaburi 119 anaelezea shauku yake kwa neno la Mungu na pia anaelezea nguvu na faida. Zaburi 119 kwa sehemu kubwa ni rejea kwa vitabu vitano vya kwanza vya Biblia. Soma Zaburi hii taratibu na kwa kutafakari kwa siku 10 zaidi, huku ukiwa una nukuu...
 - a. Maelezo mbalimbali yanayohusu kufurahia au kulipenda Neno.
 - b. Matokeo na faida mbalimbali za Neno.
 - c. Njia mbalimbali [vifungu vya maneno au istilahi] ambazo kwa hizo Neno la Mungu linaweza kufafanuliwa.
 - d. Tumia muda wa kutoa shukrani kwa kila ulichosoma, shukuru na msifu Mungu kwa Neno lake lenye nguvu.

KUMFUNUA KRISTO KUTOKA KATIKA MAANDIKO.

Lengo: Ufunuaji wa Ki-Uungu kwa kumwonesha Kristo kutoka katika Neno la Mungu.

SAFARI NDEFU YA KI-UUNGU KUELEKEA UFUNUAJI WA KI-UUNGU.

LUKA 24:1-53

1. *Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari.*
2. *Wakalikuta lie jiwe limevingirishwa mbali na kaburi,*
3. *Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu.*
4. *Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo, tazamawatu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta*
5. *Nao walipoingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia kwanini mnamtafuta aliye hai katika wafu?*
6. *Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyo sema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya*
7. *akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulubiwa na kufufuka siku ya tatu*
8. *Wakayakumbuka maneno yake.*
9. *Wakaondoka kaburini, wakarudi; wakawaarifu wale kumi na mmoja na wengine wote habari za mambo hayo yote.*
10. *Nao ni Mariamu Magdalene, na Yoana na Mariamu mamaye Yakobo, na wanawake wengine waliokuwa pamoja nao*
11. *.hao waliwaambia mitume habari ya mambo hayo.*
12. *Maneno yao yakaonekana kuwa kama upuzi kwao, wala hawakuwasadiki. Lakini Petro aliondoka akaenda mbio hata kaburini, akainama akachungulia ndani, akaviona vile vitambaa vya sanda tu; akaenda zake akiyastajabia yaliyo tukia.*
13. *Na tazama siku ileile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emmau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.*
14. *Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yaliyotukia*
15. *Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia akaandamana nao.*
16. *Macho yao yakafumbwa wasimtambue.*
17. *Akawaambia, ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea? Wakasimama wamekunja nyuso zao.*
18. *Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, je wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yalitotukia humo siku hizi?*
19. *Akawauliza, mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kunena na kutenda mbele za Mungu na watu wote;*
20. *Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyo mtia katika hukumu ya kufa, wakamsulubisha.*
21. *Nasi tulikuwa tukitumaini kuwa yeye ndiye atakaye wakomboa Israel. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;*

22. *tena, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha , waliokwenda kaburini asubuhi na mapema.*
23. *wasiuone mwili wake; wakaja wakasema yakwamba wametokewa na malaika waliosema kwamba yu hai.*
24. *Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyo sema, ila yeye hakumwona.*
25. *Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyo yasema manabii.*
26. *Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?*
27. *Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyo mhusu yeye mwenyewe.*
28. *Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele,*
29. *Waka mshawishi wakisema, kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao.*
30. *Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.*
31. *Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua kisha akatoweka mbele yao.*
32. *Wakaambiana, je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?*
33. *Wakaondoka saa ileile, wakarejea Yerusalemu, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na wale waliokuwa pamoja nao,*
34. *Wakisema, Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea simoni.*
35. *Nao waliwapa habari ya mambo yale ya njiani, na jinsi alivyo tambulikana nao katika kuumega mkate.*
36. *Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, amani iwe kwenu.*
37. *Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho.*
38. *Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwanini mnaona shaka mioyoni mwenu?*
39. *Tazameno mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.*
40. *Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake.*
41. *Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula chochote hapa?*
42. *Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa.*
43. *Akakitwaa akala mbele yao.*
44. *Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyo waambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyo andikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*
45. *Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.*
46. *Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;*
47. *na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*
48. *Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.*
49. *Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.*
50. *Akawaongoza mpaka Bethania, akainua mikono yake akawabariki.*

51. *Ikawa katika kuwabariki, alijitenga nao; akachukuliwa juu mbinguni.*

52. *Wakamwabudu; kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu,*

53. *Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu.*

Tuna badilishwa ili tufanane na mifano ya sura yake ambayo anaiweka wazi kwetu (2Wakorinto 3:18). Kwa kadri tunavyo tazama ndivyo tunavyo badilishwa. Uwakilishi wetu kwa niaba Yake ni lazima ufanyike kwa usahihi zaidi, kwa usafi wa ndani sana na kwa kukubali kukabiliana na ufunuo wa Nafsi yake kupitia Neno lake.

Katika Luka 24, mna kanuni muhimu kwa ajili ya kuifikia asili ya Kristo kupitia Neno Lake. Mna kanuni za msingi ambazo zinawezesha kufunuliwa kwa Kristo kwetu.

Ni masharti gani yanayo tupa mpenyo wa kufikia kile alichoko na shauku ya kutuonesha Yeye mwenyewe?

KANUNI ZENYE DONDOO.

MSHIKAMANO- MUKTADHA KWA AJILI YA KUJIFUNUA

Ona kwamba kulikuwa na wanafunzi WAWILI

Yesu alijifunua mwenyewe kwa wanafunzi hawa wawili kupitia maandiko. Muktaadha aliotumia kufanya hili ulikuwa ni mmoja wa ‘makubaliano.’

Tarakimu **mbili** [2] ni alama ya ‘makubaliano’, ‘ushahidi’ au ‘ushuhuda’.

Amos 3:3 NKJV: *Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?*

Hali ya mshikamano na makubaliano ndio iliyo bora zaidi yenye maadili mema na yenye kutengeneza mazingira ya ndani ambayo Neno la Mungu lina fasiriwa kwa urahisi na kwa kufanya hivyo, Kristo anaonekana.

Sikiliza ushuhuda wao:-

Luka 24:32 [NASB] *Wakaambiana, je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?*

[KJV] *Wakaambiana wao kwa wao, je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu wakati alipokuwa akizungumza nasi tulipokuwa njiani, na wakati anatufunulia maandiko?*

Zingatia watu wawili walikuwa na moyo mmoja- ni kiashirio cha kwenda kama mmoja- umoja [mshikamano] kamili na wenye mapatano /mabadiliko.

Chini ya mchakato wa matengenezo ya Nehemia, Ezra, mwandishi alisema na kutoa ufafanuzi/ uelewa kutokana na sheria ya Musa kwa mara sita [sawa na robo ya siku]

Ninaamini kilicho sababisha utulivu kuwepo na jambo hilo kufanyika, ni kwa sababu watu walijikusanya kama mtu mmoja.

Nehemia 8:1 *Na watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la maji, wakamwambia Ezra, mwandishi, akilete kitabu cha torati ya Musa, Bwana aliyowaamuru Israel.*

Kwa watu kusimama kwa muda mrefu kiasi kile ili kujihusisha na Neno la Mungu, ni jambo la kiroho/la ki-Uungu.

Fundisho hapa ni: Hali ya mshikamano inawezesha kusanyiko la wana wa Mungu kufikia kipimo cha kipekee cha neema kuvuka mipaka ya ukomo wa mwili na akili wa kuhimili uchovu ili kwa makini waweza kupokea na kwa intelijensia, waweze kuelewa na kisha kwa kufahamu watii kweli za maana zinazotokana na Neno la Mungu.

Mgongano, mafarakano, mpasuko, kutokuwa na muafaka n.k huwa kikwazo dhahiri cha kutoachiliwa kwa kina, ufunuo muhimu na wa sasa kutoka Neno la Mungu. Mungu hataachilia vipande vya Neno vilivyo hifadhiwa katika hazina yake kwa nyumba iliyofarakana.

Pia zingatia maandiko haya yafuatayo:

2Mambo ya Nyak 30:12 *Tena katika Yuda mkono wa Mungu ulikuwa ukiwapa moyo mmoja, waitimize amri ya mfalme na wakuu kwa neno la BWANA.*

Mdo 2:46 *Nasiku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula kwa furaha na kwa moyo mweupe.*

Mdo 4:32 *NaNa jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja, wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alichu nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika.*

Angalia hili:- Mahali palipo jengwa hali ya mshikamano imara wenye makubaliano katika roho ambamo ndimo Neno la Mungu linapo pokelewa, basi uwezekano wa kuenea kwa utii wa pamoja huwa dhahiri.

Hagai 1:12 *Ndipo Zerubabeli mwana wa Shealtieli, na Yoshua mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, pamoja na hayo mabaki yote ya watu, wakaitii sauti ya BWANA, Mungu wao na maneno ya Hagai nabii kama Bwana Mungu wao alivyomtuma, nao watu wakaogopa mbele za BWANA.*

Kutoka19:8 *Watu wakaitika pamoja wakasema, hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda. Naye Musa akamwambia BWANA maneno ya hao watu.*

1. HAMU YA KUJUA NA KUELEWA MAJIRA.

Ukweli, kati ya nyingi ambayo iliwaimarisha wanafunzi hawa wawili, ilikuwa kule **kujihusisha kwa kumaanisha na shauku ya kufahamu na kuelewa maana ya kiroho na namna wangehusika na majira** ambayo walijikuta wenyewe wamo. Yesu alikuwa ameshakufa, lakini walikuwa hawajui alishafufuka kutoka kwa wafu na alikuwa hai.

Luk 24:14 Unaonesha kwamba “**walikuwa wakizungumza wao kwa wao kuhusu mambo yote yaliyotokea**”- hili linatupa picha kuwa hayakuwa ni mazungumzo mepesi tu ya kithiolojia, lakini ni shauku makini ya kufahamu ni nini Mungu anachoshughulika nacho ulimwenguni kwa wakati uliopo hivi sasa.

Wale ambao mnafuatana kwa karibu lazima wawe na mzigo unaotokana na shauku yenye nguvu ya kujua na kuelewa majira tunayoishi ili mienendo yenu hatimaye iweze kuhusika sawa sawa na anachohitaji Mungu.

Usiambatane na mtu ambaye mnatofautiana kiroho katika saa hii muhimu tunayoishi sasa. Ukosefu wao wa kuwa na utambuzi na wepesi vitatafsiriwa kuwa ni mtindo wa tabia na siyo kushikilia anachotaka Mungu kwa majira hayo. Vile vitu ambavyo wewe unavipa heshima hakutakuwa tena na kipaumbele kwa ajili yake.

1Mambo ya Nyak 12:32 *Na wa wana wa Isakari, watu wenye akili za kujua nyakati kujua yawapasayo Israel wayatende, vichwa vyao walikuwa watu mia mbili na ndugu zao wote walikuwa chini ya amri zao.*

Ikiwa utayajua majira, utajua na cha kufanya. Kukosa kuyajua majira hutafsiri tabia na shughuli zako kuwa siyo halali na siyo sahihi. Zaidi bado utaangukia katika hali ya kuwa na misisimko hasi. Wale wanafunzi wawili walikuwa na ‘huzuni’ kwa kufikiria kwamba Yesu hakuwa hai.

Zingatia la pembeni.

Hagai 1:2-11

2. *Bwana wa Majeshi asema hivi, ya kwamba, Watu hawa husema, Huu sio wakati utupasao kuja, huu sio wakati wa kujenga nyumba ya BWANA.*
3. *Ndipo neno la bwana lilikuja kwa kinywa cha Nabii Hagai, kusema,*
4. *je! huu ndio wakati wa ninyi kukaa katika nyumba zenye, mapambo ya mbao, iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika?*
5. *Basi sasa, Bwana wa Majeshi asema hivi, Zitafakarini njia zenu.*
6. *Mmepanda mbegu nyingi mkavuna kidogo; mnakula lakini hamshibi; mnakunywa lakini hamkujazwa na vinywaji; mnajivika nguo lakini hapana aonaye moto; na yeye apataye mshahara apata mshahara ili kuutia katika mfuko ulio toboka-toboka.*
7. *Bwana wa majeshi asema hivi, zitafakarini njia zenu.*
8. *Pandeni milimani mkalete miti, mkaijenge nyumba; nami nitaifurahia, nami nitatukuzwa, asema BWANA.*
9. *Mlitazamia vingi, kumbe vikatokea vichache; tena mlipovileta nyumbani nikavipeperusha. Ni kwa sababu gani? asema Bwana wa majeshi. Ni kwa sababu ya nyumba yangu inayokaa hali ya kuharibika, wakati ambapo ninyi mnakimbilia kila mtu nyumbani kwake.*
10. *Basi, kwa ajili yenu mbingu zimezuiliwa zisitoe umande, nayo nchi imezuiliwa isitoe matunda yake.*
11. *Nami nikaita wakati wa joto uje juu ya nchi, na juu ya milima, na juu ya nafaka, na juu ya divai mpya, na juu ya mafuta, na juu ya kila kitu itoacho nchi, na juu ya wanadamu, na juu ya wanyama, na juu ya kazi zote za mikono.*

Kazi **zisizopasa** zinatokana na kushindwa kufahamu majira [wakati] na kutojua ni nini cha kufanya. Katika siku ya Hagai, watu walitawaliwa na kitu kisichofaa [kujenga nyumba za paneli] katika wakati ambao hekalu la pamoja lilipaswa kupewa kipaumbele. Matokeo yake uchumi wao ukaporomoka. Mafanikio yatakuwa mengi mahali ambapo watu wa Mungu wameelekeza nguvu zao na kufanya juhudi kwa kile ambacho ni cha msingi katika moyo wa Mungu kwa kila majira kwa wakati. Neno la unabii la BWANA lingali linalijia kanisa lake na linasema; *Tafakarini njia zenu.*

- ‘Nyumba za paneli dhidi ya hekalu’ mtazamo huu unaweza kutumiwa katika viwango vingi tofauti.
- Nyumba ya paneli=kanisa la mahali; Hekalu=Kanisa la Jiji.
- Nyumba ya paneli=kutawaliwa na shughuli binafsi za siri na kunai makuu;

Hekalu maana yake ni *kutawaliwa na umoja na ukuaji wa kanisa (familia)*.

2. KUSOGEA KARIBU NA BWANA: UFUNULIWAJI WA KI-UUNGU UNAHITAJI UKARIBU WA KI-UUNGU.

Ufunuliwaji unahitaji ukaribu ulio jirani, haitokei kutoka mbali. Angalia jinsi Yesu alivyosogea karibu na wale wanafunzi wawili ambao walikuwa WANAJADILIANA kuhusu matukio ya wakati wao.

Luk 24:15 *Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.*

Jadiliana au Suzeteo lina maanisha:-*kuchunguza kwa pamoja, huko ni kujadili, kubishana, kusaili, kuhoji (kwa) maswali (na) kutoa sababu, (kwa pamoja).*

Kumbuka katika somo la kwanza: Baba na Mwana hujifunua wenyewe kwa wale wanaojihusisha na MCHAKATO wa kulisikiliza Neno na kutii.

Yohana 14:21. *“Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake”*

Mungu anavutiwa na Neno lake. Mahali ambapo Neno Lake linasikilizwa na kulitii, Yeye husogea karibu na kujifunua mwenyewe. Pia mahali penye mjadala wenye mtazamo kuhusu Neno na njia zake, Yeye hukaribia ili aende pamoja nawe katika kujifunua Yeye mwenyewe kwako.

Malaki3:16a[KJV] *Ndipo wale waliomcha BWANA waliposemezana wao kwa wao ...*

Malaki 3:16-18 [NASB]

16. *Ndipo wale waliomcha BWANA waliposemezana wao kwa wao. Naye BWANA akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha BWANA, na kulitafakari jina lake.*

17. *Nao watakuwa watu wangu, asema BWANA wa majeshi, katika siku ile niifanyayo; naam, watakuwa hazina yangu hasa; nami nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye.*

18. *Ndipo mtakaporudi, nanyi mtapambanua kati ya wenye haki na waovu, na kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia.*

3. BIDII YENYE SHAUKU KWA AJILI YA NENO LA MUNGU.

Watu wawili waliokuwa na moyo mmoja walikuwa wakisafiri pamoja kuelekea mahali palipokuwa pakijulikana wazi, kijiji cha Emau. Jina la mahali, huwakilisha *tabia katika roho*. Maana moja ya jina ‘Emau’ ni ‘**ari ya kuhitaji**’. Maana nyingine ya neno Emau ni ‘**chemchemi za moto**’.

Amosi 3:3. NASB: *Je, watu wawili wanaweza kutembea pamoja ispokuwa wapeana ahadi?*

AMP: *Je, wawili wanaweza kutembea pamoja ispokuwa wameahidiana na kuwa na makubaliano?*

MSG: *Je, watu wawili waweza kutembea na kushikana mikono ikiwa hawaendi mahali pamoja?*

NLT: *Inawezekana watu wawili wakatembea pamoja bila ya kukubaliana uelekeo?*

Ni jambo la muhimu kwenda na wale ambao wana shauku ile ile kama yako. Watu hawa walikuwa na lengo la kufika mahali pa kiroho penye tabia ya ARI ya kuhitaji. Hili linazungumzia shauku kali. Kiunabii, lina ashiria kwetu hitaji la KUFURAHIA Neno la Mungu tukiwa na utulivu makini kufikia kiwango cha kuwa, hakuna chochote kitakacho vuruga upendo wetu kwa Mungu kupitia kulipenda Neno lake. Ilikuwa ni kule Emau ambapo Yeye Kristo alitambuliwa nao baada ya kuumeza mkate na baada ya kujieleza Mwenyewe kutoka kwenye maandiko hadi kufikia kiwango kile. Ujifunuaaji wa Mungu hufanyika ndani ya muktadha wa shauku imara. **Shauku ya ki-uungu ndiyo udongo wenye rutuba kwa ajili ya ujifunuaaji wa Ki-uungu au shauku kwa ajili ya Uungu amba huwezesha ujifunuaaji wa ki-uungu. Hakuna shauku- hakuna kufunuliwa.**

4. USIKATE TAMAA- DUMU KATIKA NENO:

Safari hadi Emau ilikuwa ya umbali wa maili saba. Kwa istilahi ya kiyunani ‘stadia’ iliyotafsiri neno ‘maili’ inalinganisha kama ni kati ya kilometa 10.4 hadi km 12 kutegemeana na neno stadia linafafanua kitu gani. Walitembea kwa kisio la km 12 kutoka Yerusalemu hadi Emau. Kwa vyo vyote vile ni matembezi marefu- na tunaweza tukayaita matembezi haya, safari Ndefu ya kwenda Kujifunua. Tendo hili linahitaji juhudi na kujipa moyo. Hatupaswi kupoa katika ufukuziaji wetu wa kila siku, wa kumtafuta Bwana, baada ya kumfahamu Kristo kikamilifu zaidi kupitia ufunuo wake Mwenyewe katika Neno lake. Ni lazima uwe na upendo endelevu na wenye msimamo na mapenzi makali kwa Neno la Mungu. Usiupoteze ‘upendo wako wa kwanza’- ambao ni upendo kwa Neno la Mungu.

Pia zingatia kuwa hawa wanafunzi wawili walirudi Yerusalemu kuwapa taarifa wanafunzi wenzao kuhusu kufunuliwa kwa Kristo kwao. Nina hisi huenda walikwenda wakikimbia kilometa zote kumi na mbili kwa furaha walipokuwa wanarudi.

[Zaburi 119:32](#) Nitakwenda mbio katika njia ya maagizo yako utakapo nikunjua moyo wangu.

Wale wanafunzi wengine walikuwa bado katika hali ya kutokuamini na kukandamizwa. Yesu hakuwakaribia wao kwanza ili ajifunue Yeye ni nani, bali kwa wanafunzi wawili, ambao ingawa pia mwanzoni walikuwa wamehuzunishwa namatukio ya majira yao na kuvunjwa moyo kutokana na kutokuamini kuhusu kufufuka Kwake, walichagua kutobakia kuwa mapooza katika hali ya sinto fahamu(uzito), bali waliamia katika kuendelea kutafuta, kutunza na kuimarisha shauku yao kwa ajili ya Mungu.

5. SHIKILIA KWA NGUVU MBEBAJI WA NENO LA MUNGU.

Wale wanafunzi wawili walishuhudia kuwa mioyo yao ilikuwa inawaka ndani yao, wakati Yesu aliponena maandiko kwao; kisha wakati Yesu alipofanya kama anasonga mbele kupita Emau, walimsihi akae pamoja nao. Hili lilikuwa jaribio kwao. Yesu alikuwa akichunguza kwa makini ili aone kwa usahihi walivyokuwa makini- walikuwa na njaa kiasi gani kwa ajili ya Neno lake. Walikataa kumwachia Yeye aende, hata ingawa walifikia hatua ile hawakunjua kuwa ndiye Yeye Kristo mfufuka.

BWANA aliheshimu shauku hii motomoto- na akajifunua yeye ni nani wakati mkate unamegwa. Mkate ni alama ya neno la Mungu. Wakati neno linafunguliwa, kumegwa na kuenezwa ndani ya utamaduni ambao unalipa heshima ya hali ya juu, kuthaminiwa, kuaminiwa kwa umakini wa hali ya juu na kumshikilia vizuri mtu yule ambaye kupitia yeye Neno

linagawiwa, HATIMAYE ufunuo wa Mungu unaobadilisha maisha utajitokeza pasipo kufanya jitihada yoyote.

Chunguza ile safari ya kwenda Emau, Yesu alijieleza yeye mwenyewe katika torati na manabii. Hawakuwa wanafahamu alikuwa ni Yesu. Alijulikana kwao baada ya yeye kuamua kukaa nao na kuumega mkate pamoja nao akiwa ameegemea meza.

Hivyo kwa wao kumsihi akae pamoja nao hakukutokana na wao kumfahamu kuwa ni Yesu, isipokuwa haswa kama mtu aliyekuwa na uwezo wa kuyafafanua maandiko na kumfanya Kristo aonekane katika maandiko husika kwa ajili yao.

Katika muktadha huu, Yesu anatenda kama mmoja ambaye anaweza kugawa neema kutoka Neno na kumwasilisha Kristo kwa watu. Katika hili, Yesu ni mwakilishi wa baba wa kiroho.

Baba yako wa kiroho katika Bwana anapaswa kuwa ndiye njia ya msingi ambayo kwa hiyo Neno la Mungu kwako linagawiwa. Ni lazima kuwe na kuheshimiwa kwake (mwanamme au mwanamke) ili kwa pamoja wawe mfano halisi wa wema na katika kulieleza Neno la Mungu kwako.

Kukaa karibu zaidi nao, kusema kweli, ni ufunguo wa mchakato mzima wa Bwana Mwenyewe kwa kujifanya ajulikane kwako. [Zaidi kuhusu hili utalipata katika kipindi kijacho]. Taswira ya nafasi iliyomo ndani ya moyo wako kama mwana wa kiroho, lazima iwe ya kumsihi baba yako wa kiroho akae au aambatane nawe.

Wale wanafunzi wawili walimwomba Yesu akae nao. Hili linatuonesha shauku kali ya kushikamana ndani ya muktadha ule ule wa kiroho au mazingira yale yale ya kiroho kama ndiye anayegawa neema kwako kupitia lile neno.

6. KUWA BABA NDIYO UKAMILIFU WA HALI YA JUU ZAIDI WA KUMWAKILISHA MUNGU.

Ukweli ambao unapaswa kuzingatiwa katika kutafuta ni, kwa nini Yesu alisogea karibu na hawa wanafunzi wawili? Ni kule kuwepo na kanuni ya ubaba au tabia iliyokuwemo ndani ya Kleopa. Jina la mmoja wa wanafunzi wale wawili halikutajwa ila yule mwingine aliitwa Kleopa lenye maana ya **utukufu wote; baba aliyejulikana tena.**

Majina katika maandiko huelezea tabia (utambulisho) au utendaji (hatima). Kleopa hutoa taswira za maumbo ambayo ni bora kwa ajili ya Bwana kujifunua mwenyewe na kutoa kuelewa kusudi lake.

Yeye ama anawakilisha mtu aliye tayari kuupata utukufu wote na kuhuishwa kuwa baba au mtu ambaye tayari ni taswira halisi ya mambo haya.

Zingatia:

Utukufu wote ni Uwakilishi ulio kamilika wa hali ya juu wa sehemu zote tendaji katika Mungu.

Baba aliye julikana tena ni Uwakilishi sahihi wa ubaba wa kiroho ambao unaheshimika na kupokelewa kwa shangwe.

Kleopa ni alama ya mtu anaye oneshwa taswira halisi ya Mungu kama baba kwa ukamilifu wote na kuwa na ufahamu kamili. Ni mwonekano wa ukomavu wa Mungu kama baba. Hili pia

linafanyika kuwa jambo litakaloweza kupata ufunuo mkubwa na kujifunua kwa Mungu kwetu.

7. KRISTO ANAONGOZWA ILI AJITOKENZE KATIKA MAANDIKO.

Mwanzoni wakati Yesu kwa mara ya kwanza alipowakaribia wale wanafunzi wawili, macho yao ya mwilini yalizuiwa ili wasimtambue Yeye. Yesu hakujiachia ili ajulikane kwao kwa mvuto wa mwili, ushahidi wa nafsi ulihibitajika kwanza. Naam alichagua kuonesha utambulisho Wake kutoka kwenye maandiko.

Kwa kweli Yesu alifanya mambo matatu, yaani :-

- (i) Alifungua Maandiko
- (ii) Alifungua Macho yao na
- (iii) Alifungua Akili zao ili wayaelewe Maandiko.

ALIYAFUNGUA MAANDIKO.

Luka 24:27 Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyo mhusu yeye mwenyewe.

Akamweleza au diermeneuo lenye maana ya kufafanua kikamilifu, kwa uwazi na sawa sawa. *Maana nyingine ni tafsiri, fafanua, fasiri.*

Kuweka wazi maana ya kinachosemwa.

Yohana 5:39 Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayo nishuhudia.

ALIYAFUNGUA MACHO YAO.

Luka 24:31. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua, kisha akatoweka mbele yao.

Macho yao yalifumbuliwa ili wamtambue yeye ndani ya muktadha mahsusi. Mukdadha huu ulikuwa ni moja wapo ya utamaduni wa kitume ambao ndani yake kanuni nne za Matendo ya Mitume 2:42 zilisimikwa imara ndani ya mazingira ya familia ya imani. Kanuni hizi ni *fundisho la mitume, ushirika, kumega mkate na maombi.*

Fundisho la mitume: Alifungua maandiko kwao –mstari wa 27.

Ushirika: Aliegemea meza kushirikisha neema.

Kuumega mkate: Waliumega mkate pamoja wakisherekea meza ya Bwana.

Maombi : Bidii ya kuhitaji, hupelekea *kuomba/maombi.*

Macho yao yalifumbuliwa: kile walicho kiona ndani ya maandiko kilifanyika mwili mbele yao kwa uhalisia. Maandiko yakatimia ndani ya utamaduni wa kitume. Kile kilicho sikiwa sasa kinaonekana.

ALIZIFUNGUA FAHAMU ZAO ILI WAELEWE.

Luka 24:44-45. Kisha akawaambia, haya ndiyo maneno yangu niliyo waambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa na katika manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.

Kwa mara hii ya pili alipowatokea wanafunzi wote waliokuwa wamejikusanya kule Yerusalemu, sasa hafungui tu maandiko ili ajieleze yeye mwenyewe kutokana nayo, au hata kuonesha mbele ya macho yao utambulisho wake binafsi hasa, lakini pia aliingiza katika fahamu zao uwezo wa KUYAELEWA MAANDIKO.

Uelewa huu waliopewa uliwaruhusu kujihusisha na maandiko kitume kwa kuendelea na kuongezeka katika kumfunua Kristo kutoka katika maandiko dhidi ya torati ya Musa na manabii na Zaburi “[Agano la Kale lote]. Wewe na mimi tunalo Agano la Kale na Jipya- logos yote, ambayo imesanifiwa ili kutupa sisi ufunuo wa Kristo.

Ujuzi muhimu ulioingizwa [pashwa] kwao ulikuwa ni wa kuunganisha pamoja (kama vile mchezo fumbo wa kupanga vipande) kweli kadhaa zinazohusiana na Yeye Mwenyewe. Yesu alileta vipande vya ukweli na akaviunganisha kwa pamoja ili waweze kuuona ukweli wote. Katika kipindi cha miaka mitatu, Mtume Paulo alifundisha mausia yote ya Mungu kwa Waefeso.

[Mdo 20:27](#). *Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari za kusudi lote la Mungu.*

Naomba maombi yetu yawe kama ya mwandishi wa Zaburi.

[Zaburi 119:18](#). *Uyafumbue macho yangu niyatazame, maajabu yatokayo katika sheria yako.*

[Waefeso 1:18](#) *Macho ya mioyi yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi lilivyo.*

Leo hii uwezo wa kufunua siri za Neno la Mungu wamepewa Mitume na Manabii [Waefeso 3:5]. Neema, ambayo ni uumbikaji ndani ya utatu wa Mungu, inawasilishwa kupitia Neno la Mungu. Suala muhimu la fundisho lenye utata linaamuliwa na Mitume na Manabii. Paulo alishawishika kuwa Mungu aliwekeza neema ndani yake ili igawiwe kwa makanisa [Waefeso 3:2]. Hili ni la muhimu sana kwa ajili yetu kuunganishwa na chanzo cha kitume ambacho kinaweza KUFAFANUA maandiko kwetu, na kwa kufanya hivyo wanaufukua tena ukweli na ufunuo wa maandiko, na hivyo kuongoza ili Kristo atoke kwenye maandiko. Kwa kifupi, kama yule towashi wa Kushi, wewe na mimi tunamhitaji mtu atakaye tufafanulia maandiko kwa usahihi zaidi (kama vile Priskila na Akila walivyo fafana njia za BWANA kwa usahihi zaidi kwa Apolo)

[Soma Mdo 8:25-35](#)- Tukio la Filipo akifafana akiwa safarini kumhusu Bwana kwa yule Towashi wa Kushi.

MAANDIKO YANAFUNUA NA KUWEKA BAYANA KILA KIPINDI KILICHO KATIKA MUNGU.

Baada ya ufufuko, wanafunzi hawakuweza kufahamu lile tukio la majira yao. Yesu aliwaelezea ufunuo wake mahsus kutokana na maandiko. Kabla ya hili, utambuzi wao wa kusudi la kifo chake, nafasi na utendaji wake kwa namna fulani vilikuwa vimepotoshwa kiasi kwamba walikuwa wanatarajia angekuwa mkombozi wa kisiasa wa Israel.

Hawakuuamini ule ushuhuda wa yule mwanamke kwamba Kristo amesha fufuka kutoka kwa wafu na alikuwa hai. Kwa maneno ya Yesu walikuwa wajinga na wazito kuamini [[soma Luka 24:25](#)].

Ujinga au anijetos lenye maana ya ukosefu wa intelijensia, mjinga, mtu asiye na ufahamu ambao ni upeo wa nguvu ya hali ya juu wa maarifa ndani ya mtu. Ni kiungo ambacho kwa hicho vitu vya Ki-Uungu vinatambuliwa na kujulikana au kupuuzwa.

Walikuwa wajinga kiroho yaani walikosa intelijensia ya kiroho ya kutambua kikamilifu mambo ya kiroho yaliyokuwa yanaingia katika siku zao. Kushindwa huku kwa sehemu kulitokana na kulidharau Neno lililoandikwa.

Wakati wowote unapodharau ule mchakato wa kuwa chini ya ufunuo wa utu wa Kristo kupitia njia ya Neno lake linalokujia kupitia baba wa kiroho, basi uwezo wako wa kupambanua maana ya kiroho ya muda wowote unaoishi wewe unakuwa umeharibiwa vibaya. Uwezo wa utambuzi wako wa kiroho unakuwa na kikomo na kisha wewe pia utakuwa na ‘moyo mzito’ kuyaamini maneno ya kinabii yaliyo fungamanishwa ndani ya neno lililo andikwa, ambalo limesanifiwa ili kukupa kuyaelewa majira unaoishi.

Katika kukutana nao kwa mara ya kwanza wakiwa njiani kuelekea Emau, aliweza kufunua tu zile pande mbili za neno [TORATI na MANABII] kwa sababu ya hali ya mioyo yao ambao anawaelezea kama ni watu **wajinga** na walio ‘**wazito wa moyo kuamini**’. Mara tu walipofika Emau- alama ya kufikia upeo wenye ari wa mioyo yao, macho yao yalifumbuliwa, imani yao ikainuliwa na wakarudi kushirikisha ujuzi huu kwa wanafunzi wengine kule Yerusalemu.

Hapa, alijifunua Yeye Mwenyewe kutoka Torati, Manabii na Zaburi. Mwandishi wa Zaburi anamzungumzia mtu binafsi aliyekutana na ujuzi katika neno yaani mahali ambapo fundisho linakuwa hai.

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Ni nini kinacho sababisha mshikamano na makubaliano viwe vutivu kwa Mungu kama ndio muktadha bora ambao huo angechagua kujifunua Yeye Mwenyewe kwa kina kupitia Neno lake?
2. Jadili suala la umuhimu wa kufahamu maana muhimu ya kiroho ya wakati unaoishi, na namna Neno la Mungu linavyokuwa msingi ambao kutokana nao tunaweza kutafsiri matukio ya kiroho na misisitizo katika wakati wetu.
3. Kuna uthamani na faida zipi zilizomo katika mazungumzo ya ana kwa ana kuhusiana na kujadiliana mambo ya rohoni na fundisho au kuhusu majira maalum ambayo Mungu anaweka msisitizo wa mambo fulani?
4. Kwa kurejea dondoo namba 5 pamoja na hili zingatia pia Matayo 23:37-39, chunguza ule umakini wa kumpokea sawa sawa na kwa kujihusisha na mtu ambaye Mungu amemweka kama baba wa kiroho katika maisha yako.
5. Boresha mbinu iliyotumiwa na Yesu katika kujifunua Yeye Mwenyewe ambapo: (a) Aliyafunua maandiko (b) Alifumbua macho, na (c) Alifungua fahamu kuelewa maandiko.

KIOO CHA NENO.**Lengo: Jione wewe mwenyewe katika Kristo katika Neno.****MUHTASARI KWA KIFUPI WA KANUNI ZILIZOJITOKEZA KATIKA VIPINDI VILIVYOPITA.**

- ❖ Mungu na Neno lake ni wamoja.
- ❖ Kimsingi Mungu hunena kupitia Neno Lake. Kinachosikiwa kama ‘rhema’ hunenwa kutoka logos.
- ❖ Mungu anafunuliwa kupitia Neno lake.
- ❖ Neno lake, Jina la Mwana kondoo huelezea asili yake (utambulisho) na utendaji (makusudi).
- ❖ Mungu anajifunua Yeye Mwenyewe kwetu kupitia Neno Lake.
- ❖ Mchakato wa kulipata (kulisikia) na kulitii Neno la Mungu ndiyo namna ambayo kwa hiyo Yeye anajifunua Mwenyewe kwetu na kuendelea kuongezeka daima.
- ❖ Kila wakati tunaposikiliza kwa usahihi na kwa makini tukatii, tutakuwa tunashiriki asili yake ya Ki-Uungu, na hivyo tunafanyika kama Yeye alivyo au kiuumbaji tunaelezea ukweli kuwa kama alivyo Yeye na sisi ndivyo tulivyo [1Yoh 4:17].
- ❖ Neno la Mungu ni mbegu ya Ki-Uungu isiyoharibika, yenye vinasaba vyenye mfumo kamili wa asili na kusudi la Ki-Uungu. Kwa hiyo tunazaliwa, au kuzaliwa upya kama wana wa Mungu.
- ❖ Utii endelevu kwa Neno hutakasa nafsi. Mbegu hii [Neno] hukaa ndani yetu na kwa jinsi hiyo hatutatenda dhambi kama ndio mtindo wa maisha. Kushiriki katika asili ya Ki-Uungu ya Mungu kwa namna hii, tuna epukana na uharibifu ulioko duniani.
- ❖ Kiwango cha uzaaji matunda kinacholetwa na Neno ndani yetu hutegemea kiasi [kipimo] cha kusikiliza na kutii.
- ❖ Tunaishi kwa kila Neno la Mungu linalotujia.
- ❖ Wajibu wetu wa kujiweka wenyewe katika nafasi ya kusikia na kutii Neno Lake unategemea kiwango cha hali ya juu cha kulipa heshima, uthamani na stahakwa UNENAJI WAKE.
- ❖ Ni mara chache tuta angukia kwenye makosa na uongo ikiwa tutatoa kipaumbele kuzifahamu NJIA za Mungu juu ya KAZI ZAKE.
- ❖ Uwakilishi wetu kwa ajili yake unavyokua, tunafanyika kuwa Yeye katika dunia yetu.

Maandiko yote yanamfunua Kristo na kutupa uelewa na uwazi kwa kila wakati [majira] katika Mungu.

Mbegu ya Neno hufanyika kuwa MWANA wa Ufalme. Kila kanuni ya neno la Mungu ni lazima ishikamane na maisha yetu. Neno alifanyika mwili na akaishi katikati ya wanadamu ambao waliuona utukufu wa Ki-Uungu au asili ikidhihirishwa.

Yakobo 1:14-25

14. Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa.

15. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.

16. Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike.

17. *Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.*
18. *Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake.*
- 19 *Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika;*
19. *Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu.*
- 20 *Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lilipandwa ndani, , liwezazo kuziokoa roho zenu.*
- 21 *Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.*
- 22 *Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia **uso wako katika kioo.***
- 23 *Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.*
- 24 *Lakini aliye itazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*

1. NAMNA UNAVYOSIKIA NI JAMBO MUHIMU.

Yesu alijihusisha sana na yote mawili NINI na NAMNA watu walivyosikia au kusikiliza.

Mark 4:24a *Akawaambia, “angalieni ni NINI msikialo”.*

Hili linatilia mkazo umuhimu wa kuwa na uchaguzi wa, ni fundisho la namna gani unalosisikiliza.

Luk 8:18a *“Jiangalieni basi JINSI/NAMNA msikiavyo”*

Mstari huu unatilia mkazo jukumu la kuwajibika binafsi na uwepo wa mtazamo sahihi ndani ya wale wanaosikia neno sahihi na lenye kuhusika na wakati wa sasa.

Ile namna ambayo Neno la Mungu linapokelewa hubainisha uzaaji wake wa matunda mengi yenye afya au matokeo katika maisha yako. Namna unavyo lipokea Neno ni ya muhimu sana.

Zifuatazo ni baadhi ya kanuni muhimu zinazopaswa kuzingatiwa kila wakati tunapo SIKILIZA/SIKIA Neno.

a) SIKIA NA UELEWE

Yesu alitilia mkazo umuhimu wa kuelewa kile unachosikia:

Matayo 15:10, 11 *Akawaita makutano akawaambia, “Sikilizeni; mfahamu”*

Matayo 13:13 *Kwa sababu hii ninasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.*

Kuto kuelewa ni kukosa uwezo katika hatua ya kwanza ya kutambua kwa akili kanuni ya Neno linalowasilishwa, na kisha kwa sababu ya hili, inafuata kushindwa kutii [soma Zaburi 111:10]

Zaburi 111:10b *Wote wafanyao haya wana akili njema.*

Waebrania 5:11 *Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake, na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia.*

Waaminio wa Kiebrania walishindwa kuzishika baadhi ya kanuni zilizo mhusu Melkizedeki. Sababu iliyotolewa kwa hili ilikuwa ni ‘uvivu wa kusikia’

Uvivu= nothros maana yake ni = *uzito, vivu na uzembe.*

Kimuktadha [soma sura ya 5 yote ya Waebrania] uvivu huu wakusikia ulikuwa ndio matokeo ya kipindi kirefu ambacho kulikuwa hakuna ukuaji uliokusudiwa wa kuendelea hadi ukomavu; hasa katika kuhama kutoka maziwa ya Neno hadi nyama ya Neno.

Hapa watu hawa pia wanaelezwa kama watu wasiokuwa na ujuzi katika Neno la wenye haki na ni watoto wachanga. Mtume Paulo katika 1Wakor. 3:1-3 anaangazia zaidi kuhusu uchanga kwa wale ambao bado wanasumbuliwa na mambo ya mwilini, kijicho, wivu, na kujiinua. Yote haya yalisababisha uvivu wa kusikia na huzuia watu kuelewa. Hivyo kutolitii Neno kunaweza kuwa ndiyo matokeo pekee.

Katika Yakobo 1:14-25

Katika **Yakobo 1:14-25** kama ilivyo nukuliwa hapo juu, Yakobo anatusihi tutoke katika kila aina ya tamaa ambazo ikiwa tutazikaribisha zitatupeleka kwenye kutenda dhambi, na matokeo yake ni kifo cha kiroho [mst 15]. Kwa muktadha huo huo anaonya kuhusu asili idanganyayo ya tamaa na dhambi [mst 16]. Ana endelea kutukumbusha kwamba tumezaliwa kwa NENO LA KWELI [mst 18]- mbegu ya asili ya Ki-uungu imo ndani yetu.

Akiwa amesha imarisha hili, Yakobo anatupa ishara ya kutokuwa wepesi kusema, ila tuwe wepesi kusikia na kutokuwa wepesi kukasirika na kisha anataelekeza kuweka mbali ubaya wote - tabia mbaya, mabaki yoyote au uchafu wote wowote k.v chuki, kijicho, kudhamiria kuua, ugonjwa wa kufisha/ kudhamiria kuua n.k. Kisha anaangazia kanuni zaidi za **namna mtu anavyoweza kulipokea NENO LA MUNGU.**

b) Lipokee NENO kwa UNYENYEKEVU/UPOLE

Yakobo 1:21 “*Na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani liwezalo kuziokoa roho zenu.*”

Unyenyekevu/ upole= “prautes” maana yake ni “ulaini wa moyo, upole wa roho, sikivu.”

Angalizo: Unyenyekevu ni kinyume cha kiburi na hasira.

Zaburi 25:8-9

8. *Bwana yu mwema, mwenye adili; kwa hiyo atawafundisha wenye dhambi njia.*

9. *Wenye upole atawaongoza katika hukumu, wenye upole atawafundisha njia yake.*

Yakobo 4:6 *Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi, kwa hiyo husema Mungu huwapinga wajikuzao, lakini huwapa Neema wanyenyekevu.*

c) Lipokee Neno kwa UHAJI, STAHA NA KULIENZI KULIKO

Zaburi 25:12-14

12. *Ni nani amchaye BWANA? Atamfundisha katika njia anayo ichagua*

13. *Nafsi yake itakaa hali ya kufanikiwa, Wazao wake watairithi nchi*

14. *Siri ya BWANA iko kwao wamchao, naye atawafundisha Agano Lake.*

Isaya 66:1-2

1. *Bwana asema hivi, mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu, mtanijengea nyumba ya namna gani?*

2. *Maana mkono wangu ndio uliofanya hivi vyote, vitu hivi vyote vikapata kutokea, asema BWANA, lakini mtu huyu ndiye nitakaye mwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neon langu.*

Waebrania 12:25 *Angalieni msimkataye yeye anenaye.*

Kataa= Paraiteonai maana yake ni **epuka, jitenga, tupa, inama.**

d) Lipokee Neno kama ni “NENO LA MUNGU” kupitia wanadamu

Ikiwa utalichukulia neno la Mungu linalokujia wewe kama ni mawazo tu ya mwanadamu, basi hilo Neno la Mungu halitakuwa na matokeo yaliyokusudiwa kwa ajili yako.

Kama baba wa kiroho aliyesimamia kanisa kule Tesalonike, Paulo aliendelea kuwashukuru kwa kumpokea yeye na lile neno alilokuwa amebeba kama aliyetumwa na Mungu.

Kwa Watesalonike, neno la Paulo lililinganishwa na Neno la Mungu. Hali kadhalika katika kulipokea Neno la Mungu, walimkubali kama mchukuzi na muwasilishaji wa neno lile; kwa pamoja neno naye anenaye lazima wapokelewe vizuri.

Lakini cha muhimu ni kila wakati kulipokea neno linalo sambazwa kupitia vyombo wanadamu, lakini unapaswa kutambua ya kwamba ni Mungu mwenyewe anayesema nawe.

1WATESALONIKE 2:9-13

9. *Maana, ndugu, mnakumbuka taabu yetu na masumbufu yetu, kwa kuwa mchana na usiku tulifanya kazi tusije tukamlema mtu wa kwenu na awaye yote, tukawahubiri hivi. Injili ya Mungu. mtu wa kwenu awaye yote, tukawahubiri hivi Injili ya Mungu.*

10. *Ninyi ni mashahidi, na Mungu pia, jinsi tulivyokaa kwenu ninyi mnaoamini, kwa utakatifu, na kwa haki, bila kulaumiwa;*

11. *Vile vile kama mjuavyo jinsi tulivyo mwonya kila mmoja wenu kama baba awaonyavyo watoto wake mwenyewe, tukiwatia moyo na kushuhudia;*

12. *Ili mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika Ufalme wake na utukufu ake.*

13. *Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe wa Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu, na ndivyo lilivyo kweli kweli, litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnao amini.*

Hapa kuna maneno ya Kiyunani yaliyo tafsiri neno ‘mlilipokea’ na ‘mlipopata’/ ‘mlipo likubali’ katika mst wa 13 na kudokeza;

Lilipokelewa = paralambano maana yake ni **kusogeza karibu, pamoja na, au kwa mwenyewe.**

Lilikubaliwa = dechomai maana yake ni **kukubali zawadi bila ya masharti na kwa utayari.**

= kumpelekea mtu kilichotolewa au kilicho letwa na mwingine, kupokea

=pokea, kukubali kwa akili na moyo kwa kumaanisha, kuhakikisha, kushikilia, kufuata.

Hivyo Watesalonike hawakupokea tu neno kutoka kwa Paulo kwani hawakuwa wamepakana kwa karibu naye au katika ujirani ule ule kama yeye, bali walipokea kile alichosema na kupendelea kumpokea yeye pia.

Hata hivyo, situ kwamba walimpokea yeye na maneno yake, lakini pia WALIMKUBALI yeye na maneno yake. Neno **walikubali** linaonesha kwamba wao, ndani ya mioyo na akili zao na kwa moyo wote walihakikisha na hivyo kumkubali yeye na ujumbe wake.

Paulo na ujumbe wake walikuwa wamoja. Mjumbe amefanyika kuwa ujumbe, na hivyo kuukubali ule ujumbe ina maanisha kumkubali mjumbe pia. Lakini kumkubali mjumbe inamaanisha kwamba unao utambuzi sahihi kumhusu mhusika' kama mtu aliye tumwa- kama mwakilishi wa Mungu mwenyewe.

Hagai 1:13 *Ndipo Hagai mjumbe wa BWANA, katika ujumbe wa BWANA, akawaambia watu akisema, mimi nipo pamoja nanyi, asema BWANA. [KJV]*

e) **Lipokee neno kwa HAMU na JIWEKE KATIKA MCHAKATO WA KUHITAJI.**

Mdo 17:1-13

1. *Wakiisha kupita kati ya Amfipoli na Apolonia wakafika Thesalonike, ambapo palikuwa na sinagogi la Wayahudi.*
2. *Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu,*
3. *Akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.*
4. *Wengine miongoni mwao wakaamini, wakashikamana na Paulo na Sila; na Wayunani walio mcha Mungu wengi sana, na wanawake wenye cheo si wachache.*
5. *Na Wayahudi wakaona wivu, wakajitwalia watu kadha wa kadha katika watu ovyo wasio na sifa njema, nao wakakutanisha mkuitano, wakafanyia ghasia mjini, wakawaendea watu wa nyumba ya Yasoni, wakataka kuwapeleka mbele ya watu wa mji;*
6. *Na walipo wakosa, wakamkokota Yasoni na baadhi ya ndugu mbele ya wakubwa wa mji wakipiga kelele, wakisema, watu hawa walio upindua ulimwengu wamefika huku nako.*
7. *Na Yasoni amewakaribisha , na hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume cha amri za Kaisari, wakisema na kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu.*
8. *Wakafadhaisha ule mkutano na wakubwa wa mji walipo yasikia hayo.*
9. *.Nao walipokwisha kumtoza dhamana Yasoni na wenziwe wakawaacha waende zao.*
10. *Mara hao ndugu wakawapeleka Paulo na Sila usiku hata Beroya. Nao walipofika huko wakaingia katika sinagogi la Wayahudi.*
11. *Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*
12. *Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini, na wanawake wa Kiyunani wenye cheo, na wanaume si wachache.*
13. *Lakini Wayahudi wa Thesalonike walipopata habari ya kwamba neno la Mungu linahubiriwa na Paulo hata katika **Beroya**, wakaenda huko nako wakawachafua na kuwafadhaisha makutano.*

Paulo, alitoa hoja kutokana na Maandiko, aliweza kuwathibitishia Wayahudi wa Tesalonike kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo ambaye angekufa na kufufuka tena.

Alitoa hoja= dialegomai maana yake ni **kujibizana au kwa kupokezana, kusemezana na, fikiri, wasilisha hotuba ya viwango vya akili; kusema kikamilifu, ndivyo ilivyo, jadili.**

Baadhi ya Wayahudi waliamini pamoja na wanawake wenye cheo katika jiji. Idadi kubwa ya Wayahudi wa Thesalonike hata hivyo, walikuwa wanasumbuliwa na wivu na kwa ukali walilipinga neno ambalo Paulo aliwaletea na waka chochea vurugu katika jiji na hivyo likatokea kundi lililompinga Paulo.

Wenye mamlaka ya jiji nao wakashawishika dhidi ya Paulo. Paulo alilazimika kuliacha jiji na kuendelea hadi Beroya. Wayahudi wa Beroya walistaarabika zaidi ya Wayahudi wa Thesalonike.

Kama vile istilahi ya Kiyunani '*engenes*' [ilivyotafsiri wastaarabu/waadilifu zaidi] ina dokeza walikuwa na vyeo na wa tabaka la juu au kule kwa wao kujitambua ni wenye cheo kuliwatenga kama watu waadilifu zaidi.

Kwa hakika kilicho watofautisha wao kama waadilifu au kuwa na ufahamu adilifu kilikuwa ni mwikio wao kwa mafundisho ya Paulo.

Kwanza, walilipokea Neno kwa HAMU:

HAMU= prothunia maana yake ni **moyo, roho, utayari wa akili, wepesi.**

Kwa hamu ni pamoja na utendaji wa kupokea kama ni 'kweli' kile unachosikia. Wayahudi wa Thesalonike waliasi na walikuwa wapinzani wa Neno,

Waberoya kwa hamu na kwa furaha walilipokea Neno. Kwa hamu ni pamoja na hudumisha *uchangamfu, mapenzi, upendeleo, utayari na kuamua kwa moyo.*

Kinyume chake ni *kutokuwa na hamu, kutojali, kuwa na chuki, kutofautiana, uzito n.k.*

Cha pili: Kwa ustadi wa kimahakama walichunguza au waliyapeleleza maandiko kila siku ili waweze kuuhalalisha ule ukweli ambao Paulo alikuwa anafundisha.

Chunguza= anakrino maana yake ni **angalia kwa makini, ndiyo kusema, [kumwingiza mtu hatarini] pima, saili, kubaini.**

Sisi pia ni lazima tuwe na tabia zenye sura hizi mbili kila wakati tunapolisikia neno la Mungu. Tabia ya kuwa na HAMU na KUCHUNGUZA [KUPIMA] ni muhimu sisi kuwa nazo.

Tunapaswa kuwa na vyote yaani *kukubali kushikilia Neno* katika mkono mmoja na mkono mwingine uhusike na mchakato wa kila siku wa *kuyachunguza Maandiko* ili kupima tulichosikia.

Matokeo yalikuwa kwamba WENGI WALIAMINI yaani Wayahudi wengi na wanawake wa Kiyunani na wanaume wenye cheo. Katika majira haya tutaanza kuona kundi kubwa la watu waliofungwa na dini na tamaduni zilizopitwa na wakati za udini wa 'Kikristo' wakihama na kuliadini Neno la sasa linalotoka kwa Mungu, likiwa lina tangazwa kupitia mitume na manabii wa kweli.

Pia na watu wenye cheo na wanazuoni [wasomi] waliobobea katika Neno [kama inavyo ashiriwa na Wayunani], wenye ushawishi na matajiri nao wataanza kuukubali msisitizo uliopo hivi sasa wa kitume kupitia Neno la Mungu.

LA MUHIMU:

- [Yakobo 1:21](#) Unaashiria kwamba wakati Neno la Mungu linapokelewa kwa unyenyekevu, linakuwa na UWEZO WA KUOKOA NAFSI. ule uwezo wa kuokoa wa Neno la Mungu unao husiana na mchakato unaoendelea wa kufanya upya nia [\[Rum 12:1na 2\]](#) utaachiliwa tu kutegemeana na jinsi neno lilivyopokelewa kwa unyenyekevu. Unyenyekevu unahusisha pia kuvua mawazo binafsi uliyo nayo na kuacha kujiona kwamba unalijua Neno na unamjua mtu yule anayekuletea neno husika.
- [1Thes 2:13a](#) *kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile Neno la ujumbe wa Mungu mlilolisika kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu. [NLT]*
- [1Thes 2:13](#) unatueleza kuwa wakati Neno linapo pokelewa kama ni Neno la Mungu, na siyo neno la mwanadamu, hapo ndipo nguvu yake ya “kutenda kazi yake ndani yako wewe uaminiye” inaamshwa.

Tenda= energeo maana yake ni kuwa hai, - kufaa, -enye matokeo, -enye uwezo katika, kuwa tendaji, kuwa kazini, toa nguvu/ nishati.

2. UMESIKIA SASA UNALAZIMIKA KUTII

Yakobo 1:22-25

- 22. *Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.*
- 23. *Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo.*
- 24. *Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.*
- 25. *Lakini aliye itazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*

Yakobo analifananisha Neno la Mungu na kioo. Kioo kinakuakisi wewe sawa na mwonekano na hali yako ya nje, ni kweli kinaakisi mwonekano wako wa nje kama ulivyo na siyo zaidi ya hapo, wala siyo pungufu ya hapo.

Mara unapojiangalia mwenyewe kwenye kioo, unafanya marekebisho muhimu kwa chochote ambacho hujaridhika nacho ndani ya shauku ya kutaka kuonekana bora.

[Waebrania 4:12](#) *Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo vya mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

[Soma pia Zaburi 19:7-14 na Zaburi 139:23-24]

Neno la Mungu lina viwango vya tabia na asili ya Ki-Uungu kwa ajili



yetu. Kila wakati tunapolisikia, linatuletea viwango vya Ki-Uungu ambavyo tunapaswa kuvitilia maanani. Wakati tunapo gundua kwamba, tupo mbali na asili ya Kristo, iwe tunasoma au tunajiona katika Maandiko tunapaswa kutubu na kutafuta kuingiza katika maisha na katika tabia zetu kile tulicho kiona ni cha Kristo kupitia Neno.

Kama ilivyo fundishwa katika kipindi kilichopita kupitia mchakato wa kusikia na kutii, tunatakasa nafsi zetu na kufanyika washiriki wa asili ya Ki-Uungu ya Mungu, mahali pekee tunapoepuka uharibifu wa ulimwengu. Yakobo anafundisha kitu kinacho fanana na hicho hapa.

Kila wakati uwezo wako wa kumwona Mungu unapoongezeka, unakuruhusu wewe uone mahali ulipo, kulingana na ile sura ya Mungu uliyo na njozi nayo. Wakati Isaya alipomuona BWANA yuko 'juu na kuinuliwa,' katika Isaya 6 hili la kumtazama Mungu kulimsababishia yeye kuona hali yake ya ukengefu.

Alipaaza sauti, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea"

Kwa kadri dhana yako kumhusu Mungu inavyokua na kufikia katika usahihi mkubwa zaidi, kile unachokiona cha asili yake kinatoa nuru kwenye maeneo ya giza katika maisha yako- na hivyo wewe unajirekebisha ili kupatana na kile unachoona.

Hatua kwa hatua Mungu hujifichua/hujifunua mwenyewe kwako kupitia maandiko ili upate fursa ya kujikagua ni wapi wewe uko sambamba na asili yake. Mungu atakuonesha wewe mwenyewe jinsi ulivyo kwa kukuonesha wewe jinsi Yeye mwenyewe alivyo. Ulitoka kwake na ulichaguliwa ndani yake kabla ya wakati. Hivyo, katika ukweli, wakati unaposoma au kulisia Neno, unajiona mwenyewe kukamilishwa ndani ya Mungu na umekamilika katika Yeye.

Unaweza ukajisawazisha tena katika nafasi hii kwa kadri unavyo gundua kuna kukengeuka katika maisha yako, kutokana na kile alichokiandaa Mungu kwa ajili yako ili uwe ndani yake.

[Zaburi 40:7-8](#) Ndipo niliposema, Tazama nimekuja, (Katika gombo la chuo nimeandikwa). Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.

Kadri unavyo sikia au kujifunza Neno la Mungu, Mungu wa Neno anakusoma wewe.

Kadri unavyo soma au kusikia Neno la Bwana, usiingize humo mawazo yako ya kuwa mwenye haki juu ya kile unacho soma au kusikiliza. Unapaswa kuyaruhusu maandiko yalete marekebicho katika utambuzi wako katika mambo yote, hata katika yale unayofikiri kuwa wewe uko sahihi kabisa kuyahusu. Kuwa tayari kubadilika.

[Mithali 21:2](#). *Kila njia ya mtu ni sawa machoni pake mwenyewe, bali BWANA hupima mioyo.*

• [KUKOSA KUTII=KUSAHAU=KUTOFAUTIANA AU KUPUUZA](#)

Kusikia na kutotii Neno la Mungu kunafananishwa na mtu, ambaye baada ya kujiona yeye mwenyewe katika kioo, ANASAHU anafanana na nini.

Sahau= epilanthanomai maana yake ni **dharau, kutojali tena, kuwekwa katika hali ya kusahauliwa, -isiyo jaliwa.**

Kama linavyoonekana, neno 'sahau' hali ashirii kukosa kukumbuka kama vile inavyofikiriwa kwamba kwa hakika mtu anaweza asijihusishe sana na kile alichona mtu mwingine kumhusu yeye mwenyewe katika kioo cha Neno la Mungu.

Hili linaturejsha kwa mtu ambaye, baada ya kujihusisha na Neno la Mungu ambalo linamletea asili ya Mungu, bado anakuwa anaenenda kinyume, kutojihusisha, kutojali au kutokuwa na mwelekeo wowote wa kubadilika.

Kushindwa kutii kunaashiria kutofautiana na kuwa na mashaka ni kipi tunataka tukifikishe kwenye viwango vya Ki-Uungu vya Mungu. Mungu 'anasahaulika' wakati kanuni zake hazifuatwi tena:

[Kumbukumbu 8:11a- Jihadhari usije ukamsahau BWANA Mungu wako, kwa kutozishika amri zake.](#)

KUSHINDWA KUTII=NI KUJIDANGANYA MWENYEWE

Wale wanaosikia na hawatii wanajilaghai wenyewe(**Yak 1:2**)

Laghai/danganya = paralogzomai maana yake ni **kufikiri kwa uwongo au isivyo sahihi-potosha au hadaa, fanya hila.**

3. NDANI YA MCHAKATO WA WEWE KUTII UNASHIRIKI NDANI YA ASILI YAKE YA KI-UUNGU.

[2Kor 3:17-18](#)

17. *Basi, 'Bwana' ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru,*
18. *Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*

Ule utukufu wa Mungu hutupeleka kwenye uwakilishaji halisi wa asili na tabia ya Mungu, ikiwa ni pamoja na nafsi na nguvu zake. Neno la Mungu ndicho kioo chetu. Kwa kadri tunavyosoma na kujiangalia katika kioo hiki, tunaviona vipengele vya utukufu wa Mungu – asili yake, tabia, nafsi, nguvu n.k. Mstari huu unafundisha kwamba, kwa kadri tunavyo UTAZAMA utukufu huu, TUNA BADILISHWA kwa kile tunachokiona! Kristo anajitokeza/anajionesha kutoka katika maandiko kila wakati tunapo yasikia au kuyasoma.

Asili na kusudi lake huwa wazi kwetu. Kwa kadri tunavyo endelea kutazama ni nini anacho jifunulia Yeye Mwenyewe, tendo hilo la KUTAZAMA au KUONA ni nini kilichofunuliwa kwetu kina nini, tuta ona ndani yake mna uwezo na nguvu ibadilishayo.

Ufunguo ni kuwa:-unavyoona kile anachokuonesha, TII kinachojitokeza au kuwa wazi kwa mahitaji ya Bwana na katika mchakato wako wa utii uta anza kupokea nguvu ibadilishayo ya Neno lake ndani yako kupitia Roho Mtakatifu.

Badilishwa= metamorphoo maana yake ni **kubadili kuwa katika muundo mwingine, kubadilisha, geuza kuwa nzuri zaidi.**

Neno la Kiingereza, **metamorphosis**, linatokana na neno la Kiyunani, **metamorphoo**. Likimaanisha **kupitia mabadiliko ya haraka katika taasisi ya ndani** na katika **muundo wa nje** (kama vile Kiwavi anapogeuka kuwa kipepeo) ili kwamba mabadiliko yote ya mtu, utendaji na uwezo mbalimbali vyote vinaongezeka sana. Hiyo ndiyo nguvu ya utii kwa Neno.

Yohana 14:21. Yeye aliye na amri na kuzishika yeye ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.

TAZAMA KWA MAKINI

Yakobo 1:25. Lakini aliyetazama kwa MAKINI sheria kamilifu iliyo ya uhuru na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.

Tazama kwa makini= parakupto maana yake ni **kuinama kwa karibu**, ndiyo kusema, **kuegema kwa juu** ili **kuweza kuangalia katikati**.

Kuangalia ndani ya, kuinamia kitu ili uweze kukiona, kwa kumaanisha, kwa uangalifu, kwa makini ndani, kukagua kwa udadisi.

Unavyokuwa makini zaidi kuangalia ndani ya neno la Bwana, ufunuo wa asili wa Kristo kutoka kwenye maandiko utaongezeka na kuwa mkubwa zaidi, na unapo tii, siyo tu utabadilishwa ili uwe kama kile ulichoona, lakini pia utapokea ujuzi wabaraka za Mungu kwa yote utakayo fanya.

Yohana 13:17. Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda.

Yoshua 1:8. Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawa sawa na maneno yote yaliyo andikwa humo, maana ndipo utakapo ifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapo stawi sana.

4. KUTAKASWA NA MATOKEO YA KUPATA ELIMU YA NENO LA MUNGU.

WAKATI ALIPOLIJENGA LILE HEMA, Musa alichukua metali za vioo vya kujitazamia vya wanawake, akaunda lile birika. Hivi vioo vya kujitazamia vilikuwa vimepakwa shaba. Birika lile lilikuwa ni beseni kubwa sana lililokaa kati ya madhabahu ya shaba ya kutolea dhabihu na mahali patakatifu. (Soma Kutoka 30:17-21 kwa maelezo zaidi). Lile beseni lilijazwa maji, na makuhani waliosha humo mikono na miguu yao katika birika kabla hawajaingia mahali patakatifu kuhudumu. Ile Shaba iliyopakwa ilitumika kama kioo.



Kile kioo kilifichua hali ya uchafu ya kuhani, na kisha kwa kutumia maji, angejitakasa yeye mwenyewe, yaani mikono na miguu.

Kioo cha Neno la Mungu siyo tu kina fichua dhambi na makosa yetu, lakini kinatutakasa kutokana na hayo. Maji ni alama ya Neno la Mungu.

Yohana 15:3. Ninyi mmeshakuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia.

Waefeso 5:25-27

25. Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Krsito naye alivyolipenda kanisa, akijitoa kwaajili yake.

26. *Ili makusudi alitakasena kulisafisha kwa maji katika neno.*

27. *Apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lolote kama hayo, liwe takatifu lisilo na mawaa.*

Yoh 17:17. *Uwatakase na ile kweli, neno lako ndiyokweli.*

MIKONO SAFI

Mikono katika maandiko ni **alama ya uwezo wa kutekeleza** au kwa **ukweli kutimiza makusudi ya Mungu.**

Mikono hutenda kazi ya Ki-Uungu. ‘Mikono’ pia huashiria uwezo wa ‘kulichambua Neno la ukweli’ kwa ustadi, usahihi na UAMINIFU.

2Wakorinto 4:2. *Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyo sitirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuudhirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu.*

MIGUU SAFI

Miguu hugusia kutembea kwetu ndani ya Kristo – yaani ujumla wa tabia na mawazo yetu katika maisha. Pia inazungumzia maendeleo kusonga mbele na kuongezeka katika njia na makusudi ya Mungu.

Wakolosai 1:10. *Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa, mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu.*

JIOSHE MWENYEWE NDANI YA MAFUNDISHO YA KITUME

Ni jambo la lazima kwako kujiweka wazi kwa kujihusisha na fundisho la kitume kutoka kwa baba wa kweli, mwaminifu na mwenye neema ya kitume. Utume una mtazamo wa kulirudisha kanisa kwenye utaratibu sahihi wa Kibibilia.

Soma maelezo katika Yohana 9 ya namna mtu aliye zaliwa akiwa kipofu alivyo pokea kuona baada ya kutii maagizo ya Yesu ya kwenda kunawa katika birika la Siloamu.

Siyo tu kwamba Neno la Mungu linatutakasa dhambi, lakini kwa kadri tunavyo endelea kuyaosha macho yetu ndani ya fundisho la kitume [kama inavyoonekana katika birika la Siloamu likimaanisha aliyetumwa alama ya utume] kuona [uoni] kwetu kirohona kuelewa kunafanywa bora zaidi na huongezeka sana hadi kuanza kuona ukamilifu wote wa Kristo kama unavyofunuliwa katika Neno lake.

Inavutia kuona kwamba kabla Yakobo hajatoa maoni ya namna ya kupokea Neno la Mungu lililopandwa kwa unyenyekevu na hivyo kuamsha utekelezaji wake wa kuokoa, anatuagiza sisi kwanza “tuweke mbali uchafu wote na ubaya uzidio” kisha akaendelea kujadili mfanano wa Neno la Mungu na kioo n.k.

Uchafu unazungumzia tabia za uovu na ubaya. Huzungumzia nia mbaya, kijicho, kusudio la uovu, shauku ya kudhuru, mambo haya huzuia kuona kiroho.

Neno linaweza kusafisha kabisa mambo haya, lakini unahitajika utii wa dhamiri wa KUYAWEKA MBALI. Mara suala la kutakasa maisha ya mtu lina shughulikiwa, ule uwezo wa kupenya hadi kuona asili ya Mungu na makusudi yake utaongezewa nguvu kubwa.

Na hivyo kadri utakavyo endelea kutii kile unachoona cha asili na mahitaji ya Mungu katika Neno Lake unabadilishwa ufanane naye daima katika viwango vya ongezeko la ‘utukufu hadi utukufu’ kwa Roho wa Bwana.

Ikiwa hatimaye, tunataka kufanana na Neno la Mungu yaani barua za Kristo, zinazo someka na kujulikana na watu wote [2Kor 3:1-3] kisha katika kukua kwetu katika ukamilifu na ukomavu wa kufanana na Kristo, uhalisia wa maisha yetu utafanyika kuwa kioo cha Neno kwa wengine.

Hivyo kanuni zote zenye mahusiano na neno kama kioo, zinakuwa rahisi na zinawezekana KWETU! Wewe ndiwe kioo cha Neno la Mungu kwa wanadamu walioko duniani. Kadri utakavyo oneshwa asili yake mbele za watu, nao pia kama watatii, watabadilishwa na kile cha Kristo wanacho kiona ndani yako.

Viumbe vyote vinatazamia kwa shauku ukweli huu-*‘kufunuliwa kwa wana wa Mungu’* [[Rum 8:19](#)]

ONGEZEANA

Waebrania 4:12-13

Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena la choma hata kuzigawanya nafsi, na roho na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu,

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Hali ya ndani ya moyo wa mtu na akili katika KULISIKIA Neno la Mungu ni muhimu kupindukia. Jadili usemi huu.
2. Onesha umuhimu na fafanuzi juu ya tabia nne muhimu katika KULIPOKEA neno la Mungu kama linavyofundishwa kwako, ili kwamba matokeo ya juu au athari zilizokusudiwa ziweze kuonekana.
3. Neno la Mungu linafanaishwa na kioo. Ni kanuni zipi baadhi unazoweza kupata kutokana na mfanano [analojia] huu /hii?

KUCHANGANYA IMANI NA USIKIAJI WA NENO.

Lengo: Imani kama kiini kuelekea asili ya Mungu.

Ebr 4:26 “*Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa wao, kwa sababu halikuchanganyikana na imani ndani yao waliosikia*” [NKJV]

Muktasari kwa kifupi wa kanuni zilizojitokeza kutokana na somo la 5

- Kwa pamoja:- NINI tunasikia na NAMNA GANI tunasikia vina umuhimu ulio sawa.
- NI NAMNA GANI tunasikia ni pamoja na yafuatayo:
 - a. Kusikia na kuelewa hujumlisha vyote viwili kwa kwa pamoja:- uwezo wa kutambua na kutii kile kilicho sikiwa.
 - b. Kulipokea Neno kwa unyenyekevu
 - c. Kulipokea Neno kwa uchaji, hisia na kulitukuza sana.
 - d. Kulipokea Neno kama ni Neno la Mungu, na siyo neno la mwanadamu, hata ingawa linaelezwa kupitia wanadamu ambao pia tunawapokea.
 - e. Lipokee Neno kwa kuwa na hamu na kisha jitoe kuchunguza kile ambacho umesikia.
- Kanuni hizo hapo juu zitahakikisha kwamba, nguvu ya asili ya Neno itafanya lifae kikamilifu; Neno linaweza kuokoa, [Yak 1:21] na ‘kutekeleza wajibu wake’ [1Thes 1:13]
- Ikiwa umesikia kwa usahihi, utii ndio mwikio pekee unaokubalika.
- Neno la Mungu linafananishwa na kioo likifichua hali zetu za kweli za ndani.
- Linafanya hivi kwa kuangazia ile asili ya Mungu na kwa hiyo tunajiona wenyewe tunapokumbuka hiki.
- Ni kweli tunajiona wenyewe ndani ya Kristo kwa kadri tunavyo endelea kuwepo kabla ya wakati.
- Kila kufunuliwa kwa asili ya Kristo kutoka maandiko kunatupa fursa kwa ajili ya kubadilishwa zaidi kuingia katika ile taswira ya Ki-Uungu kutoka hatua moja ya utukufu kwenda nyingine.
- Kubadilishwa kwa kawaida kunaamshwa kwa hatua mbili: wakati unapoiona asili ya Kristo ndani ya Neno Lake, na wakati unapochukua hatua ya kutii ile kanuni ya kile ulichokiona katika maisha yako.
- Kuona kwa usahihi kunamhitaji mtu awe endelevu katika kusafisha macho yake [uoni wa kiroho] katika fundisho la kitume [birika la siloamu]. Hili ni la muhimu kwani hatimaye husahihisha mitazamo yetu tuliyo nayo ambayo tunaiona katika kioo cha Neno, ili kwamba tusitangulie kuwaza au kuwa na mtazamo usio sahihi wa kile, tunachoona kuhusu asili ya Kristo katika Neno lake.
- Yakobo anaendelea kututia moyo tuweke mbali uovu wote [uchafu wote] na tabia za kukusudia kutenda uovu [uovu] na kuamsha ule ukamilifu wa nguvu na uwezo wa Neno la Mungu. Neno la Mungu ni endelevu kututakasa lakini pia maamuzi ya kuweka mbali tamaa za mwili huzidisha uoni wetu [kuona kwetu] na kutuamshia uwezo kwa ajili ya mabadiliko zaidi.
- Hatimaye [mwishowe] mwana wa ukweli wa Mungu ndiye Neno la Mungu, ambalo limefanyika mwili [Yoh 1:14]. Ikiwa Neno ni kioo, hatimaye maisha yetu yatafanyika kuwa

kioo cha Neno la Mungu kwa wanadamu. Kwa kadri wanavyotuona, wao pia watapokea fursa kwa ajili ya mabadiliko ndani ya taswira ya Ki-Uungu.

Waebrania4:1-3 [NASB]

1. Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.
2. *Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao kwa sababu halikuchanganyikana na imani ndani yao waliosikia.*
3. *Maana sisi tulio amini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyo sema “KAMA NILIVYO APA KWA HASIRA YANGU, HAWATAINGIA RAHANI MWANGU” iwapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.*

Aya hiyo hapo juu inawasilisha mpangilio ufuatao:

- Kuna ‘habari njema’ zinahubiriwa. Hili linahusisha kukubaliwa kwa mhubiri na kile alichokuwa akihubiri.
- Kuna ahadi iliyokwisha tolewa
- Wapokeaji WANALISIKIA hili.
- Kile walichosikia hakijachanganyikana na imani.
- Matokeo yake? Neno ambalo walisikia halijawapa faida.

Tumepoteza nguvu ya utendaji iliyomo katika Neno wakati wote tulipoacha kuchanganya imani na Neno. Hili linasikika kuwa la ajabu kwa sababu kila tendo halisi la kusikia linapaswa lizalishe imani, kwani imani huja kwa kusikia Neno la Mungu.

Jibu pekee linaweza kupatikana katika ukweli kwamba, ikiwa Neno lime SIKIWA kwa makosa au kwa mtazamo potofu na kwa mwelekeo wa ndani kama ilivyooneshwa katika somo lililopita, kwamba hatimaye halitaweza kuzalisha imani ambayo itajidhihirisha kwa nje ndani ya utii.

1. KUISHI KWA IMANI

ANGALIZO: Kwa lengo la sehemu hii, tutashughulika na imani katika hatua za awali. Itagundulika vizuri zaidi katika moduli ijayo.

Kwa pamoja upendo na matumaini, UPENDO ni moja ya maadili matatu ya kuzingatiwa yasiyo na mwisho yaliyo orodheshwa ndani ya maandiko .[1Kor 13:13] Ebr 6:1 unaangazia madhumuni ya imani dhidi ya Mungu mwenyewe [imani kwa Mungu]. Imani katika Mungu au kwa Mungu ni maelezo kamili ya kumtegemea Yeye kwa maisha yote na kwa utendaji wetu wenye matokeo katika maisha haya.

Imani ni zaidi ya dhana ya kiinjilisti ambayo inatufanya tuokoke au kutufanya waaminio. Kwa hakika tumeokolewa kwa imani [Efe 2:8-9] lakini kuna zaidi ya hayo ndani yake kuliko hili. Tunahitaji imani kwa ajili ya wokovu. Hiki ni kiwango cha imani cha kuingia, wakati tunaokoka na kuanza kukua kutoka uchanga kuelekea ukomavu. Katika hatua ya awali ya kuongezeka kiroho, tunakuwa kwa sehemu kubwa kuwa waangalifu katika kuitumia imani kupata vitu kutoka kwa Mungu. Kupata mahitaji yetu, kwa mfano imani kwa Mungu huanza na ni nini Mungu anaweza kukutendea wewe. **Lakini haitaweza kunasa katika kiwango hicho.**

Maandiko, imani **siyo** ki msingi, ni dhana ambayo kiini chake ni kupokea mahitaji kama ilivyo ndani yetu kwaajili ya kumtumaini Mungu kwa ajili ya vitu katika baadhi ya mizunguko. ‘Imani’ imewasilishwa kama ni jambo linalojaza ile sehemu binafsi ya starehe ya baadhi.

Imani ni lazima iwe MTINDO WA MAISHA. Imani haihusiani tu na maisha yetu ya kiroho, lakini pia ya kijamii, kifamilia, ya kiufundi, n.k. yako maandiko manne yanayotujulisha kwamba ‘mwenye haki ataishi kwa imani’

Habak 2:4. *Tazama roho yake hujivuna, haina unyoofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.*

Gal 3:11. *Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria, kwa sababu MWENYE HAKI ATAISHI KWA IMANI.*

Ebr 10:38. *Lakini MWENYE HAKI WANGU ATAISHI KWA IMANI NAYE AKISITASITA ROHO YANGU HAINA FURAHA NAYE.*

Rum 1:17. *KWA MAANA HAKI YA Mungu inadhihirishwa ndani yake toka imani hata imani, kama ilivyo andikwa MWENYE HAKI ATAISHI KWA IMANI.*

Hili neno ‘ishi’ linazingira kila eneo la maisha na utendaji wetu. Wenye haki huishi kwa kanuni za imani. Fundisho la Kibibilia kuhusu imani limeenda mbali kupita kiwango cha kumwamini Mungu kwa vitu. Hii ni sehemu ya imani, lakini kwa watakatifu katika Bibilia, imani iliainisha [elezea] kuhusu kuwepo kwao na maisha yalivyokuwa. Maisha yalikuwa hayaaminiki mbali na imani. Kuwa na imani lilikuwa ndilo sharti la msingi katika maisha.

Kama vile kupumua ni muhimu kwa uhai wa mwili, imani ilikuwa ndiyo kiini muhimu cha uhai kwa watakatifu walioko katika maandiko. Kwa wao imani ilikuwa ndicho kiini mama cha maisha; yaani kiambata muhimu katika kukamilisha mapenzi ya Mungu juu ya nchi. Kuiacha imani ni sawa na mtu kuacha kuwepo. Kukaa mbali na imani inakuwa vigumu kabisa kumpendeza Mungu.

Warumi 11:6. *Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yupo, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafuta.*

Mwanzo wa kuishi maisha ya imani unaanza na kukubali kuwa Mungu yupo: **‘na lazima uamini kwamba Yeye Ndiye’**. Kufanya vizuri katika maisha ya imani, ndilo fungu la wale ambao wana amini katika asili ya Mungu kama ndiye anayewazawadia wale wanao mtafuta Yeye kwa bidii. Mungu atawazawadia wanaomfuata Yeye- wanao mwonea shauku na walio thabiti katika kuliadini neno lake.

Kutokuwa na imani ni kutokuwa na uwezo wa kumpendeza Mungu na hivyo kutokuwa na kinga dhidi ya dhambi na hatimaye kumwasi Mungu. Tendo ambalo moja kwa moja ni kutompendeza Mungu. Rum 14:21-23]...*na chochote kisichotokana na imani ni dhambi.*

Kanisa ambalo ni mwili wa Kristo, linafanuliwa [elezewa] kwa namna nyingi kwa kutumia semi [misemo] nyingi/mingi. Moja wapo ya fafanuzi hizo kuhusu kanisa, ni ‘nyumba ya imani’ Wagalatia 6:10] [KJV]. Kanisa linapaswa liwe na tabia ya kuwa na imani kwa Mungu.

Imani inajieleza kupitia matendo ya utii, na sio kutoamini, mashaka, woga, kiburi au kukosa uvumilivu, na ndiyo kanuni katika mazingira ya mtakatifu wa Mungu katika familia ya imani.

Funzo kutoka Waebrania 11 litaweka wazi jinsi mtu mmoja mmoja alivyotumiwa kwa kufuata kanuni za imani na akaweza kukamilisha majukumu maalum ya mapenzi ya Mungu katika maisha yao, familia zao, kizazi chao na taifa lao.

Kwa watakatifu wa Agano la kale neno ‘imani’ halikuwepo hata katika misamiati yao, wala haikuwa dhana ya kithiolojia. Kwa urahisi walitumika katika majukumu mbali mbali kwa Kufuata kanuni za imani: Mahusiano na Mungu yalikuwa ya karibu mno, na utekelezaji wa mapenzi yake duniani ulikuwa ni wa muhimu sana na hivyo kupewa kipaumbele cha hali ya juu, kiasi cha kutotetereka, kujiamini kulikokuwa thabiti na kuwa na uhakika ndani ya Mungu na Neno lake au ahadi zake vilitosha. Baadhi kama Daudi waliita ‘tegemeo’ wengine tumaini na wengine kama Ibrahimu, kwa urahisi ‘aliamini’

2. IMANI NI NINI?

Waebrania 11:1. *Basi imani ni uhalisia wa mambo yatarajiwayo, ni ushahidi wa mambo yasiyoonekana [NKJV]*

Waebrania 11:1. *Sasa imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni Ithibati [kusadikika] ya mambo yasiyo onekana [NASB]*

Imani=pistis	Uhakika/uumbikaji=hupostasis	Tarajia =Elpizo	Ithibati =Elegchos
“Ushawishi thabiti kushawishika <u>kunatokana na kusikia</u>	Ni hali ambayo ndiyo msingi dhahiri, kujiamini au matajio ya kuaminika	Kutenda kwa shauku	Uthibitisho, ambao kwa huo mtu anatahiniwa au kuhakikishwa

Maneno ‘ya mambo’ katika sehemu ya kwanza ya Waebrania 11:1 hayakuwepo katika nakala asilia za maandiko- katika Bibilia nyingi maneno hayo yalionekana kwa herufi mlazo [italiki/italics] au katika mabano. Mstari huu unapaswa kusomeka “sasa imani ni dutu/uhalisia/uumbikaji utarajiwayo, ithibati ya mambo yasiyo onekana.

Kumbuka:- Suala la imani linahusiana na ushawishi au kujiamini imara/thabiti.

- Muundo wa imani unahusiana na asili ya Mungu mwenyewe [kama inavyooneshwa kwa neno dutu/uhalisia/uumbikaji]
- Uhakika huu umejikita ndani na chimbuko lake, ni kutokana na ile asili halisi na tabia ya Mungu mwenyewe.

Neno lililotafsiriwa kama ‘dutu’ [KJV] au ‘uhakika’ [NASB] ni istilahi ya Kiyunani ‘hupostasis; neno ambalo linatumika kuelezea ule uhalisia na asili ya asili ya Mungu mwenyewe (soma Waebrania 1:3).

Waebrania 1:3. *Yeye kwa kuwa ni mng’ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu.*

Maana kamili ya 'hupostasis' ni kile ambacho kinaweka msingi dhahiri, kwa hiyo ni ukweli, asili, jambo, kile ambacho ndicho kiini cha kitu, kuanzia hapa, uhakika ulio hakikishwa, kujiamini, jambo, ambacho bado kipo katika muonekano wowote, uhakika, asili muhimu.

“Wakati wababa wa kanisa la mwanzo walipokuwa wanajaribu kuelezea kuwa, Ukristo una Mungu mmoja katika nafsi tatu, walisema kwamba, Mungu ni Mungu wa nguvu [**hupostasis**]. Hakuumbika kutokana na kitu chochote. Zile nafsi tatu katika utatu wa Mungu zina uweza ulio sawa ndani yake na uumbikaji wake ni sawa.

Hivi ndivyo ulivyo ufanyikaji wa Mungu. Kila sehemu ya utatu wa Mungu ina uzito na ufanyikaji ulio sawa; lakini tabia ya ufanyikaji huo inaweza ikajionesha kiutofauti.

Huu ndio msingi ambao juu yake sura ya Mungu inajionesha. Kwa ndani, ni lazima tubebe ufanyikaji wa Ki-Uungu ambao unabeba na kuelezea tabia zetu. Huu ndio msingi ambao juu yake maisha yako yalijengwa. Huzingira kila kitu katika maisha yangu/yako kinachojitokeza kama ndio sura ya Mungu.

Huu ndio msingi usiotikisika wa maisha yako. Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo. Imani ndio njia ya uhakika huo ambao ndio asili ya vyote alivyonavyo Mungu.

Thamo Naidoo: Kipindi cha 19 katika shule ya huduma ya kitume [ASOM] mwezi Machi 2011.

Kwa sababu hiyo, imani ambayo ni msimamo au kusadiki kuliko imara, ina malengo na muundo au kanuni au uumbikaji wa asili ya Mungu.

Kushiriki asili hii ya Mungu kunatokea wakati tunapoamua kutii kile tulichokwisha sikia kuhusu asili hii na maagizo, vikiwasilishwa kwetu kupitia neema katika Neno. Asili ya Mungu huakisi kwetu kwa pamoja tabia na dhamira au malengo yake.

Haiwezekani utimize lengo lake bila ya kufanana na tabia yake kwanza. Lengo la kwanza kabisa la imani kupita yote ni MUNGU MWENYEWE- 'ufanyikaji' WAKE au 'hupostasis' yaani Umuhimu wa asili Yake. Baada ya hapo hutumiwa katika mwitikio wa utii katika kuyatii matarajio Yake kwa ajili yetu na pia kutekeleza majukumu Yake mahsusi tuliyopewa sisi.

Kiashiria muhimu cha kuwepo kwa imani ni utii. Mtu wa imani ni mtu wa utii aliyejawa na kujiamini imara, kuhusiana na uwakilishaji wake wa tabia ya Mungu na katika utekelezaji wa mapenzi Yake, kwa masharti ambayo kwamba, kwa kawaida kuna upinzani dhidi ya mapenzi ya Ki-Uungu. 'ufanyikaji/uumbikaji' [ufanyizi] huu yaani '**hupostasis**, ni wa msingi na ndio unaoshikilia ule uhai wa kujiamini, na utajionesha wenyewe katika kuwa na imani imara kwa kile ambacho KIMENENWA na Mungu, hata mbele ya uso wa ushahidi wa nje wa mwilini unaopinga.

Kwa kutilia maanani maana ya maneno ya ufafanuzi huo hapo juu, tunaweza tukaifafanua imani kama ifuatavyo:-

Imani ni kusadiki au msimamo ulio imara sana au ushawishi ulio jikita katika kitu alichokisema Mungu, inatokea kwa kusikia 'rhema' yaani Neno la Mungu, ambalo linatuwasilishia 'neema' ambayo ni umbile halisi la Ki-Uungu la Mungu, ambaye ni Roho alivyoumbika.

Kuamini huku siyo msimamo wa kiakili wa kuamini na kuweka makubaliano, isipokuwa ni ukweli wa Ki-Uungu, yaani ile asili ya Mungu ndani ya mtu ambayo ina fungamanisha na kuzalisha matarajio ya kujiamini na matumaini.

Tumaini humsababisha mtu atende akiwa na shauku kali sana kwa nje katika kutii, hata bila ya kuhakikisha au kuwa na ushahidi wa kuonekana au ulio dhahiri, kwa sababu imani hutoa maono [taswira] ndani ya ukweli usio onekana na usio wezekana. Ukweli huu au maono [taswira] haya/hii yana/ina heshimiwa kana kwamba yameshatimiza mambo yaliyokwisha nenwa na Mungu.

[Marko 11:22](#), Anasema, “*Mwaminini Mungu*”. Baadhi ya matoleo ya Biblia kama vile lile la Modern King James [toleo la mfalme Yakobo la sasa] lina elezea hili kama ‘kuwa na imani ya Mungu’ - kiuhalisia ni kuwa na aina ya imani ya Mungu.

Ikiwa imani inazalishwa kwa kuwa wazi na kujiachilia na kuamini kile ambacho anasema Mungu, na ikiwa Mungu na Neno lake ni wamoja, basi tungeweza kusema kwamba, wakati ule ulipo kubali toka ndani kwamba, alichosema Mungu kitatokea, basi kupitia hili unapokea kipaji cha Imani yaani uwezo wa kumtumani Yeye pasipo kutetereka.

Biblia ya ‘The message Bible (Bibilia ya Ujumbe) inaweka katika [Mark 11:22](#) kwa namna hii ‘Yesu alikuwa ndiye ukweli wote: “[Shikilia maisha ya Mungu. Kwa kweli yashikilie...](#)”

3. IMANI NI KUONA UPEO USIO ONEKANA WA UMILELE

[2Kor 5:7](#). *Maana twaenenda kwa imani, si kwakuona*

Angalia Waebrania 11:1 Unafafanua imani kwa kusema kwamba ni bayana ya vitu VISIVYO ONEKANA. Hii inamaanisha tu kwamba, hakuna ushahidi unao onekana kwa nje kwa ajili ya kukubaliana na ile imani mahsusi iliyo imara au ushawishi kuhusu ahadi au agizo la Mungu. Ubayana huo umejikita katika uhalisia usio onekana na ambao bado haujadhihirika katika ulimwengu wa asili, unao onekana na katika ujuzi wa kibinadamu. Hata hivyo ubayana huo una nguvu sana, kiasi kwamba pamaja na kuto kuwepo kwa uhalisia wa asili wa ahadi, mtu mwenye imani kwa Mungu ambaye ndiye mwenye kuahidi, huichukulia ahadi hiyo kuwa imeshatimia. Ubayana una nguvu sana.

Imani haitegemei tunavyo viona kwa nje- inategemea Neno la Mungu. Baada ya hili, ahadi ile inapokuwa ni uhalisia unao onekana, kwa uhakika huo ndiyo matokeo ya ‘imani’ yetu katika kukamilishwa kwake hata kabla haija tokea.

[2Kor 4:18](#). *Tusiviangalie vinavyo onekana, bali visivyo onekana. Kwa maana vinavyo onekana ni vya muda tu, bali visivyo onekana ni vya milele.*

Kule kusema ‘kuona ni kuamini’ kwa mtazamo wa kiimani wa kibibilia siyo kweli nani kujiweka katika nafasi ya kutokuwa na imani. Tomaso alitaka amwone Yesu katika mwili kabla hajaamini kwamba kweli amefufuka kutoka kwa wafu [soma Yoh 20:25-29]

Imani haina cha kukitegemea au haihitaji ushahidi wowote ili iwe na uhai wenye nguvu. Inachohitaji pekee ni Neno kutoka kwa Mungu. Imani imepandikizwa na kujikita ndani ya

ulimwengu usioonekana katika upeo wa roho yaani ulimwengu wa kiroho. Imani hufuata mkondo wake na inashawishika kwa hakika zisizo onekana kwa macho ya asili ya kibinadamu.

Kwa uelewa huu, imani zaidi sana ni utendaji wa ufalme wa Mungu, ambao unatenda kazi kutoka ulimwengu usio onekana na inafanyika mwili katika maisha yetu ya nyama. Imani siyo wazo la kutamani au tafakari utupu, ila ni **uumbikaji** wa KI-UUNGU ni ukweli halisi.

Pata fikra kuihusu. Ikiwa ushawishi au kusadiki ni ukweli halisi wa asili ya Mungu mwenyewe ulioshikamana ndani yako kama mwana wake, na asili hii ya Mungu ni ya milele na ni roho, basi utendaji wa imani kwa nje pia unategemea kutazamwa kiroho au kuonwa ndani ya upeo huo ambao ndani yake Mungu mwenyewe anakaa yaani ule umilele.

4. IMANI INAKUJAJE?

Ki-elelezo cha imani ni Mungu. Tunayo imani KATIKA MUNGU au imani ya Mungu. Mungu na Neno au ahadi zake ni wamoja. Wakati anaposema, anajielezea Yeye Mwenyewe. Huwezi ukamtenganisha jinsi alivyo Yeye na Neno lake. Wakati anapo nena na kutoa maagizo mahsusi au ahadi kwetu, kila tendo la utii wa kusikia ndani yetu huzalisha imani ya kuamini kwamba, kile alichogiza au kuahidi kina uwezekano wa kutendeka au kutimia. Imani yetu katika Neno, kwa kile alichosema, ni ushawishi wenye nguvu ambao huzalisha ari yenye matarajio na matendo hata katika hali ya nje yenye kuonesha kupinga. Hili linakuwa hivyo kwa sababu Neno Lake ndilo mwakilishi wake Mwenyewe kabisa kwa asilimia mia moja na ni la kutumainiwa, kuaminiwa na kutegemewa.

***Warumi 10:17.** Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*

Ikiwa imani inakuja kwa kusikia Neno Lake, mtu anaweza akaipata imani wakati wowote ‘ANAPOLISIKIA’ NENO LAKE. Unenaji mwingine wowote wa Mungu ni lazima uwe endelevu na usio pingana na kile alichokwisha weka wazi kupitia Neno lake ambalo ni endelevu na lenye kuakisi asili yake.

Imani ya kweli ya kibibilia inainuka kutokana na kusikia **rhema** ya Neno la Mungu kutoka kwa ubaba wa kiroho wenye neema ya kitume wa kweli na ulio halali.

Ibrahimu aliamini na alikuwa na imani kwa Mungu kufuatana na kile alichosikia Mungu akinena. Unenaji wa Mungu ulizalisha imani ndani yake.

***Warumi 4:18.** Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonena, ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

5. UTII- NDIO MAELEZO YA IMANI

***Yakobo. 2:26.** Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.*

‘Matendo’ hapa, ni kiashiria cha nje cha matendo ya utii kwa sababu ya kile ulichosikia ambacho kimezalisha imani ndani ya moyo na katika maisha yako. Wakati unapokuwa na imani kwa Mungu KWA SABABU ya Neno Lake kwako, matendo au kazi zako zitakuwa

katika kuoa nishwa na kunyooshwa ili ziende sawa sawa na imani yako. Utii wako na matendo yako ya nje yenye kufaa au kazi ndio ushahidi wa kuwepo kwa Imani. Matendo yangu ya nje yatatoa ishara kwa uwepo na uthamani wa imani iliyomo ndani yangu.

Ikiwa hakuna mojawapo ya matendo yako ya nje lisilokubaliana [fanana] na imani unayodai unayo, basi huu ni uthibitisho kwamba hakuna imani iliyo hai na tendaji ndani yako.

Yakobo 2:14, ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Imani yake humuokoa?

Kabla ya kuanguka kwa Adamu kule bustanini, kulikuwa hakuna haja ya imani. Imani ni mhimili wa ukweli ambao haujaanguka. Alichopaswa kufanya Adamu ni KUMTII Mungu kabisa. Mara tu baada ya macho yake kufunguka na kujua jema na baya kwasababu ya dhambi, aliingizwa katika ulimwengu wa uwiano wa kufikiri na kujadili maagizo au mapenzi ya Mungu. Lengo la mwisho la imani ni kurejesha na kuzalisha utamaduni wenye nguvu kamili na utii usio tiliwa mashaka kwa maagizo yote ya Mungu.

6. MAADUI WA IMANI

Katika somo lijalo tutachunguza kwa kinagaubaga ni nini vilivyo vikwazo vya imani. Kinachotosha tu kwa sasa, ni kuorodhesha kweli ambazo zinazuia upokeaji na /au ukuaji wa imani.

- Kutosikia na kutii lile Neno linaloachiliwa kupitia uangalizi wako wa kiroho.
- Kulipuuza Neno, Neno la rhema
- KUTO AMINI ni kukosa imani
- MASHAKA ni kiashiria cha kusitasita- kuenenda kati ya kuamini na kutoamini
- DHANIO/KUDHANIA ni imani potofu, haina msingi wa uhakika katika Neno au kutoka kwa Mungu.
- Pupa/haraka huzaa Ismaeli kitu kilichotengenezwa kibinadamu na kuonekana kama ni utoaji wa Mungu au kama ni matokeo ya imani [kuamini].
- Woga ni imani inayoelekea upande pinzani [kinzani].

Ukweli wa kwanza katika orodha hiyo hapo juu ndio hasa tunataka tuangazie hapa.

7. HESHIMU UANGALIZI WAKO WA KIROHO NA UWE NA UTII KWA NENO LILILOACHILIWA HUSAWAZISHA IMANI.

Kumbuka kwamba Neno la Mungu linapaswa kupokelewa sio kama neno au shauri la mtu - **1Thes 2:13**. Ikiwa utapokea shauri la mtu, halitakuzalia imani. Kwa kulipokea Neno kama wazo la mwanadamu inaweza ikawa ni kwasababu unamdharau yule mtu ambaye kupitia yeye Neno linakujia wewe, na hivyo kwasababu ya utambuzi usio sahihi wa yule mtu anaye kuletea Neno unapunguza nguvu ya lile Neno.

Mahali ambapo mjumbe wa neno hapokelewi kwa heshima na Baraka, lile Neno ambalo yeye me/ke analiachilia halitasikika kwa usahihi na kwamba imani haizalishwi na sababu inaweza kuwa ni kuto tii.

Matayo 13:54-58

54. *Na alipofika nchi yake, akawafundisha katika sinagogi lao, hata wakashangaa wakasema, huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii?*
55. *Huyu si mwana wa seremala? Mamaye si yeye aitwaye Mariamu? Na nduguze si Yakobo, na Yusufu, na Simioni, na Yuda?*
56. *Na maumbu yake wote hawapo hapa petu? Basi huyu amepata wapi haya yote?*
57. *Wakachukizwa naye Yesu akawaambia, Nabii hakosi kupata heshima isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwake mwenyewe.*
58. *Wala hakufanya miujiza mingi huko, kwa sababu ya kutokuamini kwao.*

Katika aya hii maneno ya Yesu hayakuwa na matokeo yaliyo tarajiwa ya kuzalisha imani na utii. Badala yake, kutokuamini kuliongezeka. Kwanini? Hawakuniheshimu kama ni mwana wa Mungu aliyekuwa katikati yao, lakini wakamshusha hadi kuwa mtu wa kawaida mwana wa seremala, walimvunjia hadhi uwakilishi wake wa Uungu katikati yao. Hivyo, kwa sababu ya wao kumshushia hadhi yake na utambulisho wake, maneno aliyoyanena yaliumba chuki ndani yao badala ya imani.

Wakati mtu wa Mungu hapokelewi kwa usahihi na hapewi hadhi yake na kuheshimiwa kama ni mdomo wa Mungu kwa watu alio itiwa awatumikie, hatimaye lile Neno atakaloliachilia litaumba hatia na halitazaa Imani. Matokeo yake, kwa muktadha huo, kazi za Mungu zinakuwa vigumu kuzisimamia na zina kwama. Imani inapitia moja kwa moja katika heshima ya hali ya juu kwa ajili ya unenaji wa Bwana kupitia baba wa kiroho aliyewekwa juu ya maisha yako ili anene Neno lake kwako. Mahali ambapo hili linakosekana, kazi katika ulimwengu wa kiroho na miujiza ya Mungu vinaondolewa.

Kwa maelezo yanayofuata kule kutambuliwa kwa Yesu kwa hali ya juu na yule akida, kunatiliwa maanani na Yesu kwa imani kubwa. Heshima inalinganishwa na imani kubwa.

Luka 7:1-10

1. *Alipokwisha kuyamaliza maneno yake yote masikioni mwa watu, aliingia Kapernaumu.*
2. *Na mtumwa wake akida mmoja alikuwa hawezi, karibu na kufa; naye ni mtu aliyempenda sana..*
3. *Aliposikia habari za Yesu, alituma wazee wa Wayahudi kwake kumwomba aje amponye mtumwa wake.*
4. *Nao walipofika kwa Yesu, walimsihi sana wakisema, amestahili huyu umtendee neno hili;*
5. *Maana, analipenda taifa letu, naye alitujengea sinagogi.*
6. *Basi Yesu akaenda pamoja nao. Hata alipokuwa si mbali na nyumba yake, Yule akida alituma rafiki kwake, akamwambia Bwana, usijisumbue, maana mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu;*
7. *Kwa hiyo nilijiona sistahili mwenyewe kuja kwako; lakini, sema neno tu, na mtumwa wangu atapona.*
8. *Kwa kuwa mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, nenda, huenda; na huyu, njoo, huja; na mtumwa wangu, fanya hivi, hufanya.*
9. *Yesu aliposikia hayo alimstaaambia, akaungeukia mkutano uliokuwa ukimfuata, akasema, na waambia, hata katika Israeli sijaona imani kubwa namna hii.*
10. *Na wale waliotumwa waliporudi nyumbani, wakamkuta Yule mtumwa ni mzima.*

Utamaduni wa heshima na staha ya hali ya juu kwa wale ambao wanaleta Neno kwako ndilo hitaji la msingi kwa ajili ya Neno la Mungu kuzaa imani ndani yako. Mahali pasipokuwa na kumheshimu mjumbe aletaye Neno, ujumbe ulio ndani ya Neno huumba hatia na kuikana imani ambayo ni kwa ajili ya uwakilishwaji sahihi wa ile asili ya Mungu na pia kwa ajili ya utii na matendo makuu katika utekelezaji wa makusudi yake.

Wale wanafunzi wawili waliokuwa wanasafiri kuelekea Emau, walimpa heshima ya hali ya juu mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kuwafungulia maandiko, akifafanua asili na kazi za Kristo zilizomhusu katika siku ambayo walikuwa wangali wanaishi [Luk 24]. Kwa kweli walimpa ishara kwa kupunga mkono kumkaribisha yeye aendelee kukaa nao wakati ule alipoonesha kama anaendelea mbele kuelekea mji mwingine. Mtu huyu alikuwa ndiye Kristo, lakini macho yao yalikuwa yamefumbwa kiasi cha kuto mtambua ni Yeye. Wakiwa wametilia mashaka ushuhuda wa mwanamke ambaye alikuwa ameusikia ushahidi wa malaika pale kaburini kwamba Yesu alishafufuka kutoka kwa wafu. Yesu aliwafafanulia kama wajinga na wazito wa moyo kuamini.' Ni pale tu Yesu alipo jifunua yeye mwenyewe kwao katika kuumeza mkate [alama ya kuji funua Yeye mwenyewe), ndipo sasa wakaamini. Kitu ambacho ushuhuda binafsi kutoka kwa nafsi ya mwanamke aliyeungwa mkono na ushahidi wa malaika haukuweza kufanya. Ni NENO LA MUNGU likifunua 'dutu/uumbikaji ya/wa Ki-Uungu au Asili ya Kristo liliweza kufanya. Imani huja kwa kusikia Neno na kupitia hilo Kristo anaonekana. Baada ya kumwona Kristo, wanabadilishwa kuwa ndani ya sura ya Kristo, kuamini kwao na imani ilikuwa zaidi kuliko tu ushawishi wa ndani wa kiakili wa ukweli mahsusi/K.v. Yu hai], lakini ilizaliwa na kuanzishwa kwa ufunuo wa ajabu wa nafsi yake kutoka kwenye Neno. Imani siyo zoezi la kiakili-lakini zaidi sana ni msimamo wa kiroho ulio hodari wa kuweza kuona ndani ya upeo wa milele wa MUNGU MWENYEWE. Wale wanafunzi wawili walirudi Yerusalemu ili sasa waweze kutoa taarifa kwa wengine. Siyo kwa msingi wa ushahidi wa kimalaika, isipokuwa wao wenyewe, walipokutana na kufunuliwa kwa Kristo kutoka katika Neno lake. Imani yako hutiririka kutoka katika mfumo wako wa nafsi ya Mungu, kutoka katika Neno lake. Ukosefu wa imani unaashiria kutokuwepo kwa ufahamu wa asili ya Mungu.

Waebrania 11

- 1. Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*
- 2. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.*
- 3. Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*
- 4. Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena.*
- 5. Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana kwasababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa anashuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.*
- 6. Lakini pasipo imani haiwezekani kumpandeza Mungu; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yupo na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*

7. *Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu kwa habari ya mambo yasiyo onekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.*
8. *Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.*
9. *Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.*
10. *Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambaye mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*
11. *Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba, alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu.*
12. *Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.*
13. *Hawa wote wakafa katika imani, wasizozipokea zile ahadi, bali wakazona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.*
14. *Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe.*
15. *Na kama wangaliikumbuka nchi ile waliyotoka, wangalipata nafasi ya kurejea.*
16. *Lakini sasa waitumaini nchi iliyo bora, yaani ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao, maana amewatengenezea mji.*
17. *Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa manawe, mzaliwa pekee;*
18. *Naam, yeye aliyeambiwa, katika Isaka uzao wako utaitwa ;*
19. *Akihesabiwa ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano.*
20. *Kwa imani Isaka akawabariki Yakobo na Esau, hata katika habari ya mambo yatakayo kuwa baadaye.*
21. *Kwa imani Yakobo, alipokuwa katika kufa, akawabariki kila mmoja wa wana wa Yusufu, akaabudu akiegemea kichwa cha fimbo yake.*
22. *Kwa imani Yusufu, alipokuwa amekaribia mwisho wake, alitaja habari ya kutoka kwao wana wa Israeli, akaagiza kwa habari ya mifupa yake.*
23. *Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri; wala hawakuogopa amri ya Mfalme.*
24. *Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao;*
25. *Akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo.*
26. *Akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo.*
27. *Kwa imani akatoka Misri; asiogope ghadhabu ya mfalme, maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyeonekana.*

28. *Kwa imani akafanya pasaka na kule kunyunyiza damu ili Yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wao.*
29. *Kwa imani wakapita kati ya Bahari ya Shamu, kama katika nchi kavu; Wamisri walipojaribu kufanya hivyo wakatoswa.*
30. *Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba.*
31. *Kwa imani Rahabu Yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapepelezi kwa imani.*
32. *Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitisha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yefta na Daudi na Samweli na za manabii;*
33. *Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya samba,*
34. *Walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga, walitiwa nguvu baada ya kuwa dhairifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni.*
35. *Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufu ulio bora,*
36. *Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani.*
37. *Walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya;*
38. *[watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao], walizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.*
39. *Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi;*
40. *kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.*

**MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA
KIKUNDI.**

1. Mtu anawezaje kupata imani au kukua katika imani?
2. Mwenye haki ataishi kwa imani. Maelezo haya yana maanisha au yana umuhimu gani?
3. Ni nini mtazamo na kusudi la imani?
4. Imani inathibitikaje katika maisha ya mtu? Ni nini matokeo ya hisia yanayotazamiwa ya imani?
5. Elezea namna heshima kwa mtu aliye baba wa kiroho ambaye anakuletea Neno la Mungu inavyoweza kulinganishwa na imani?
6. Changanua Waebrania 11 sura inayoitwa ya imani. Tenganisha kikamilifu ni nini kila mmoja aliyetajwa hapo alivyoitumia imani. Uchambuzi wako huo unatoaje mtazamo wa imani ambao unaweza kuwa tofauti sana kutokana na uelewa finyu na mwembamba wa imani kama vile, imani kwa ajili ya kupata vitu ilivyo kwa ujumla katika kanisa la leo.

SAUTI NDANI YA SAUTI.**Lengo : Mungu hunena kupitia Baba yako wa kiroho.****MAMBO MUHIMU YA KUTAFAKARI KUTOKA KWENYE MADA ZILIZOTANGULIA.**

- Imani ni dutu / uumbikaji halisi ya/wa ki-uungu ya asili ya Mungu, inayojitokeza kupitia kusikia kwa usahihi Neno la Mungu.
- Imani inakomazwa ndani yako kupitia kurudia rudia kwa uwazi kwa baba halisi mwenye Neema ya kitume, ambaye kwa huyo daima utaendelea kusafishwa kwa Neno la Mungu linalokujia.
- Heshima ya kuenzi ubaba wa kiroho kama unavyoakisiwa ndani ya heshima sahihi ya uthamani wake (me/ke) na uwakilishi wa ki-uungu kwa upande mmoja na kukubalika /kuelewa kwa ukweli kwamba, maneno yake baba (me/ke) kwa uhakika ni maneno ya Mungu kwa upande wa pili, na yanafaa kwa ukuaji wa imani na kutii.
- Kusudi la mwisho kwa kila mwana wa Mungu ni kuumba Asili ya Baba wa Mbinguni kwa kila mtu.

NENO LA MUNGU NDANI YA SAUTI YA BABA YAKO WA KIROHO.

Mungu ni Roho na amejaa NEEMA “ROHO” haina umbo la kimwili wala umbile. Haionekani na haiwezekani kuiona kwa macho ya nyama. Roho ni kama vile upepo, ni pumzi au ni hewa iliyo katika mwendo. Neema ni anatomia ya hulka au tabia ya Mungu kama Roho. Mungu ambaye ni Roho hana mdomo wa nyama. Anawatumia wanadamu walioko duniani ambao kwa kupitia wao anaweza kunena Neno Lake. (Rejea kwenye mwongozo wangu juu ya NEEMA kwa ufafanuzi zaidi.)

Warumi 10:14-15a

14. Basi wamwiteje yeye wasiye mwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri?

15. Tena wahubirije wasipo pelekwa?

Neema ya Mungu inafafanuliwa au imo ndani ya yale Maneno anayonena Mungu. Neema inawekwa ndani ya watu kupitia Neno la Mungu linalonenwa kwao. Wakati watu wanapolitii Neno hili, neema inaamshwa katika maisha yao. Ubaba wa kiroho kimsingi huchukua nafasi yake kupitia kuachiliwa kwa Neno la Mungu kutoka kwa Baba wa kiroho kwenda kwa mwana wa kiroho. Siyo kila mtu kwa namna yake, mwenye uwezo wa kutosha wa kuwa baba wa mtu mwingine. Ni kupitia tu katika neema ya baba wa kiroho iliyo ndani ya baba wa kiroho aliyeko duniani ambaye ubaba wa kweli wa kiroho huchukua nafasi yake. Neema hii hutolewa kupitia njia ya Neno la Mungu kutoka kwa baba kwenda kwa mwana. Hivyo ni sauti ya Baba wa Mbinguni inayo jipambanua ndani na kwa kupitia sauti ya baba wa kiroho hapa duniani

ambaye kwa kweli ndiye baba yako. Wakati baba yako wa kiroho anaponena unapaswa utambue sauti ya Mungu iliyomo ndani yake, yaani tambua “ile sauti iliyomo ndani ya sauti.” Kumbuka kwamba Wathesalonike walilipokea lile neno ambalo waliletewa na Paulo kama Neno la Mungu, na siyo neno la mwanadamu.

1 Wathesalonike 2:13

Kwa sababu hiyo tunamshukuru Mungu bila kukoma kwa kuwa ,mlipopata lile Neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea kama si kama neno la wanadamu bali kama Neno la Mungu, na ndivyo lilivyo kweli kweli, litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.

YOHANA ALIGEUKA ILI AIONE ‘SAUTI’.

- 10. Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana, nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu.*
- 11. ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo ukayapeleke kwa hayo makanisa saba. Efeso, na Smirna, na Pergamo , na Thiatira na Sardi , na Filadefia, na Laodikia.*
- 12. Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami na nilipogeuka niliona vinara vya taa saba vya dhahabu.*
- 13. na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa mwanadamu amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.*

Zingatia hapa kwamba, Yohana anasikia sauti nyuma yake, kisha anageuka ili AIONE sauti (sio kusikia sauti). Wakati anapogeuka anaona **vinara vya taa saba vya dhahabu** ambavyo ni **alama ya uwasilishwaji wa fundisho kamili. Vinara vya taa ni taswira ya fundisho la kitume.** Katikati ya vyote hivi anamwona mmoja kama mwana wa mwanadamu, hivyo ile sauti aliyosikia ambayo sasa anageuka ili aione, ilitoka kwa mwanadamu (mwana wa mtu). Baba yako wa kiroho wa hapa duniani ni mwanadamu mwenye mimba ya fundisho kamili la kitume, ambaye wakati anaponena katika maisha yako, inakuwa kama ni kuamshwa kinabii (kama inavyoashiriwa na maneno, ‘sauti ya baragumu) huwezi kudharau ‘sauti ‘ yake. Ni kubwa na ina uwezo wa kukubadilisha uwe katika ukamilifu wa kusudi na hatima yako.

Mungu anawasiliana na kanisa lote kupita BABA wa kiroho aliyewekwa juu ya kanisa kama unavyoonekana ushahidi katika mpangilio wa mistari hiyo hapo juu. Neno la Mungu na sauti yake kwako vimefungiwa ndani ya baba yako wa kiroho.

Wakati baba wa kiroho anazungumza nawe anazungumza kama mwakilishi wa Roho wa baba wa Mbinguni.

Matayo 10:20– Kwa kuwa si ninyi msemao bali ni ROHO WA BABA YENU asemaye ndani yenu.

2Sam. 23:2-Roho wa Bwana alinena ndani yangu , na Neno lake likawa ulimini mwangu.

Malaki 2:7- Kwa maana yapasa midomo ya kuhani ihifadhi maarifa, tena yawapasa watu kuitafuta sheria kinywani mwake, kwa kuwa yeye ni mjumbe wa Bwana wa majeshi.

Waaminio wa Galatia waliompokea Paulo, baba yao wa kiroho kama Kristo mwenyewe (Wagalatia 4:14) kusudi lake lilikuwa ni kumuumba Kristo ndani yao. (Wagalatia 4:19). Kwa ajili ya hili kukamilishwa ilipasa wamuone Yeye siyo kwa upeo wa kimwili, bali wamwone kama Kristo anayekuja kwao.

Wagalatia 4:12:20

12. *Ndugu zangu, nawasihi iweni kama mimi, maana mimi ni kama ninyi. Hamkunidhulumu kwa lolote.*
13. *Lakini mwajua ya kuwa naliwahubiri injili mara ya kwanza kwa sababu ya udhaifu wa mwili.*
14. *na jaribu lililowapata katika mwili wangu hakulidharau wala kulikataa, bali linipokea kama malaika wa Mungu kama Kristo Yesu.*
15. *Ku wapi , basi kule kujiita heri? Maana nawashuhudu kwamba , kama ingaliwezekana, mngaling'oa macho yenu mkanipa mimi.*
16. *Je ! Nimekuwa adui yenu kwa sababu nawaambia yaliyo kweli?*
17. *Hao wana shauku nanyi, lakini si kwa njia nzuri bali wanataka kuwafungia nje, ili kwamba ninyi mwaonee wao shauku.*
18. *Navyo ni vizuri kuonewa shauku katika neno jema siku zote wala si wakati nikiwapo mimi pamoja nanyi tu.*
19. *Vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.*
20. *Laiti ningekuwapo pamoja nanyi sasa na kuigeuza sauti yangu! Maana naona shaka kwa ajili yenu*

Angalizo : Mstari wa 19 una lengo la hatimaye la baba wa kiroho yaani mpaka Kristo aumbike ndani yenu.

Neno “*mlinipokea*” katika Wagalatia 4:14 ni “*dehomia*” linalo maanisha kukubali zawadi kwa uangalifu na kuwa na utayari wa kupeleka kwa mtu mwingine kitu kilichowasilishwa au kilicholetwa. Mtu anayefuata hupokea, hukubali kwa nia na kwa moyo yaani huhisani na huthibitisha, hushikilia au hufuata. Hivyo Wagalatia ndani ya mioyo na fahamu zao, kwa moyo mmoja walikubali na hivyo kumkumbatia Paulo katika uwakilishi wake kwa ajili ya Kristo, kwa kuwaletea neema ya baba kwao.

Kwa kweli Wagalatia walimpokea Paulo kama ni malaika wa Mungu- ingawa hata hivyo KRISTO MWENYEWE alikuwa anawajia (Wagalatia 4:14) Paulo alikuwa ndiye mwakilishi wa Kristo kwao, wakati walipomuona Paulo , walitazama zaidi ya ubinadamu wake, udhaifu na mapungufu ya kibinadamu na wakamuona KRISTO MWENYEWE akiwa anasimama ndani yake. Uthibitisho wa hali ya juu wa upendo na utiifu kwa baba yako wa kiroho ni lazima upimwe juu kama unampokea au humpokei, mwitikio na uhusiano wako naye kama ambavyo ungefanya kwa Kristo mwenyewe. Paulo alisema, ‘Nifuateni mimi kama ninavyomfuata Kristo yaani anasema “Ikiwa utanifuata mimi utakuwa unamfuata Kristo. Ona ukubwa wa utii wao kwa maneno yake kwa sababu ya mstari wa 15 ‘mngaling’oa macho yenu mkanipa mimi” Kuna wakati kanisa la Wagalatia lilienda mrama kutokana na mafundisho ya Paulo na kukumbatia sheria za Kiyahudi. Kwa hili Paulo, katika kitabu cha Wagalatia aliwaonya na kuwatia adabu (adibisha). Kama sehemu ya kauli ya marekabisho (marudia) yake, aliwathibitishia namna walivyompokea yeye mwanzoni kama kumpokea Kristo mwenyewe.

Kumbukumbu yake kwao kama watoto katika mstari wa 19 inaonesha wazi ubaba wake kwao . Hili linatuhimiza kuwathamini baba zetu wa kiroho walio juu yetu kama ndio wawakilishi wa Kristo. Kusihhi kwa Paulo alikofanya kwa Wagalatia ni jitihada zilizofanywa au ni kichocheo kwa iliyokuwa imeimarishwa ya ubaba wake juu yao. Hivyo kama baba kwao angeweza akasema kwa maneno makali kwao (k.v nimefadhaishwa, nina wasiwasi, nina mashaka) kuwahuu ninyi. Mst wa 20. Angeweza kusema kitu cha namna hiyo kwa Wakorintho.

1Wakorintho 4:14-15

14. Siyaandiki hayo ili kuwatahayarisha, bali kuwaonya kama watoto niwapendao.

15. Kwa kuwa uwapokuwa una waalimu kumi elfu katika Kristo walakini hamna wababa wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya injili.

Wakati maonyo na marudia yanapokuja kutoka kwa baba yako wa kiroho ona ile Roho ya Baba wa mbinguni ndiyo iliyomo ndani yake.

Mathayo 10:20

Kwa kuwa si ninyi msembo bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.

MUONE BABA YAKO WA KIROHO KAMA ‘MALAIKA’- MJUMBE KUTOKA KWA MUNGU ALIYETUMWA KWAKO.

Zingatia jinsi Wagalatia walivyosema na kumpokea Paulo kama malaika. Lakini hili siyo muhimu kumaanisha kuwa walimstahi yeye kama kiumbe wa kiroho aishiye mbinguni. Neno la Kiyunani linalotafsiriwa kwa Kiingereza kama malaika *linamaanisha* yeye ambaye analeta ujumbe kutoka kwa Mungu.

Malaika =Angel = angelos *maana yake ni*= Mjumbe anayetumwa ili atangaze, afundishe, atekeleze au apeleleze chochote.

Katika kitabu cha ufunuo, wale malaika wa makanisa yale saba ni rejea ya wababa wa kiroho au viongozi wa makusanyiko yale; wawakilishi au wajumbe wa Mungu kwa yale makanisa. Ona hapa kwamba, Mungu atanena kiushirika kwa kanisa zima kupitia mjumbe mteule (aliyetengwa) au malaika ambaye amemweka aongoze kanisa hilo yaani awe ndiye mwakilishi Wake .

Ufunuo 2:1“*Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika;*

Ufunuo 2:8- “*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika;*

Ufunuo 2:12-“*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Pergamo andika;*

Ufunuo 2:18-“*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatra andika;*

Ufunuo 3:1-“ *Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika;*

Ufunuo 3:7 “*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadefia andika;*

Ufunuo 3:14“*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika;*

Musa aliwekwa kama malaika wa kuwaongoza wana wa Israel (Israel ni picha ya kanisa lililokuwa jangwani (nyikani) soma Matendo ya Mitume 7:38.

Kutoka 23:20-22

20. “Tazama mimi namtuma malaika aende mbele yako ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipo kutengenezea.

21. “Jitunzeni mbele yake, mwisikize sauti yake, wala msimtie kasirani, maana hatawasamehe makosa yenu, kwa kuwa jina langu limo ndani yake.

22. “Lakini ukiisikiza sauti yake kweli na kuyatenda yote ninenayo mimi ndipo mimi nitakuwa ni adui wa adui zako mtesi wa hao wakutesao.

Chunguza mstari wa 21; *Jina langu limo ndani yake*; una tukumbusha kwamba ‘Jina’ linataja kwa pamoja asili na utendaji. Wababa wa kiroho wanaakisi ile asili na tabia ya Mungu kwa wana wao wa kiroho. Pia wanafahamu kusudi au matendo ya Mungu kwa wanadamu katika uelewa wa jumla na kipekee jukumu ambalo kwamba wao na wana wao wa kiroho wanapaswa kulitekeleza katika kukamilisha mapenzi ya Mungu.

Chunguza mstari wa 20, majukumu mawili ya malaika /baba wa kiroho ya kuzingatiwa katika hili.

1. Yeye anakuwa mlinzi uwapo njiani.
2. Hukufikisha mahali ambapo Mungu alipaandaa kwa ajili yako.

Chunguza pia mstari wa 22, namna Mungu anavyosawazisha sauti yake (“Tenda yote ninayosema”) na sauti ya baba wa kiroho (“Tii sauti yake”) . Wanadamu ambao ndio baba wa kiroho wanaweza kwa usahihi kuwakilisha sauti ya Baba wa Mbinguni kwa wana wao wa kiroho. Utii kwa sauti , ni wa muhimu, na unawataka wana wa kiroho kuwaheshimu baba zao wa kiroho, siyo kwa sababu ya ubinadamu wao, lakini ni kutilia mkazo/umuhimu ule uwakilishi wa Kristo ndani ya baba zao wa kiroho. Roho ya mpinga Kristo itaendelea kupambana na ukweli huu, na hivyo matokeo yake yatakuwa ni kuenea sana hali ya kutoitii sauti ya Mungu.

Kumpokea Kristo kunakustahilisha kuwa mwana wa Mungu halali, kwa maana kwamba u mali Yake na wa ufalme Wake. Mchakato huu unaanzia pale ulipoamua kumkubali Kristo awe Bwana na Mwokozi wako.

Yohana 1: 12-13- *Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake waliozaliwa si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.*

Ili kuweza kukua na kukomaa kama mwana wa Mungu, kunapaswa kuwepo na mapokezi endelevu ya Kristo kupitia mapokezi ya Neno lake, linalowasilishwa kupitia kwa baba wa kweli wa kiroho.

Yohana 13:20 *Amin, Amin nawaambieni , Yeye ampokeaye matu yeyote nimpelekaye anipokea mimi, naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka.*

Makanisa katika mkoa wa Galatia yalimpokea Paulo, baba yao wa kiroho kama Kristo Mwenyewe.

Wagalatia 4:14b - *bali mlinipokea kama malaika wa Mungu kama Kristo Yesu.*

YAHUSU UBABA WA KIROHO

Ni nani unaye husiana naye kama baba wa kiroho na siyo kwa suala la manufaa ya kisiasa. Uamuzi huu ni lazima uwe umeshawishiwa na Roho. Kama alivyo Yeye Roho, anavyoshuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni wana wa Mungu na vivyo hivyo pia, kutakuwepo na kushuhudiwa ndani ya roho yako kuwa ni nani utakayehusiana naye kwa maana ya kupata baba wa kitume. Kuwa baba kunapata nafasi kupitia kuachiliwa kwa NEEMA kupitia NENO LA MUNGU lililo sahihi na lenye kuhusika. Neno hili hukupa ulinzi katika kusafiri kwako na kufika mahali ambapo Mungu alipaandaa kwa ajili yako. Ubaba wa kiroho

kwa uhalisia wake unalenga juu ya kumwendeleza kila mtu afikie kuwa MWANA WA MUNGU aliyekua (komaa); kupitia uendelevu wa kuumbika kwa Kristo ndani katika kule kuachiliwa kwa neema, kupitia Neno la Bwana lililopo hivi sasa.

Baba yako wa kiroho analazimika kwenda na wakati uliopo hivi sasa ikiwa ni pamoja na Neno la Bwana linaloendelea kuja hivi sasa au angalau kuunganika na chanzo cha ubaba wa kitume kilichopo. Hili ni la lazima kwa sababu ikiwa utachungwa na mtu ambaye siyo mjuzi wa unenaji uliopo au msisitizo kumhusu Mungu kupitia Neno lake, unaweza kujikuta wewe mwenyewe katika ufahamu wako, shughuli zako n.k vimepitwa na wakati na havifai tena.

Warumi 10:15- *Tena wahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema.*

Mizuri /zuri= horaios maana yake ni:- ya wakati sahihi au majira sahihi, *ndiyo kusema, (kwa kuhusisha)* kustawi, kuongeza uzuri [kiumbo] -mzuri/zuri.

Neno la Kiyunani ‘**horaios**’ linashirikiana na mojawapo ya istilahi nyingine za Kiyunani kwa ajili ya **muda dhidi ya kairos linalomaanisha wakati unaofaa ambao matukio fulani yaliyoanzishwa na Mungu ni lazima yachukue nafasi yake.**

Kwa hiyo ‘**horaios**’ linabeba kumbukumbu ya kile ambacho ni cha wakati wake au utendaji husika ambao una akisi msisitizo wa Mungu ndani ya kipindi fulani cha wakati.

Wale wabebao habari njema kupitia kulihubiri Neno la Bwana, ni lazima wawe na miguu mizuri. Kama ulivyo ufafanuzi wa neno la Kiyunani ‘**horaios**’ hapo juu linalo ashiria kwamba, neno hili limebeba mawazo matatu.

- Neno *mizuri* linamaanisha **kustawi** :-kwa hiyo ni zalishi, linazalisha matunda ndani ya maisha ya wasikilizaji ikiwa ni mbili katika moja (tendemu) pamoja na kumtarajia Mungu kwa ajili ya majira hayo.
- Neno ni kwa **wakati** na ni Neno husika, Neno la sasa.
- Neno hili ambalo linaleta **msukumo** na **mwendo wa kwenda mbele** (linahusishwa na **miguu**) kuelekea kwenye **makusudi ya Mungu.**

Siyo mtu anakuwa baba yako (anakuchunga) wewe, isipokuwa ni ile neema kupitia Neno la Mungu ndani yake ndiyo inatenda. Utafahamu ni sauti ya nani inayokuhamishia kwenye makusudi yako. Utaitambua ile sauti ambayo inakuongoza katika safari ya kuingia katika ukamilifu wa Kristo katika maisha yako na kukubadilisha ili uingie mahali penye uhusiano na utekelezaji katika makusudi ya Mungu.

USILENGE DOSARI ZA YAKOBO RUHUSU ISRAELI ALIYE NDANI YAKE **KUNENA NA KUWA BABA YAKO.**

Mwanzo 49:1-2

- Yakobo akawaita wanawe, akasema, kusanyikeni, ili niwambie yatakayowapata siku za mwisho.*
- Kusanyikeni, msikie, enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israel, baba yenu.*

Zingatia yaliyomo katika mstari wa 1. Yakobo **anaita** lakini katika mstari wa 2 Israel **ananena Neno**. Jina ‘Yakobo’ lina tupa picha ya ule ukweli kwamba alikuwa **mbadilishaji** na **mwongo**’ Neno Israeli linatupa picha ya **mabadiliko ya asili ya kiroho** kama mtu ambaye alishindana na Mungu, Wanawe wanapaswa kuona zaidi ya historia yake ya asili ya kimwili kwa kutazama

rasilimali ya Ki-Uungu aliyoiwakilisha kama baba wa kiroho. Vivyo hivyo na kwetu sisi. Wababa wa kiroho wanaweza wakawa na dosari nyingi hawakukamilika; lakini bado wana rasilimali ya Ki-Uungu ya neema, ambayo ikiwa itatambuliwa na kutafutwa hadi kupatikana, itaachilia unenaji wa Mungu ulio safi na usio chakachuliwa ambao ni muhimu katika kufunua na kuelekeza wana wao wa kiroho kwenye hatima.

Ile NEEMA ya Mungu iliyomo ndani ya baba wa kiroho ni lazima ITAMBULIWE/IFAHAMIKE na ipatikane. Mwanga wa neema hii hufunika madhaifu ya asili ndani yao na hivyo hatutaharibu kule kupokea neema ya Mungu waliyopewa wao kwa ajili yetu.

Wagalatia 2:9a-*Tena walipokwisha kuijua ile neema niliyopewa.*

Wagalatia 4:14- *Na jaribu lililowapata katika mwili wangu hamkulidharau wala kulikataa bali mlinipokea kama malaika wa Mungu , kama Kristo Yesu.*

SHIKA SANA MANENO YA MUNGU YANAYOACHILIWA KUPITIA BABA YAKO WA KIROHO.

Kuna umuhimu wa kipeo cha juu kwamba mtu aendelee na kwa kurudia rudia mtu kujiweka wazi mwenyewe kwa Neno la Bwana kama linavyoachiliwa kupitia wababa wa kweli wa kiroho wa kitume ambao wameunganika na Neno la Mungu husika na endelevu linalotenda kazi sasa.

Chunguza maelekezo ya Paulo (baba wa kiroho) kwa Timotheo (Mwana wa kiroho)

2Timoteo 1:13- *Rudia kile kiwango cha maneno yenye uzima uliyoyasikia kwangu katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu. (NASB).*

2Timoteo 1:13- *Shika kielelezo cha maneno yenye uzima uliyoyasikia kwangu katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu.*

Kiwango /kielelezo= hupotuposis maana yake ni kama kifani (umbo) kwa ajili ya ufuatishwaji, umbo, fuatisha mtindo.

Muhtasari, mchoro wa haraka, kwa ufupi na ufafanuzi wa kumalizia, mfano, kielelezo.

Timotheo anapaswa kurudia au kushika sana ile ramani ya mistari au mchoro wa haraka wa mafundisho yanayofaa ambayo ameshayapokea kutoka kwa Paulo, baba yake wa kiroho.

Sahihi /yanayofaa =hugiano maana yake ni kutovurugwa, yasiyo na mchanganyiko wa makosa.

Rudia /shika = echo maana yake ni kushikilia mwenyewe, kuwa na umiliki katika ufahamu, kuwa nacho k.v miliki, kamata, kuganda/nata au ng'ang'ania, kuambatana kwa karibu na mtu au kitu.

Sawa sawa na yaliyo kuwemo kwenye mafundisho ya Timotheo, hayakuwa zaidi ya yale ambayo aliyasikia kutoka kwa baba yake wa kiroho. Yaliyo kuwemo katika maneno ya Timotheo yalikuwa na mahusiano na kila kitu kilichofungamana na njia za baba yake wa kiroho, Paulo. Hakunena zaidi ya hicho. Mfano wa maisha ya Paulo ulikuwa wa utendaji

ambao ndani yake Timotheo alinena na kutenda. Wana huwa na fundisho linalo fanana na la baba yao.

1Wakorintho 4:17 - *Kwa sababu hii nime mtuma Timotheo kwenu aliye mwanangu mpendwa mwaminifu katika Bwana atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa.*

Chunguza maelekezo ya Paulo kwa Timoteo katika mistari ifuatayo.

1 Timoteo 1:1-3 (KJV)

- 1. Paulo mtume wa Kristo Yesu, kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na Kristo Yesu tarajia letu.*
- 2. Kwa Timoteo mwanangu hasa katika imani, Neema na iwe kwako na rehema na amani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.*
- 3. Kama vile nilivyokusihika ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine.*

1Timotheo 4:11-*Mambo hayo uyaagize na kuyafundisha (KJV)*

2Timotheo 2:1-2- *Basi wewe mwanangu uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*

Yale mambo ambayo Timotheo alipaswa kuwafundisha watu waaminifu yalipaswa kuwa mambo yale yale ambayo Paulo alimfundisha yeye. Asingeweza kufundisha kitu kingine. Fundisho lake lilibainishwa na kile ambacho alikisikia kutoka kwa Paulo. Wana wa kiroho hupokea na kuwa ambukiza wengine mambo waliyokwisha jufunza kutoka kwa baba yao wa kiroho, ambao kwa usahihi wanamfuata Kristo na kanuni za Neno.

2 Timotheo 3:10-16

- 10. Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu na mwenedo wangu na makusudi yangu na imani na uvumilivu.*
- 11. na upendo, na saburi, tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antokia katika Ikonio na katika Listra, kila namna ya adha niliyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote.*
- 12. Naam na wote wapendao kuishi maisha ya utaua katika Kristo Yesu wataudhiwa.*
- 13. Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendela na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika.*
- 14. Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao.*
- 15. Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu ambayo yaweza kaukushimisha hata upate waokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu.*
- 16. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwadibisha katika haki.*

Ndani ya muktadha wa kuwa mwovu, na kuharibika kwa hali ya mwanadamu na kuongezeka kwa nguvu ya udanganyifu, mwana wa kiroho (Timotheo) anaambiwa AENDELEE na MAFUNDISHO aliyopokea kutoka kwa baba yake wa kiroho (Paulo). Katika mistari ya 10-16,

Paulo anataja sababu kwa Timotheo za kuendeleza yale mambo aliyokwisha jifunza na anashawishika nayo:

1. Watu waovu wataendelea kufanya ubaya zaidi na zaidi hadi katika utamaduni wa kuongezeka kwa uongo (mst 13)
2. Ameshajifunza na akawa AMERIDHIKA na mafundisho ya uhakika (mst 14).
3. Mtu ambaye amejifunza kwake mambo haya, ni wa kuaminika kwa hali ya juu na ni baba yake katika Bwana.
4. Ameshuhudia kwa macho mafundisho ya mfano wa kuigwa katika maisha ya mwalimu wake,(mst 10na 11)
5. Kile alichokwisha jifunza kinaendelea kuwa sambamba na ukuu wa maandiko matakatifu ambayo anayajua tangu utoto wake na ufahamu huu unaongoza hadi kwenye hekima nakupata wokovu. (mst 15)
6. Maandiko yote YAMEVUVIWA – ni pumzi ya Mungu (mst 16)
7. Kuendelea na fundisho au andiko ambalo amekwisha sikia, kwa haraka linakuwa na faida zenye nguvu na linafaa kwa :
 - a. Mafundisho
 - b. Kuonya
 - c. Kuongoza
 - d. Kuadhibisha katika haki (mst. 16)

1Wakor. 11:1-*Mnifuuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.*

1Wakor. 11:2-*Basi nawasifu kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea.*

2Watesalonike 2:15-*Basi , ndugu, simameni imara mkayashike mapokeo mliyofundishwa ama kwa maneno ama kwa waraka wetu.*

2Watesalonike 3:6-*Ndugu twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu.*

Paulo alikuwa ni mwenye shukrani kwa ukweli kwamba Warumi walifanyika kuwa WAAMINIFU kwa ile aina ya fundisho mahsusi ambalo YEYE, PAULO ALILIPELEKA KWAO. Sisi pia tunalazimika kubaki waaminifu kwa aina au mtindo wa fundisho ambalo tunapokea kutoka kwa wababa wa kiroho halali, ambao wanaunena ukweli uliopo sasa katika roho ya maandiko, kama wanavyomsikia Baba akinena.

Warumi 6:17 - *Lakini Mungu na ashukuruwe kwa maana mlikuwa wataumwa wa dhambi lakini mlitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*

Yohana 12:49 *Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu, bali Baba aliyenipeleka yeye mwenyewe ameniagiza nitakayo nenana nitakayosema.*

KAA KATIKA ‘NYUMBA’ NA LIRUHUSU NENO LIPATE NAFASI AU LIENDELEE NDANI YAKO .

Yohana 8:28-31.

28. *Basi Yesu akawaambia , Mtakapokuwa mmekwisha kumwinua Mwana wa Adamu, ndipo nitakapo fahamu ya kuwa mimi ndiye na ya kuwa sifanyi neno kwa nafsi yangu ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo.*
29. *Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha peke yangu, kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo.*
30. *. Naye alipokuwa akisema hayo, wengi walimwamaini*
31. *Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini , Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.*

Mstari wa 31:-Kudumu katika Neno la Mungu, ndiko kunako kuhalalisha wewe kuwa mwanafunzi wa Kristo.

Kuendelea lina maanisha:- kubaki au kukaa, kuwa na hali ya kudumu.

Kuendelea katika Neno ni kulitii Neno.

Yohana 8:32-Tena mtaifahamu kweli , nayo kweli itawaweka huru.

Mst wa 32- Ufahamu wa kweli huleta uhuru mbali na dhambi ambao ndio unaokufanya uondoke na kwenda katika njia sahihi za Mungu. Mpangilio wa mambo katika hili ni

- a. Endelea katika Neno
- b. Ijue kweli
- c. kweli itakuweka huru.

Uhuru mbali na dhambi unakuja kutokana na kuufahamu ukweli kwa sababu mtu anaendelea kukaa humo. Kuendelea katika Neno kunahusisha utii. Hata hivyo utii kwa ukweli kufichua ule ukweli ambao ni mtu mmoja tu mwenye ufahamu wa kweli wa ukweli ambao unamweka mtu huru.

Yohana 8:33:36

33. *Wakamjibu, sisi tu uzao wake Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wowote, nawe wasemaje, mtawekwa huru?*
34. *Yesu akajibu Amin amin nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.*
35. *Wala mtumwa hakai nyumbani siku zote, Mwana hukaa siku zote.*
36. *Basi Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli.*

Kukubali na kujitoa kutenda dhambi, kunakufanya wewe uwe mtumwa wake na inafanyika kuwa bwana wako. Unahitaji uhuru utokane na hiyo. Yesu anaendelea kufafanua jambo hili kama kujiweka katika hali ya utumwa kiashiria cha mtu ambaye ni mtumwa wa dhambi.

Tofauti na hili, Ametoa tena nafasi ya Mwana akimaanisha kwamba mwana siyo mhusika wa kuwa mtawala wa dhambi juu ya maisha yake, lakini katika uwana kuna uhuru mbali na dhambi yote. Haya yanatokeaje? Jibu rahisi ni kuwa “kaa ndani ya nyumba milele” Mtumwa hakai ndani ya nyumba milele, lakini mwana anakaa. Nyumba ina maana kaya ya watu wenye imani, chini ya usimamizi wa ubaba wa kiroho, mahali ambapo ndani yake, neema

inasambazawa kupitia kule kuachiliwa kwa neno la Mungu. Kukaa ndani ya nyumba inamaanisha mtu kujiweka katika nafasi na kuwa na msimamo katika kulisikia Neno la Bwana kupitia baba na kuchukua hatua ya utii. Mtumwa huondoka nyumbani akiwa hajakomaa (siyo lazima iwe kimwili inaweza kuwa kwa ndani) na anaendelea kusumbuliwa kwa kukosa uwezo wa kuishinda dhambi.

37. *Najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu lakini mnatafuta kuniua kwa sababu neno langu halimo ndani yenu.*
38. *Niliyoyaona kwa Baba ndiyo niyanenayo, nanyi vivyo hivyo mliyoyasikia kwa baba yenu ndiyo myatendayo.*
39. *Wakajibu wamwambia , Baba yetu ndiye Ibrahimu !Yesu akawaambia, kama mngekuwa watoto wa Ibrahimu, mngezitenda kazi zake Ibrahimu.*
40. *Lakini sasa mnatafuta kuniua mimi, mtu ambaye nimewaambia iliyo kweli, niliyoisikia kwa Mungu. Ibrahimu hakufanya hivyo.*
41. *Ninyi mnazitenda kazi za baba yenu. Ndipo walipomwambia sisi hatukuzaliwa kwa zinaa, sisi tunaye Baba mmoja yaani Mungu.*
42. *Yesu akawaambia, kama Mungu angekuwa baba yenu mngenipenda mimi, kwa maana nalitoka kwa Mungu nami nimekuja, wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma.*
43. *Mbona hamyafahamu hayo niyasemayo? Ni kwa sababu ninyi hamwezi kulisikia neno langu.*
44. *Ninyi ni wa baba, yenu Ibilisi, na tama za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni mwongo , na baba wa huo.*
45. *. Nami kwa sababu nasema iliyo kweli , hamnisadiki.*
46. *Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi? Nami nikisema kweli mbona ninyi hamnisadiki?*
47. *Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu, hivyo ninyi hamsikii kwa sababu ninyi si wa Mungu.*

Mstari wa 37.

Madai ya kuwa wazao wa Ibrahimu yangehalalishwa kwa kutenda matendo ya Ibrahimu, ambayo ni pamoja na kumkubali Yesu na maneno Yake. Madai yao ya kuwa wana kwa Ibrahimu ni batili, kwa sababu wao wanalikataa Neno la kweli lililoletwa kupitia Yesu.

Yesu aliendelea kutetea kwa dhati kwamba wao siyo wa Mungu kwa kuwa Mungu hawezi kuwa baba yao na kwa sababu hiyo, hawana uwezo wa kulisikia Neno lake. Kule kushindwa kulisikia Neno Lake, basi, kusinge wawezesha kuliruhusu Neno kupata nafasi wala kuendelea mbele ndani yao. Hili ni la kina zaidi kuliko kukanusha ile hoja kwamba wao ni wazao wa Ibrahimu. Sasa wao hata si wazao wa Mungu. Toa ushahidi kwamba wewe kwa kweli ni wa Bwana kwa kule kumkubali mtu yule ambaye anakuletea NENO LA KWELI. Mpokee kama ni mtu anayekufaa na tilia maanani lile Neno na hivyo uta kuwa una udhihirisha ule ukweli kwamba, Mungu ni Baba yako.

Yohana 8:37- *Najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu, lakini mnatafuta kuniua kwa sababu neno langu halimo ndani yenu.*

Katika Kiyunani cha asili, “kifungu hiki, *neni langu halimo ndani yenu*” kwa kawaida husomeka, kama ifuatavyo:- *Neno langu halikupata maendeleo ndani yenu*”

Mahali = choreo maana yake ni kupita, ingia, kushikilia, kukaribisha, kuandaa chumba, toa mahali, toa, kwenda mbele, songa, endelea, fanikiwa, kuwa na nafasi au chumba kwa ajili ya kupokelea au kuhifadhi kitu fulani.

Yesu anasikitika kwa ukweli kwamba ingawa wasikilizaji Wake wangeweza kufuatiliwa asili yao kimwili hadi kwa Ibrahimu ambaye ndiye babu yao, bado tabia zao zilikuwa mbali na uhalisia ule. Walitafuta kumuua. Tendo hili halikukusudiwa kwa ajili ya kuendelea kushikilia madai yao ya kuwa uzao wa Ibrahimu. Yesu alitathimini makosa yao yasiyokubalika na kusudio ovu la kupanga kumuua YEYE kama ndiyo sababu ya kimwili ya jambo muhimu, dhidi ya Neno la Mungu ambalo halikuwa na nafasi ndani yao au hata lile Neno ambalo Yeye Yesu aliliachilia halikuwa na mahali pa kukaa ndani yao kama inavyooneshwa hapo juu. Neno la Kiyunani linalotafsiri neno **mahali** linaonesha kwamba, lile Neno halikuingia ndani yao. Halikuruhusiwa liingie, ndani yao. Hawakuweza kulishikilia lile Neno.

Yote haya kimsingi, yalikuwa ni matokeo ya ukweli kwamba, hawakuweza kuifananisha kwa usahihi sura ya Kristo kama ndiye Mungu Mwana na matokeo yake hawakulipa kipaumbele wala nafasi lile Neno alilosema. Kulikuwa hakuna nafasi ndani ya mioyo yao kwa ajili ya Neno la Mungu kwa sababu, kulikuwa hakuna kutathimini kwa kweli na hata kumpokea Yule mtu ambaye alinena Neno kwao.

Muhimu zaidi, hasa kama kuyaheshimu maneno:-*neno langu HALINA NAFASI ndani yenu* inamaanisha kwamba lile Neno la Mungu *halikuleta maendeleo au halikutenda kazi ndani yao.*

Vitu vingi vinalisonga Neno la Mungu kutokana na maisha yetu. Ni kweli, kuna vitu vingi ambavyo vinalisonga sana Neno la Mungu ili litoke katika mioyo yetu. Tunahitaji kulienzi Neno kwa hali ya juu na kulipa kibali sahihi na uthamani katika maisha yetu. Cha muhimu zaidi tunahitaji kuliruhusu Neno lifanye kazi sahihi ndani yetu.

Kwa kuliruhusu Neno lipate mahali sahihi na kuendelea ndani yetu, kutatuhakikishia kwamba, hatustawishi fahamu na tabia ambazo ni pinzani kwa Mungu na makusudi Yake. Watu wali tafuta kumuua Yesu, sisi pia tunaweza kuwaua wajumbe wa Mungu na ujumbe wenyewe, ikiwa hatutakuwa waangalifu.

Shikilia aina hiyo ya mafundisho unayopokea kutoka kwa wababa wa kiroho wa kweli. Tembea ndani yake. Tii na yakumbatie. Liruhusu listawishe asili ya Kristo kikamilifu ndani yako. Fundisha mtindo huu au aina hii ya fundisho kwa wengine. Kwa pamoja, kupitia mtindo wako wa maisha au tabia yako pamoja na kuelekeza kwa kinywa chako.

Waebrania 13:7-*Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza waliowaambia Neno la Mungu, tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao.*

Ipe uthamni SAUTI YA Bwana unayoisikia. (Soma Zab 119:11, Zab 37:31, Zab 40:8, Luk 2:29 na 5).

**MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA
KIKUNDI.**

1. Mojawapo ya njia muhimu ambazo kwa hizo Neno la Mungu linakuja ni kupitia sauti ya mtu hasa sauti ya baba wa kiroho wa mtu katika Bwana. Halalisha maelezo haya kwa maandiko ya Bibilia.
2. Jadili uzito wa kuwa na baba wa kiroho mhusika ambaye anawasilisha kwako Neno lililopo sasa, endelevu na halali na siyo kitu cha kale au kisichofaa kwa sasa.
3. Ni lazima mtu ajishike kwenye mtindo, kiwango/muundo/ kigezo / mwongozo/mchoro rahisi wa fundisho kamili (linalofaa) linaloletwa kwake na baba yake wa kiroho katika Bwana. Wewe unaelewa nini kwa hili na ni nini baadhi ya mambo unayoweza kuyahusisha na hili?
4. Katika Yohana 8 mna kanuni ambazo kwa hizo uwana wa kweli unathibitshwa au kuhalalishwa. Zipi ni baadhi ya kanuni hizi ?

NENO LA MUNGU KATIKA NYUMBA YA MUNGU – SEHEMU YA KWANZA.

Lengo: Nyumba ya Mungu- Familia ya Mungu hulipa kipaumbele Neno la Mungu.

Ni jambo la muhimu kwamba mada ya 7 imeeleweka vizuri kabla hujaendelea na mada hii. Kanisa la Mungu ndilo familia ya Mungu na linatajwa kama “mlima wa nyumba ya Bwana ambayo itaimarishwa kama ndio mkuu wa milima yote ya dunia.

ANDIKO LA MSINGI:

MIKA 4:1-3

1. Lakini itakuwa katika siku za mwisho ya kwamba mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima, na watu wa mataifa watauendea makundi makundi.
2. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njooi, twende juu mlimani kwa Bwana, na nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake, kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na Neno la Bwana litatoka Yerusalemu.
3. Naye atafanya hukumu kati ya watu wa kabila nyingi, naye atawakemea mataifa wenye nguvu walio mbali, nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu, taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe.

‘Sayuni ‘hapa ni rejea ya kanisa (hasa – lililokomaa, kanisa kamilifu)

Waebrania 12:22-23-Bali ninyi mmeufikia milima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkuatano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika,

UFALME WA MUNGU NA KANISA LA MUNGU.

Ufalme wa Mungu na kanisa la Mungu ni dhana mbili tofauti. Ufalme ni pamoja na Kanisa lakini pia vinaunganisha kule kuwepo kwa wanadamu wote, maelezo mbalimbali ya maisha na mpangilio wote wa uumbaji. Ufalme wa Mungu umeenea kote na juu ya viumbe vya Mungu na mapenzi juu ya kila usemi katika maisha na sekta au milki juu ya sayari ya dunia na uumbaji wote wa uumbaji wa kimbingu. Kanisa la Mungu ndilo wakala wake na kwa kupitia hilo Ufalme wa Mungu unapokelewa, unaunganishwa na kuelezewa. Ufalme wa Mungu una nguvu za ajabu za kujieleza na kujieneza kupitia kanisa. Ili liwe na uwezo na utoshelevu wa kuelezea Ufalme wa Mungu, kanisa linahitaji kupangiliwa kwa usahihi, siyo kikatiba kama vile taasisi fulani halali, ila kimahusiano kama kiumbe hai.

NYUMBA YA MUNGU NI FAMILIA YA MUNGU

Mara kwa mara kanisa linaonekana kama ni nyumba ya Mungu.

1Timoteo 3:15- Lakini nikikawia upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli.

Wagalatia 6:10- *Kwa hiyo kadiri tuapatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, na hasa jamaa ya waaminio.*

1Petro 2:5- *Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa muwe nyumba ya Roho , ukuhani mtakatifu mtoe dhabihu za roho zinazokubaliwa na Mungu , kwa njia ya Yesu Kristo.*

Waefeso 2:19-22- *Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu, Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaunganishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya MUNGU KATIKA Roho.*

Waebrania 3:1-6

- 1. Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu Yesu.*
- 2. Aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyeniweka, kama Musa naye alivyokuwa, katika nyumba yote ya Mungu.*
- 3. Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba.*
- 4. Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu, ila yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu.*
- 5. Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu Kama mtumishi awe ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye.*
- 6. Bali Kristo, kama mwana juu ya nyumba ya Mungu, ambaye nyumba yake ni sisi kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.*

Matayo 16:18- *Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu, wala milango ya kuzima haitalishinda.*

Neno la **Kiebrania** kwa ajili ya neno **nyumba** ni **bayithi** na la **Kiyunani** ni **oikos**.

Bayith ni **nyumba**- katika mabadiliko makubwa ya matumizi hasa familia (Tafsiri ya strong)

Oikos ni **makazi**- Kwa kuhusisha ni familia (Tafsiri ya strong).

Kama wakati ambapo **bayith** na **oikos** zaweza kutaja mahali pa kuishi pa kimwili peke yake. Lakini mara nyingi sana yanagusia **uthamani** au **utaratibu** wa **mahusiano** ambao upo katika nyumba. Nyumba hai fafanuliwi kwa kutumia muundo wa kawaida wa umbo, lakini ni kwa kueleza tabia kwa kutumia kiwango cha uthamani wa mahusiano yaliyomo ndani yake. **Bayith** linatokana na istilahi ya Kiebrania yenye kumaanisha ‘**jenga**’ yaani ‘**banah**’. Neno jingine linalotokana na **banah** ni neno la Kiebrania ‘**ben**’ ambalo linamaanisha **mwana**. Beni linamaanisha ‘**mtu**’ yaani mwana ambaye ana mzigo wa kulijenga jina la familia. Hivyo bayith ni nyumba ya Bwana iliyojaa wana ambao wana mtazamo wa kujenga jina (asili na utendaji au mapenzi) ya Mungu ndani na kwa kupitia familia ya Mungu. Ule uwepo wa wana unamaanisha kuwepo kwa kanuni ya ‘**ubaba**’

Zaburi ya 127:1a- *Bwana asipoijenga (banah) nyumba waijengao wafanya kazi bure.*

Nyumba ya Mungu imejawa na wana. Huwezi ukawa na wana bila ya kuwa na kanuni ya baba aliye mkazi na mtendaji. Nyumba ya Mungu ina wababa wa kiroho na wana wa kiroho. Hili lina shauri kuwepo na kanuni ya familia na kuanzia hapo tunakuwa na familia ya Mungu. Neno la Kiyunani la familia ni '**patria**' linalotokana na neno jingine la Kiyunani kwa ajili ya 'baba' yaani '**pater**'. Huwezi ukawa na familia au wana bila ya 'baba'.

Waefeso 3:14-15-*Kwa hiyo nampigia Baba, magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa.*

Kuna maneno mengine yanayoelezea kanisa katika Neno la Mungu (Bibilia) kama vile maneno, **mji, bwana harusi, mlima** n.k. Yote haya yana viashiria vya msingi, maumbo na tabia ambazo zinatusaidia sisi kufafanua kanisa ni nini leo. Wakati kuna maneno mengi yanayohusu kanisa katika Neno la Mungu. Kanisa kama familia, siyo kiwakilishi ila kimsingi inaonesha ni kwa namna gani kwa uhalisia, kanisa linapaswa kuwepo. Huku kulielewa kanisa kama familia ya Mungu kuna maana muhimu katika muundo na utendaji wake wenye tija kama ndio mwili wa Kristo hapa duniani.

Kanisa ni viungo vingi vya MWILI WA KRISTO. Ndio sura yote ya ukuu wa Mungu hapa duniani katika muundo na utendaji. Ni mwili wa Kristo, siyo mwili wa mtu mwingine yeyote. Mwili wa Kristo ndicho chombo ambacho kwa hicho, Kristo ambaye ndiye **kichwa**, anapata uhalali wa kujulikana na kutenda duniani. Mwili wa Kristo unapaswa uangaze yale yote ambayo yanawasilishwa na Kristo. Kristo ndiyo kanuni inayopaswa kueleweka ingawa ina utata. Kama sisi ndiyo mwili wa Kristo tunahitaji kuelewa kikamilifu Kristo ni nani. Uelewa wetu kuhusu **Kristolojia** kutavuta na kurekebisha ule uelewa wetu kuhusu "**Eklesiolojia**". Mara nyingi tunapoangalia muonekano wa kanisa kwa madai kuwa ni mwili wa Kristo, bado ni mara chache sana tunauona mng'ao wa kanisa kwa madai kuwa ni mwili wa Kristo na bado haliakisi ile asili na mapenzi ya Kristo, ambaye ndiye kichwa cha kanisa.

Kristo anaunganisha utatu wote, yaani Baba, Mwana na Roho. Uungu wote umeshikamana na ni mmoja.

Wakolosai 2:8,9 - *Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu wala si kwa jinsi ya Kristo. Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili.*

Uungu = theotes maana yake ni **Umungu** (hali ya kuwa Mungu, Uungu)

Mungu ni roho- ndivyo maandiko yanavyofundisha.

Yohana 4:24- *Mungu ni Roho , nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*

Ujumla wote wa Mungu ni Roho. Baba ni Roho, Mwana ni Roho, Roho Mtakatifu ni Roho. Mungu ni mmoja- Yeye ni Mungu mmoja anayejidhihirisha katika nafsi tatu tofauti ambazo zote ni Roho. Nguvu za Baba na Mwana ndani ya uungu wa Mungu hutuonesha sura ya kimahusiano ya Mungu. Baba na Mwana hutupa picha ya kanuni ya familia. Roho Mtakatifu ndiye msimamizi au ndiye asili au wakala, ndani ya Uungu wa Mungu ambaye anafanya vijenzi

vya kimahusiano viwezekane kueleweka kwa wanadamu. Mfumo huu unaoneshwa bayana katika maelezo ya kitabu cha Mwanzo, mahali ambapo Roho alijongea juu ya uso wa dunia ili kuelezea na kuweka bayana mchakato wa uumbaji. Roho Mtakatifu anaishirikisha dunia akiwawezesha wanadamu ili waingie katika kuwa wana na hivyo kuhusiana na Mungu kama ndiye **Baba** yao.

Hivyo tunaweza kuhitimisha kwamba kanuni ya Kristo ndani ya nguvu ya kimahusiano inashikamana na Baba na vijenzi vya Uungu vya Mungu.

2 Yohana 1:6-9

6. *Na huu ndio upendo; tuenende kwa kuzifuata amri zake. Hii ndiyo ile amri kama mlivyosikia tangu mwanzo kwamba mwenende katika hiyo.*
7. *Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani wasiokiri ya kuwa Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye Yule mdanganyifu na mpinga Kristo*
8. *Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyoyatenda bali mpokee thawabu timilifu.*
9. *Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*

Hivyo kanuni au fundisho la Kristo ni fundisho la Baba na Mwana. Kitu chochote kinachohusiana na Kristo ni lazima kiwe na kiini Chake, yaani, zile kanuni tendaji za ubaba na uwana. Ubaba na uwana havitaweza kujulikana tofauti na Roho Mtakatifu.

Kanuni ya Kristo ndani ya muktadha wa dunia inajieleza kwa kupitia kanuni ya Uwana. Uwana katika mwili wa Kristo huleta tabia yakinifu ili uweze kutenda kazi kufuatana na muktadha ulioko duniani. Lakini Uwana unahitaji ubaba. Hivyo kiriba cha baba- mwana cha kiroho ndio uwezo makini unaopaswa kuenea katika nyumba ya Mungu. Istilahi hizi **baba** na **mwana** zimeshikamanishwa ndani ya uundaji halisi wa uungu wa Mungu mwenyewe, na pia, una uhusiano wa hali ya juu unaogusia kanisa la Mungu kama familia ya Mungu.

Neema ya Mungu inapata ukamilifu wake na wingi wa wepesi wa kububujika kwake ndani ya muktadha huu. Mwili wa Kristo kama mwana mshirika wa Mungu hapa duniani, na kama vile Yesu aliye Mwana wa kuigwa, unalazimika kujawa na neema na kweli. Neema inagawiwa kwa urahisi zaidi ndani ya muktadha wa hali ya juu wa kimahusiano. Kanisa kama ndilo familia ya Mungu, mahali ambapo wababa wa kiroho wanawakilisha na kugawa neema ya Baba wa Mbingu kwa wana wao wa kiroho, linafanyika familia ya Mungu duniani, likifuata mfano wa Kristo, aliye ukamilifu wa utatu wa Mungu.

Neema ya Mungu hupitia kwa wababa wa kiroho na kwenda kwa wana wao kupitia msingi wa Neno la Mungu linalonenwa. Kama hakuna Neno la sasa lililo sahihi ‘ Nyumba ya Bwana, familia ya Mungu, kamwe haitainuka na kuingia mahali pa kumiliki na kutawala kitabia sawa na Ufalme wa Mungu.

Kanisa ambalo ndilo mwili wake

Waefeso 1:22-23-Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.

Kanisa siyo mwili wa Yesu, Kanisa ni mwili wa Kristo. Kanisa ndilo linalomkamilisha YEYE. Ndilo ukamilifu WAKE. Yuko wapi hivi sasa? Yuko ndani ya mwili Wake. Hujigawa Yeye mwenyewe kutoka ndani ya Mwili wake. Mwili huu umetajwa tu katika barua za Mtume Paulo. Jina pekee ambalo halikutajwa katika Agano la Kale ni lile kwamba, kanisa ni mwili wa Kristo. Siri hii haikuwa imefichwa katika maandiko ya Agano la Kale, lakini ilikuwa imefichwa ndani ya Mungu mwenyewe, soma Waefeso 3:9.

Wakolosai 1:25-27

25. *ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawa sawa na uwakili wa Mungu niliopewa kwa faida yenu, nilitimiza Neno la Mungu*
26. *Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake.*
27. *Ambao, Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yetu tumaini la utukufu.*

Kristo ndani YAKO ni tumaini la utukufu. Neno YAKO hapa kwa Kiyunani lina maanisha wingi – Kristo ndani YENU NYOTE MLIO KATIKA MWILI WA KRISTO ndiye tumaini la utukufu. Itauchukua mwili wote wa Kristo katika kila sekta ya viungo vingi vya mwili kiulimwengu ili kuakisi YOTE YALIYO YA KRISTO.

NENO LA MUNGU NDANI YA NYUMBA YA MUNGU

Zakaria 8:3 *Bwana asema hivi, Mimi nimerudi Sayuni, nami nitakaa katikati ya Yerusalemu, na Yerusalemu utaitwa Mji wa kweli, na mlima wa Bwana wa majeshi utaitwa mlima mtakatifu.*

Sayuni ule mlima wa nyumba ya Bwana, Mji wa kweli. Neno la Mungu ni kweli. Neno mji linamaanisha maisha ya jumua na yaliyopangiliwa na yakutegemeana kuhusu masuala ya kibinadamu. Neno la Mungu linawaleta watu wa Mungu katika kuwa wamoja na wenye uhusiano katika mtindo wenye utaratibu. Hilo hutokea kwa ushindi ikiwa kila mtu atakuwa anaogozwa kwa hilo na kuwa watiifu kwa Neno la Mungu linalowajia. Neno la Mungu ni lazima lipewe kipaumbele katika nyumba ya Mungu. Ni lazima liwe kamili, ndiyo kiini cha ukamilifu wote wa kujulikana/kuenea ndani ya Nyumba' kanisa ndilo nguzo na mhimili wa UKWELI. 1Tim 3:15.

Milima inaonesha maeneo maalumu au mazingira ya jamii za kiulimwengu kwa mfano, serikali, elimu, siasa, matibabu, madawa, sanaa, burudani n.k.

Unabii hapa unaashiria kwamba mlima wa nyumba ya Bwana utaimarishwa kama ndiyo mkuu wa milima yote katika mataifa ya dunia. Kwa uhalisia soma katika Kiebrania cha asili.

Inasomeka kama ifuatavyo;

“Ule mlima wa nyumba ya Bwana utajengwa juu uwe mlima mkuu kuliko yote. (NASB ufafanuzi wa pembeni) kwamba mlima wa nyumba ya Bwana hautakuwa tu ni mrefu kuliko yote au ndio unaotawala lakini pia ndio utakaokuwa msingi wa kuenea kwa ushawishi wote juu ya kila mkakati wa kissekta wa kimaisha ulimwenguni mwote. Ndani ya nyumba na kwa kupitia nyumba ya Bwana ufalme Wake, mamlaka na utawala utaangaza katika mataifa yote. Ufalme unafananishwa na chachu (hamira) inavyoenea kwa haraka.

Luka 13:20-21 (NIV)

20. *Akasema mara ya pili, niufafanisha na nini Ufalme wa Mungu?*

21. *Umefanana na chachu aliyotwaa mwanamke akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachacha wote pia.*

Chachu au hamira ni alama ya vitu vingi, ikiwa ni pamoja na KANUNI au funzo.

Ni kitu gani kinaufanya mlima wa nyumba ya Bwana uwe mkuu kushinda mingine hapa duniani? Una kitu gani ambacho maumbo mengine hayana? Jibu ni SHERIA au NENO LA BWANA.

Mika 4:26”*Kwa maana katika Sayuni itatoka sheria na neno la Bwana litatoka Yerusalemu*”

Sheria (torati) ni *maadili au kanuni*.

Zaburi 110:2- *Bwana atainyosha toka Sayuni Fimbo ya nguvu zake . Uwe na enzi kati ya adui zako*

Kutoka Sayuni, Mlima wa Nyumba ya Bwana, sheria itatoka katika Neno la Mungu na neno hili linawakilisha fimbo yenye nguvu ya Bwana.

Fimbo=matteh/mattah maana yake ni **fimbo, tawi, kabila**.

Neno *fimbo* pia linagusa *kabila* au *watu* -fimbo yenye nguvu katika Sayuni inaweza kurejea pia kama familia halisi ya Mungu inayoundwa na wababa na wana kiroho. Sheria ya Mungu inapata nafasi kupitia kanisa kama familia ya Mungu. Jeshi la kanisa na nguvu ya serikali yake vinatumika na kujitambulisha kupitia asili yake kama familia . Katika uwekezaji huu wa wababa na wana wa kiroho, Neno la Bwana linakwenda mbele kwa kadri ya nguvu ya uweza wa Mungu inavyo liwezesha kanisa ambalo ni familia Yake kutawala katikati ya adui zake.

Huwezi kutawala katikati ya adui zako (Zab 110:2) mpaka pale utakapokuwa umejifunza kula katika meza uliyo andaliwa katika uwepo wa maadui zako Zaburi 23:5 (Thamo Naidoo)

Adui zako ni:

1. Shetani
2. Ulimwengu
3. Mwili

1Yohana 2:15-17

Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani yaani tamaa ya mwili na tamaa ya macho na kiburi cha uzima havitokani na Baba , bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita pamoja na tamaa zake , bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.

Zaburi 23:1-6

1. *Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu.*
2. *Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza.*
3. *Hunihuisa nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.*
4. *Naam, nijapopita kati ya uvuli wa bonde la mauti, Sitaogopa mabaya;Kwa maana Wewe upo pamoja name, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji*

5. *Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika.*
6. *Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.*

Mstari wa 1- Mungu huwachunga watu wake kwa kuwaweka wachungaji wanadamu wa hapa duniani kuwa wawakilishi Wake.

Yeremia 3:15-19

15. *nami nitawapa ninyi wachungaji wanipendezao moyo wangu watakao walisha kwa maaarifa na fahamu.*
16. *Kisha itakuwa mtakapoongezeka na kuwa wengi katika nchi hiyo asema Bwana, siku zile hawatasema tena, sanduku la agano la Bwana, wala halitaingia moyoni. wala hawatalikumbuka, wala hawatalizuru, wala hayatafanyika hayo tena.*
17. *Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha Bwana na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu kwa ajili ya jina la Bwana, wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya.*
18. *Siku zile nyumba ya Yuda watakwenda pamoja na nyumba ya Israel, nao watakuja pamoja kutoka nchi ya kaskazini mpaka nchi ile niliyowapa baba zenu iwe urithi wao.*
19. *Lakini mimi nalisema, Nitawezaje kukuweka pamoja na watoto na kukupa nchi ipendezayo, urithi ulio mwema na mataifa? Nami nikasema Mtamwita, Baba yangu, wala hamtageuka na kuacha kunifuata.*

Zingatia kwa kina maana ya kiroho na mahusiano ya sehemu za maandiko zilizotiwa kivuli hapo juu.

Yeremia 23:3-4

Nami nitakusanya mabaki ya kundi langu katika nchi zile zote nilizowafukuza, nami nitawaleta tena mazizini mwao, nao watazaa na kuongezeka. Nami nitaweka juu yao wachungaji watakao walisha, wala hawataona hofu tena wala kufadhaika wala hatapotea hata mmoja wao asema Bwana.

Mstari wa 2

Hawa ni wababa wa kiroho ambao wanalitunza kundi la Mungu kwa kuliongoza katika malisho ya majani mabichi, kwa kuwalisha mlo au chakula cha kufaa na kamili cha kiroho kutoka Neno la Mungu.

Mstari wa 3a”**Hunihuisha nafsi yangu**”

Mungu Baba wa mbinguni ndiye Baba wa roho yako.

Waebrania 12: 9-*Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi nasi tukawastahi, basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi?*

Wababa wa kiroho wa duniani huchunga nafsi yako (Waebrani 13:7,17) wakiwa na kusudi la kuirudisha katika nafasi yake ya awali ndani ya Kristo. Nafsi ni pamoja na akili ya [nini na namna unavyofikiri] utashi wako [namna unavyochagua na kufanya maamuzi] hisia (namna unavyohisi)

Waebrania 13:17- *Watii wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zetu kama watu watakaotoa hesabu ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua. Maana isingewafaa ninyi.*

Waebrania 13:7 *Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena kwa kuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao.*

Angalizo : Unaongozwa kwa NENO LA MUNGU linalonenwa kwako. Neno la MUNGU linalonenwa na baba yako wa kiroho lina chungu nafsi yako katika nyumba ya Mungu. Kwa kukulisha Neno la Mungu, nafsi yako inafanywa kuwa mpya na inanyooshwa ili iweze “kufikiri, kuamini na kuhisi kufuatana na njia za awali alizoziumba Mungu, na hivyo mtindo wa kufikiri kwako na nafsi yako vitakuwa vimepatanishwa na roho iliyofanywa upya ikichungwa na Baba wa mbinguni.

Mstari wa 3b *na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.*

Kwa namna hii, sura ya Mungu ndani ya mwana wa Mungu inaongezeka na kukomaa na hivyo mwana anaweza sasa kuenenda katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Mwenendo wa mwana utaakisi jina la Mungu”. Istitahi *jina* inagusia vyote. Asili au utambulisho na utendaji (kusudi au hatima). Hivyo mwana katika tabia, mwenendo na mtindo wake wa maisha vitaonesha tabia ya Mungu. Pia kwa matendo yake duniani, atafuatilia na kutenda mapenzi ya Mungu na hivyo kukamilisha ile hatima ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yake.

Mstari wa 4: *Nijapopita kati ya uvuli wa bonde la mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana wewe upo pamoja nami ; Gongo lako na fimbo yako vya nifariji.*

Mwana wa Mungu aliye jaa Neno anayo kinga dhidi ya athari za mazingira yake ya asili, hasa kuhusu hofu.

Neno la Kiebrania **shebet** lililotafsiriwa *gongo* linahusiana na neno lililotafsiri fimbo (**matteh**) kama lilivyofafanuliwa hapo juu.

Fimbo – Kiebrania ni *mishenah/misheneth* likiwa na maana ya mhimili, riziki au (kwa kuonekana- ni fimbo ya kujikongoja. Linagusia lile neno linalotupa ufafanuzi na haki ya kuenenda kwetu katika Bwana.

Lile gongo na ile fimbo huleta faraja, k.v. kutulizwa na kupata fursa ya kutubu na kurekebisha njia zetu ili ziendane na njia za Mungu.

Mst wa 6. *”Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.*

Ule wema na upendo wa huruma za Mungu unawafuata wana wake siku zote za maisha yao. Mwana hukaa ndani ya nyumba ya Mungu milele. Hivyo muktadha wote wa **Zab. ya 23** unaonekana katika NYUMBA YA MUNGU.

Yohana 8:35 *”Wala mtumwa hakai nyumba siku zote mwana hukaa siku zote.*

Mst wa 5- *Waandaa meza mbele yangu machoni pa watesi wangu umenipaka mafuta kichwani pangu na kikombe changu kinafurika.*

Meza huunganisha: Mezani ndipo mahali ambapo familia inakutana kula chakula. Kwenye nyumba kubwa yenye vyumba vingi, meza hutumika kuunganisha na kuzungushia boma la mshikamano na hivyo hula chakula chao cha kiroho kwa furaha na uaminifu wa moyo.

Mdo 2:42-46

Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume na katika ushirika na katika kuumeza mkate na katika kusali. Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume. Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimeza mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe,

Meza hulisha na kutunza: Chakula ni alama ya mlo wa kiroho yaani Neno la Mungu. Mlo huo upo sawa na kile ulicho kula kwa asili na kwa kiroho. Unapaswa kuwa mnururisho wa aina ya chakula unachokula. [**Zab 100:3c** **Tuwatu wake** na **kondoo wa malisho Yake**] Chakula kutoka meza ya Baba yako kitafunika dosari zako na mapungufu yako. Ulemavu wa Mefiboshethi haukuonekana wakati alipoitwa akae na kula mezani kwa Daudi.

KATIKA NYUMBA YA BABA YAKO, JILISHE ZAIDI KUTOKA MEZA YA BABA YAKO.

Chanzo chako cha msingi cha chakula cha kiroho kinapaswa kuwa ni Neno la Mungu linalohubiriwa na kufundishwa na baba yako wa kiroho katika Bwana. Kumbuka kwamba Timotheo anaambiwa na Paulo asisitize juu yake na asifundishe fundisho jingine, kuliko lile alilopokea kutoka kwa Paulo. Usile katika meza tofauti au maeneo mengine. Wengine wanaweza wakawa na nyongeza na wakaongeza katika ukuaji wako wa kiroho, lakini chanzo kikuu cha mlo wako wa kiroho kinapaswa kuwa Neno kutoka kwa baba yako wa kiroho. (Unaweza ukawa na walimu wengi lakini baba ni mmoja (1Wakor. 4)

Zingatia ule mfano wa Ruthu

Katika kitabu cha Ruthu, Ruthu ni picha ya mwana wa kiroho (Ruth 4:15) Naomi ni baba wa kiroho na Boazi ni uwakilishi wa Kristo na kwa baadhi ya namna nyingine anafananishwa na kuwa baba wa kiroho.

RUTI 2:1-3

- 1. Basi huyo Naomi alikuwa na ndugu ya mumewe mtu mkuu mwenye mali, wa jamaa yake Elimeleki, na jina lake alitwa Boazi.*
- 2. Naye Ruthi Mmoabu akamwambia Naomi, sasa niende kondeni niokote masazo ya masuke nyuma yake Yule ambaye nitaona kibali machoni pake. Akamwambia, haya mwanangu, nenda.*
- 3. Basi akaaenda akaja akaokota masazo kondeni nyuma ya wanangu na bahati yake ikatukia kwamba akifika sehemu ya shamba iliyokuwa mali yake huyo Boazi, ambaye alikuwa wa jamaa yake Elimeleki.*

Naomi alitoa kibali chake kwa shauku ya Ruthu ya kwenda kuokota masazo (chakula) (Ruthu 2:2). Shauku hii ilikuwa imechochewa na msukumo mkali wa yeye kuhusika na ustawi wa Naomi. Ruthu alienda kuokota tu baada ya Naomi kumruhusu kwenda. Wakati anaokota, katika shamba la Boazi alipata kibali kwake. Mst. Wa 3 unadokeza kwamba hili lilikuwa ni bahati alitokea kufika. Lakini hakuna cha kufananishwa na Mungu, Ndani ya mfumo wa baba na mwana. Maamuzi ya kawaida yanafanyika kuwa mipenyo mikuu. Maamuzi ya kubahatisha yanaweza kuchukuliwa na kubadilishwa na kuwa maendeleo ya kimkakati. Kuokota ilikuwa ni shughuli halali iliyokuwa imeruhusiwa na sheria ya Mungu (taz. Walawi 19:10 Walawi 23:22, Kumb 24:19-21) kuokota ilikuwa inahifadhiwa kwa ajili ya mgeni (msafiri), mjane na yatima. Mgeni anafananishwa na wale walio nje ya usajili wa Israeli, nje ya upako unaozidi ujenzi wa kizazi cha mfumo wa baba na mwana. Mjane linamaanisha kumpoteza mume na pia baba. Pia linadokeza kutokuwa na baba. Yatima linadokeza kumhusu mtu mwenye matatizo ya kutotambuliwa, kwamba ni mwanaume au mwanamke asiye kuwa na baba na hivyo ni mtu anayetumika nje ya matunzo na kuwekezewa na wababa. Ruthu alikuwa na yote haya. Alikuwa ni mgeni (Mmoabu) mjane na yatima (lakini yatima ambaye alikuwa anakulia kuwa mwana).

Kimsingi kuokota kunafanyika pembezoni mwa mashamba (Walwi 19:9) Baadhi wako katika mashamba ya baba zao wa kiroho, lakini wanachofanya ni kuokota pembezoni na kamwe hawajafikia kuchukua ukamilifu wa neema iliyotolewa kwao iliyo katikati ya shamba. Kuokota pembezoni mwa shamba kunaweza kulinganishwa na mahudhurio hafifu katika mikutano inayoitishwa na baba wa kiroho, mahali ambapo anahamishia neema kupitia kufundisha Neno la Mungu. Pia inaweza kuchukuliwa kama ni utii nusu nusu au usio tabirika kwa neno linalofundishwa. Tunahitaji tuhame kiroho kutoka pembeni na kuhamia katikati ya shamba.

Ruthi 2:8- *Basi akamwambia Ruthu, Mwanangu, sikiliza, wewe usiende kuokota masazo katika shamba lingine, wala usiondoke hapa lakini ukae papa hapa karibu na wasichana wangu.*

Boazi alimpa maagizo Ruthu asiende kuokota katika shamba jingine. Nafaka za mashambani hutumika kuzalisha mkate, alama ya Neno la Bwana. Usiende kuokota katika shamba JINGINE inagusia kutokula aina tofauti ya misisitizo tofauti ‘Maneno’ katika meza nyingi. Timotheo alipaswa kufundisha siyo fundisho jingine isipokuwa lile alilolisikia kutoka kwa Paulo.

Uokotaji wa Ruth sasa unaondoka kutoka pembezoni mwa shamba na kuokota nyuma ya wavunaji wenyewe. Kuokota chochote watakacho dondoshwa. Ili kuhakiki shughuli hii inaendelea, Boazi alimruhusu Ruthu anywe maji kutoka kwenye magudulia ambayo watumishi walinywea ili kuweza kupata chumvi maji na kumuimarisha. Aliendelea bado, baada ya chakula na kabla miganda haijaja kuchukuliwa na wavunaji (sura yenye nguvu ya alimaye ikamfikia avunaye- Amosi 9:13_)

Ruth 2:9- Macho yako na yaelekee konde wavunalo, ufuatane nao, je! Sikuwaagiza vijana wasikuguse? Tena ukiona kiu, uende kwenye vyombo, nawe uyanywe waliyoyateka hao vijana .

Macho hunena MAONO. Ruthu hakwenda kuokota katika shamba jingine kwa sababu alitambua kwa usahihi na aka tathimini lile shamba na nyumba ya Boazi na akaona ndiyo mahali sahihi ambapo analazimika kuendelea kuokota. Jina ‘Ruthu’ linamaanisha uzuri au urembo au kitu kinachostahili kuonwa. Mzizi wake unamaanisha **mwonekano**, maono, tendo la kuona au kuonwa. Maono yake makali na kuona kwa kinabii kama yaliyo shikamanishwa ndani ya maana ya jina lake. Yalipewa umbo na masharti kwa maelekezo yaliyokuwa wazi sana au maelekezo kutoka kwa Naomi. Kwa kusikia NENO sahihi kunanoa uoni wa kinabii. Naomi alituna na aliendelea tu kuokota katika shamba moja, siyo kuokota katika mashamba

mengi. Hakuhitaji ujumbe mwingine au neno jingine . Hakula katika meza tofauti tofauti . Na cha muhimu zaidi yeye kama mwana wa kiroho aliifahamu nidhamu ya utii kwa kila agizo alilopewa na Naomi baba yake wa kiroho. Hili lilithibitishia kuingia ndani ya jukumu la katikati ndani ya makusudi ya ki ulimwengu ya Mungu ambayo hayajawekwa wazi kwa ajili ya taifa la Israeli.

- Ruthu ni mtiifu kwa maelekezo ya Boazi ya kutokwenda kuokota katika shamba jingine. Utii wake kwa amri hii ulimthibitishia yafuatayo:- utoshelevu, ulinzi, riziki.

Alitii kutoka kwa Boazi.(Ruthu 2:7)... naye ameshinda tangu asubuhi labda hadi kabla ya mchana wakati ambapo Boazi alitokea na kutoa maelekezo haya. Yeye aliendelea kutii maelekezo yake na utiifu huu sasa una mwezesha yeye kupenya na kukaa katika meza ya mlo wa mchana na kuhudumiwa siyo na mmoja wa watumishi isipokuwa na Boazi mwenyewe. Kristo atakuhudumia wewe Neno Lake ndani yako na kwa kupitia maelekezo ya baba wa kiroho.

Ruthu 2:14: Tena wakati wa chakula huyo Boazi akamwambia karibu kwetu, ule katika mkate wetu, na uchovywe tonge lako katika siki, yetu. Basi akaketi pamoja na wavunaji, nao wakampitishia bisi, naye akala, akashiba, hata akasaza.

Aliendelea Kutii : (Ruthu 2:150) Naye akainuka tena ili aende kuokota (Ruth 2:17) Akaokota masazo kondeni hata jioni.

Ule msimamo katika utii wake sasa unazidi kufungua utoaji kwa ajili yake, kama Boazi alivyowaelekeza wavunaji wake kwa kujua waache nyuma yao sehemu kutokana na miganda kwa ajili ya Ruthu. Zaidi kwa hili, Boazi pia alimwelekeza kuendelea kuokota kwa namna hii mpaka mwisho kabisa wa mavuno ya shayiri na mavuno ya ngano.

(Ruthu 2:21] kisha Ruthu mwanamke wa Kimoabu akasema,Boazi akaniambia, ukae hapa karibu na vijana wangu hata watakapo maliza mavuno yangu yote!

(Ruthu 2:23) Hivyo akafuatana na wasichana wake Boazi na kuokota hata mwisho wa mavuno ya shayiri na mavuno ya ngano pia. Naye alikuwa akikaa kwa mkwewe.

Mavuno ya misimu yamefanyika ndio fungu la mtu ambaye utii wake ni imara [muda uliotumiwa katika kipindi hiki katikati ya mavuno haya mawili ulichukuwa pengine miezi michache].

Mavuno yanahusiana na kile ambacho ni cha msimu – kuvuna kunatokea wakati unaofaa kuzalisha kunafikiwa tu katika kipindi hicho. Katikati ya mavuno, kunakuwa hakuna kukusanya chakula kwa wajane wale wawili Naomi na Ruthu. Hili kwao ni habari mbaya. Kwa mwendelezo wa utii wa Ruthu aliendelea kujilisha kutokana na lile shamba kama alivyoelekezwa na baba yake wa kiroho, ambaye sasa anavuna kwa ajili yake kiwango kipya cha kuhifadhi na kwa usalama.

Unapaswa kujiweka wazi mwenyewe mara kwa mara kwa Neno kutoka kwa baba yako wa kiroho

- Unapaswa uipe kipaumbele mikutano inayoitishwa na baba yako wa kiroho na usikose kuhudhuria bila ya sababu ya maana [msingi] kusanyiko na kukusanyika katika mshikamano huamsha unenaji wa Bwana na kwa sababu hiyo huamsha usikivu wa wana wa Mungu.

Kumbukumbu la Torati 4:10- Nikusanyieni watu hawa , nami nitawasikizisha maneno yangu

Mwanzo 49:2 “Kusanyikeni , msikie, enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israel , baba yenu,

Nehemia 8:1 - Na watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la maji, wakamwambia Ezra, mwandishi akilete kitabu cha torati ya Musa, Bwana aliyowaamuru Israeli Watu wanakusanyika kama mtu mmoja ili kulisikia neno la Bwana

Luka 24:32- Wakaambiana , Je mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema.

Luka 24:32- Wakaambiana , Je mioyo yetu [umoja- moyo wetu] haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani , na kutufunulia maandiko?

KJV: Nao wakaambiana mmoja kwa mwingine , je moyo wetu haukuwaka ndani yetu, wakati alipokuwa akizungumza nasi njiani na wakati alipotufunulia maandiko?

Luka 24:33-*Wakaondoka saa ile ile, wakarejea Yerusalemu, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika wao na wale waliokuwa pamoja nao.*

Baada ya kufa na kufufuka kwa Bwana wale mitume walibaki wamekusanyika pamoja. Hii ndio ilikuwa nukta ya egemeo ya historia ya mwanadamu na ndani ya mchakato wa makusudi ya Mungu. Katika muungano huu muhimu [wa maana] katika makusudi ya Mungu duniani, hitaji la kukusanyika linafanyika kuwa ni la maana [muhimu] zaidi ya yote.

Wale kumi na mmoja walio kusanyika walikuwa na hali bora ya kupokea taarifa za wale watu wawili ambao punde tu walitembea na Yesu njiani [barabarani] kuelekea Emau. Waliinuliwa kufatana na matukio katika siku yao na kuingia katika ufahamu sahihi na kuthamini ule ufunuo halisi [mahususi] wa Mungu kwao na kwa ulimwengu katika nukta ile maalum kwa wakati .

- Kurudia rudia ni muhimu kwa ajili ya kuwaimarisha wana.
2 Petro 1:12- Kwa hiyo nitakuwa atayari kuwakumbusha hayo siku zote uwapokuwa manyajua na kuthibitishwa katika kweli niliyo nayo.

Unapaswa kuendelea kujizamisha wewe mwenyewe chini ya sauti inayofaa ya mtu ambaye Mungu amemweka juu yako katika roho. Teknolojia za kisasa kama vile CD, MP3 zenye kurekodiwa, Video zilizorekodiwa upakuzi kutoka tovuti n.k vinatuwezesha kupata fursa za kurudia kusikiliza mahubiri na mafunzo zaidi na zaidi tena. Mlio wa sauti unapaswa uvuvie, tena na kutoa sauti tena, kuendelea kutoa mwangwi ndani ya mtu wa ndani . Hili ni la maana /muhimu sana.

- Ni la muhimu zaidi mtu kulazimika kwa kukusudia kuingia na kuwa na utii wa kile alichokwisha sikia.

Ukumbusho :

Mika 4:2; Na mataifa mengi watakwenda na kusema Njoni twende juu mlimani kwa Bwana na nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake nasi tutakwenda katika mapito yake, kwa maana katika Sayuni itatoka sheria , na neno la Bwana litatoka Yerusalemu.

Nyumba ya BWANA ni kanisa Lake. Kanisa lake kwa umuhimu ni familia inayoongozwa na wababa wa kiroho ambao wananena Neno kwa wana wao wa kiroho. Nguvu kujitoa na uthamani wa kujihusisha kwa wababa wa kiroho na wana wao katika muondoko huu vitapambanua kiwango cha kanuni kwa familia hii ya Mungu katika dunia. Lengo la mwisho ni kwa familia hii ni kuambukiza kila eneo katika jamii kwa njia za Bwana. Kutoka katika kanisa hili NENO LA BWANA , ambalo linafunua zile njia za Bwaan litagawiwa. Wababa na wana katika nyumba ya Bwana ni lazima kwa namna yoyote lihifadhiwe kwa kuangaliwa na hivyo kueleweka na kutoa kipaumbele kwa kuachiliwa kwa Neno la Mungu ndani na kwa kupitia

nyumba ya Mungu. Kufuatana na mjadala uliopo hivi sasa, vitu viwili ndivyo vinavyounda nyumba ya BWANA yenye nguvu.

1. FAMILIA yake yenye tabia ya kuwa na wababa wa kiroho na wana wa kiroho.
2. Kipaumbele chake iliyopewa kutangaza NENO LA BWANA

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Fafanua uhusiano uliopo kati ya kanisa la Mungu na Ufalme wa Mungu.
2. Kanisa ni ‘Nyumba ya Mungu, ni Familia ya Mungu iliyo safi kabisa. Familia hii inaundwaje?
3. Kwa ufupi elezea kanuni ya Kristo ukizingatia ukuu wa Mungu, na kisha oanisha namna mwili wa Kristo, ambao ni kanisa unavyopasa kuangaza kile ambacho ni cha utatu.
4. Kwa usahihi ni namna gani na kupitia nani Neno la Mungu linagawiwa katika Nyumba ya Mungu.
5. Baba yako wa kiroho anapaswa kuwa ndio asili ya msingi wa ustawi wako wa kiroho [jadili maelezo haya]
6. Fikiria umuhimu wa mahudhurio katika mikutano inayopitishwa na baba yako wa kiroho- mikutano ambayo ndani yake neema inaachiliwa kupitia Neno la Mungu.
7. Kusikia sauti ya baba yako wa kiroho mara kwa mara ni muhimu. Elezea hili.
8. Ni nini athari za mwisho za Neno la Mungu linaloachiliwa katika Nyumba ya Mungu kutoka kwa wababa wa kiroho kwa wana wa kiroho kuhusu sekta /Nyanja/ maumbo [au milima] duniani?

NENO LA MUNGU NDIYO NYUMBA YA MUNGU - SEHEMUYA PILI.

Lengo: Yakobo anavyo iona nyumba ya Mungu na mvuto kwa mataifa kuiendea nuru.

Huu ni mwendelezo wa moja kwa moja wa kipindi kilichopita. Ule unabii katika Mika 4:1-3 uliojadiliwa katika kipindi kilichopita unaoneshwa katika kioo katika Isaya 2:1-5

Isaya 2:1-5

1. *Hili ni neno aliloliona Isaya mwana wa Amosi katika habari ya Yuda na Yerusalemu.*
2. *Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima na mataifa yote watauendea makundi makundi.*
3. *Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake, maana katika Sayuni itatoka sheria na neno la Bwana katika Yerusalemu.*
4. *Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi atawakemea watu wa kabila nyingi, nao watafua panga zao ziwe majembe na mikuki yao iwe mundu, taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine wala hawatajifunza vita tena kamwe.*
5. *Enyi watu wa nyumba ya Israel, njoni, twende katika nuru ya Bwana.*

KATIKA SIKU ZA MWISHO

Kipindi cha wakati kinachoelezwa kama ni siku za mwisho kilianza na huduma ya Yesu Kristo hapa duniani na kuendelea.

Waebrania 1:1-2

1. *Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,*
2. *mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*

Petro katika siku ile ya Pentekoste wakati wa umwagiko ule wa Roho Mtakatifu, aliuelezea wakati ule aliokuwa anaishi kama ni siku za mwisho.

Mdo 2:14-17a.-*Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja akapaza sauti yake, akawambia, Enyi watu wa Uyahudi na ninyi nyote mkaao Yerusalemu lijueni jambo hili mkasikilize maneno yangu. Sivyoo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli. Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri, na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto.*

Bado tungali tunaishi katika kipindi cha siku za mwisho na hivyo unabii huu umebeba uhusiano kwa kanisa leo.

MARUDIO KWA KIFUPI

Tabia muhimu ya nyumba ya Mungu ni ile ya kuwa familia. Muundo huu wa kanisa kama familia ndio unaolifanya liwe lenye mamlaka kama serikali duniani. Ni kwa kupitia familia hii, Mwili wa Kristo unajikabidhi kikamilifu kwa Kristo, aliye Kichwa ambaye kwamba ufalme wa Mungu utapata kudhihirika na kuenea katika kila sekta katika jamii kwa pamoja kwa wenyeji hadi ulimwenguni. Shughuli muhimu katika Nyumba ya Mungu ni Neno la Mungu. Neema ya Mungu ambayo ni mchanganyiko muhimu wa vijenzi vyadutu ya Ki-Uungu vya Mungu Mwenyewe, inawasilishwa kupitia Neno la Mungu. Neema hupanga utambulisho wa Mwana, na kwa ukamilifu humpa mwana uwezo wa kufanya mapenzi ya Mungu hapa duniani. Neno la Mungu hutambulisha, asili na mapenzi ya Mungu. Wana wa kiroho katika Nyumba ya Mungu chini ya baba wa kiroho anayeona mbali wanafundishwa Neno la Mungu ili waweze kukua hadi kufikia ukamilifu na kimo cha Kristo. Katika utamaduni wa utii, wana hawa hufanyika kuwa mfano halisi wa Neno. Neno alifanyika mwili, kisha wanaionesha hiyo asili ya Mungu mbele za wanadamu na kutekeleza makusudi Yake hapa ulimwenguni. Hii ndiyo Nyumba ya Mungu. Mataifa watakwenda juu ya mlima wa nyumba ya BWANA nakuomba wafundishwe Njia za Mungu. Njia zinawasilishwa kupitia Neno la Mungu. Neno hili linaletwa kwetu kupitia wababa wa kweli wa kiroho, kama wao siyo mitume, basi angalau wameunganishwa na ubaba, halali wa kitume. Mchakato wa kukwea kwa mataifa kuelekea Nyumba ya Mungu utaongezeka kwa kadri Nyumba ya Mungu inavyokua kwa nguvu na kwa kadri inavyoongezeka katika uwakilishi ulio sahihi wa asili yake ya kweli na katikakutenda kwake.

MTAZAMO WA YAKOBO WA NYUMBA YA MUNGU

Aya ifuatayo inafafanua zaidi namna lile Neno katika ‘Nyumba ya Mungu’- Neno la Mungu linavyowasilishwa kupitia ‘walio tumwa’-yaani wababa wa kiroho wa kitume, ambao wanapokea ufunuo au “NENO” kwa kufungamana na Bwana moja kwa moja katika mbingu [kupitia NENO LAKE], na kisha kuliwekeza kwa wana wao wa kiroho.

Mwanzo 28:10-22

- 10. Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani.*
- 11. Akafika mahali fulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa;, akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale pale.*
- 12. Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimama juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda na kushuka juu yake.*
- 13. Na tazama, BWANA amesimama juu yake, akasema , mimi ni BWANA, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako.*
- 14. Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa Magharibi, na Kaskazini , na Kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa.*
- 15. Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapo kufanyia hayo niliyokuambia.*
- 16. Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, kweli BWANA yupo mahali hapa, wala mimi sikujua.*
- 17. Naye akaogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini, Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni.*

18. *Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe aliloliweka chini ya kichwa chake, akalisisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake.*
19. *Akaita jina la mahali pale BETHEL; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu.*
20. *Yakobo akaweka nadhiri akisema, Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niendeayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae;*
21. *nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu.*
22. *Na jiwe hili nililolisimamisha Kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu; na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.*

Yakobo anaielezea ndoto yake yote kama ‘ ni Nyumba ya Mungu’ – Mwanzo 28:17.

Chunguza vitu vifuatavyo vilivyomo ndani ya ‘Nyumba hii’

▪ **Ngazi inaunganisha Mbingu na Nchi**

Mbingu ni kiti cha enzi cha Mungu na dunia ni mahali pa kuweka miguu yake. Kiti cha enzi ndipo mahali ambapo kutoka hapo Yeye anahimiza mapenzi Yake. Dunia ndipo mahali pa kukutania ambapo mapenzi Yake hupata wepesi wa kukubalika na kupata nguvu. Mbingu inaitazama dunia. Dunia inapata uwezo kutoka Mbinguni. Mazingira ya Nyumba ya Mungu ni mahali ambapo falme hukutana.

▪ **Malaika wanapanda na kushuka**

Kupanda na kushuka kwa Malaika kunatupeleka kwa wababa wa kiroho wa kitume ambao wanaweza kwa neema ya Mungu waliyopewa, kupokea ufunuo au Neno la Mungu kutoka mbinguni na kulitangaza na kulitendea kazi juu ya dunia. [**Rejea kipindi cha 6 kwa maelezo kuhusu malaika**]. Malaika ni wajumbe wa Mungu wanaobeba ujumbe wa ki-uungu. Kila nyumba au kanisa la mahali linasimamiwa na malaika wa Mungu- baba wa kiroho wa kiroho aliyeko duniani anayebeba Neno kutoka kwa Mungu wa mbinguni.

Angalia mahali kwa asili kwa wajumbe hawa ni kutoka dunia-kwanza walipanda kwenda mbinguni kuchukua Neno la BWANA na kisha wanashuka duniani kuliachilia Neno hilo. Hii haitokani na uzoefu wa kimwili. Mwanadamu siku zote alikusudiwa afungamane na falme mbili, yaani mbingu na dunia. Kwa roho zetu tunafungamana na Mungu katika mbingu, na kwa nafsi zetu, kupitia miili yetu tunaweza kufungamana na mwanadamu duniani. Suala hapa ni kwamba, wale ambao wamewekewa alama katika sikio kama wajumbe wa Kristo, wana uwezo wa kipekee waliopewa ki-uungu kufahamu na kutambua nia ya Mungu, mapenzi ya Mungu, Neno la Mungu na wanao uwezo wa kuwasilisha haya kwa wale ambao wamewekwa chini ya uangalizi wao.

Fikiria. Yohana 1:49-51.

49. *Nathanaeli akamjibu, Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israel.*
50. *Yesu akajibu, akamwambia, kwa sababu nilikwambia, Nilikuona chini ya mtini, waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya*
51. *Akawaambia, Amini amin, nawaambia, Mtaziona mbingu zikifunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu.*

▪ **Bwana Anatamka mapenzi Yake kwa nyumba Hii.**

Angalia mstari wa 13-15: Bwana anarudia mapenzi yake kwa Yakobo. Hili siyo jambo jipya, lakini ni mwendelezo wa ahadi ile ile aliyofanya kwa Abrahamu. Yakobo hahitaji kugundua kitu kingine kipya, isipokuwa kile cha asili kilichokwisha ahidiwa kwa Ibrahimu. Hakuna nafasi ya malengo binafsi katika nyumba ya Mungu. Mapenzi ya Mungu kwa kanisa ni kutenda pamoja nakuonesha muundo wake wa asili kwa ajili ya mwanadamu. Yaani kumwakilisha Yeye kikamilifu duniani ikiwa ni pamoja na asili Yake [tabia Yake] na mapenzi yake [kusudi lake]. Yakobo, Kama mwana kwa Isaka na Ibrahimu, ni kuleta udhahirisho mkubwa zaidi kwa nabii zilizokwisha tolewa kwao. Kwa namna hiyo hiyo ni kweli hata kwetu leo. Sisi kama wana wa kiroho katika kaya [familia] yenye kuheshimika ambayo hukondiko makazi yetu , lazima tuendeleo kuwemo ili tuoneshe udhahirisho mkubwa zaidi wa agizo la Mungu walilopewa baba zetu wa kiroho katika Bwana. Lile agizo walilopewa wababa wa kiroho pia linabeba uhusiano wa usanifu wa Mungu uliokuwepo kwa ajili ya mwanadamu kabla mwanadamu kuwepo yaani ule ufanyikaji wa sura ya Kristo na kutumika tukimwakilisha Yeye katika kutekeleza makusudi Yake katika dunia.

▪ **Utambuzi wa uwepo wa Mungu**

Soma mstari wa 16: Nyumba ya Mungu ina uwepo wa Mungu.

Matayo 18:20. “Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.

Kukusanyika katika jina lake kuna maanisha kusanyiko lenye asili na mapenzi Yake. Mahali ambapo kusanyiko katika nyumba au kanisa la Mungu pana elezea sura ya Mungu na kutafuta kukamilisha mapenzi Yake, basi hapo kuna uhakikisho na dhamana ya uwepo Wake.

▪ **Nyumba ni LANGO LA MBINGUNI**

Nyumba ya Mungu ni lango la mbinguni. ‘Lango hugusa mahali penye mpenyo au pa kuingilia. Mlango mkubwa wa kuingilia mbinguni ni kanisa la Mungu. Ufalme wa mbinguni unapatikana kupitia Nyumba ya Mungu. Rasilimali ya mbingu inapatikana kupitia nyumba ya Mungu. ‘Malango ni alama ya mamlaka na nguvu.

Neno Babeli linazungumzia mfumo mwovu wa kinyama wa ulimwengu ambao tunaambiwa tusiupende. Babeli lina maanisha kuchangayikiwa lakini pia ni lango la miungu. Mfumo wa ulimwengu ndio mlango mkubwa ambao shetani anapata mpenyo na mvuto kwa ulimwengu. Nyumba ya Mungu ndiyo mlango mkubwa ambao Mungu anapata mpenyo na kuivuta duni. Milango ya kuzimu haitalishinda kanisa ambalo Yesu analijenga [Mathayo 16:18]. Zingatia ni KANISA LILIOJENGWA dhidi ya ambalo mamlaka ya kuzimu haitaweza kulishinda[kusimama kinyume chake].

NYUMBA ILIYOJENGWA

Mathayo 16:18- “Nami nakuambia , wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisalangu, wala Milango ya kuzimu haitalishinda.

Kanisa linalojengwa ni lile ambalo linajengwa kwa kuweka kanuni kutoka NENO LA MUNGU.

Mdo 20:32”Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu na kwa neno la neema Yake ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa.

Jenga = aikodomeo=jenga, thibitisha, imarisha:

Neno oikodomeo’ lina beba wazo la kusimamisha jengo refu na kulijenga liende juu hadi likamilike au liishe. Urudiaji na ufunuliwaji endelevu wa Neno la Mungu linalotamkwa kupitia baba wa kiroho katika Bwana lina uwezo wa KUKUJENGA WEWE.

Ikiwa kanisa ndilo LANGO [lango kubwa /lenye mamlaka] la mbinguni na kwamba milango ya kuzimu haitaweza kulishinda, basi hii ndiyo njia ya mataifa ya kupitia kwenda kuukwea huu mlima wa Nyumba ya Bwana. Kisha ni nini kinachoanzisha na kuainisha tabia ya “Nyumba ya Mungu kama IMEJENGWA?

Kanuni ya familia.

Ni kanuni ya familia ambamo ndani yake kuna baba wa kiroho anayelisha kiroho, Neno la Mungu huku akiwa anataka kuumba ule ukamilifu wa asili na mapenzi ya Kristo kwa wana wa kiroho katika nymba – [soma nukuu katika somo la 8]

Kila baba wa kiroho anapaswa awe ameunganishwa na rasilimali halali ya kitume na kinabii ili aweze kujenga misingi sahihi [imara] kwa ajili ya kujenga Nyumba juu yake.

Kila nyumba inahitaji msingi sahihi. Katika kuelezea uumbaji, Maandiko yanafundisha kwamba ‘ ile misngi ya ulimwengu iliwekwa na Mungu [soma Mat. 13:35, 25:34, Luk 11:50, Yohana 17:24, Waebrania 4:3, 9:26, 1Petru 1:20, Ufu. 123:8].

Moja ya maneno ya Kiyunani yanayotafisiri neno msingi ni THEMELIOS

Msingi = themelios = kujenga msingi kwa mawe [mawe yanamaanisha maneno] . Neno hili themelios linaundwa na maneno mawili, yaani:-

Thema= kuweka kitu chini na

Tithemi= kuweka kitu. Linamaanisha kuweka kanuni za Neno kimkakati na kiuadilifu- na siyo ovyo ovyo.

Kanisa linajengwa juu ya kanuni za Neno la Mungu zile ambazo zimekwisha fundishwa kwa umakini kimpangilio na kimkakati.

Misingi inawakilisha mifumo ya utendaji ambayo inatawala ulimwengu. Misingi ni kanuni ambazo zinaendesha mfumo wowote ili utende kazi kwa usahihi na kwa kuleta matokeo yanayotarajiwa. Neema ya upako wa Mitume na Manabii, ndipo mahali ambapo kanisa limejengwa juu yake na Kristo Yesu akiwa ndiye mwelekezaji mkuu wa msingi.

Waefeso 2:19-22

19. Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.

20. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.

21. Katika yeye jiwe lote linaungamanishwa na kukaa hata liwe hekalu takatifu katika bwana.

22. Katika yeye ninyi nanyi mnajegwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho

1Wakorinto 3:10-11- *Kwa kadri ya Neema ya Mungu niliyopewa mimi kama mkuu wa-wajenzi mwenye hekima yake naliuweka msingi , na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuweka, yaani, Yesu Kristo.*

Utume na unabii ni kanuni mbili za ujenzi. Mojawapo ya tabia za kiumbo ya kitume ni ule uwezo wa kupenya na kufasiri siri za Kristo [Rejea. Uelewa wa Paulo wa siri za Kristo. soma Waefeso 3:4-5] Paulo kama mjenzi mkuu mwenye hekima aliweka kanuni kutoka Neno la Mungu kwa makanisa ya Wakorintho. Hizi zilikuwa ni za msingi [siyo kama msingi wa mafundisho ya Waebrania]. Kwa maana kwamba zilikuwa ndizo kanuni za awali ambazo zilisimamia maendeleo yote ya kanisa kuelekea ukuaji [ukomavu]. Paulo alijenga msingi huu, na wengine, kama Apolo walijenga juu ya kile alichokianzisha. Lilikuwa ni jambo la maana kwamba ujenzi wa watu wengine ulielekezwa juu yake na uliamuliwa kwa msingi uliojengwa na Paulo. Urefu, uzito na ubora wa jengo lolote unabainishwa na msingi wake. Hakuna jengo la ghorofa linaloweza kujengwa kinyume na msingi unavyoelekeza/taka. Kila kanisa ni lazima liunganishwe na chanzo cha utume na unabii ambacho kinaweza kujenga msingi sahihi kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wenye mafanikio.

Msingi ambao unajengwa na Mitume na Manabii siyo wao, wenyewe kwa kutumia vipawa vya kihuduma ila ni KRISTO. Fundisho la Kitume halijengwi juu ya kanuni za mtume lakini ni juu ya asili ya Kristo. Kanisa halijengwi juu ya matakwa ya mitume isipokuwa juu ya MWAMBA ambao ni Kristo. [Math.16:18, Isaya 28:4] Ikiwa msingi wa Nyumba ya Mungu hauangazii asili na mapenzi ya Kristo, msingi huo siyo sahihi na unapaswa ubomolewe na kujengwa upya-hii ni sehemu ya utendaji wa kitume.

Kufundisha na kuhubiri mafundisho ya kitume yanayohusika na yaliyo endelevu.

Kuwa na utii hai kwa kujihusisha na Neno linaloachiliwa.

Utii wako kwa Neno hili huumba msingi imara wa mfanano na Kristo na ukweli katika maisha yako utakuinga dhidi ya mashambulizi ya kishetani.

Luka 6:46-48

46. Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana walakini hamyatendi nisemayo?

47. Kila mtu ajaye kwangu, na kuyasikia maneno yangu na kuyatenda, nitawaonesha mfano wake.

48. Mfano wake ni mtu ajengaye nyumba, na kuchimba chini sana, na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika, mto uliishukia nyumba ile kwa nguvu, usiweze kuitikisa; kwa kuwa imejengwa vizuri.

Jiwe au Nguzo ya Nyumba ni Uwana

Katika kitabu cha Mwanzo 28:18 neno la Kiebrania linalotafsiri neno ‘jiwe’ ni ‘**eben**’ ambalo mzizi wake ni ‘ben’ likimaanisha ‘mwana’ ambaye ndiye mjenzi wa jina la familia. Jina la Mungu [ambalo ndilo linaloakisi asili na mapenzi] Yake. Jiwe litatumika kama mto wa Yakobo wakati ule alipopata ndoto. Mto unaweza kupatikana kwa usingizi kuashiria mahali pa KUPUMZIKIA. Uwana huzalisha hali ya kiroho ya KUPUMZIKA ambayo inatokana na utii [

soma Zab 127]. Jiwe hili baadaye lilipakwa mafuta kama ni NGUZO. Nguzo inashikilia na kuimarisha jengo la nyumba . Nguzo hii pia ni ufafanuzi wa uwana uliokomaa.

Zaburi : 144:12-Wana wetu na wawe kama miche waliokuwa ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu.

Wana ni nguzo ambazo zimekomaa kupitia kutii fundisho la kitume.

Wagalatia 2:9a- tena walipo kwisha kujua ile neema niliyopewa, Yakobo na Kefa, na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika.

Kujitoea kutoa kikumi kuitikia kilicho ufunuo wa Nyumba ya Mungu.

Yakobo alikuwa na moyo wa kuunga mkono kifedha kile alichokiona ndani ya nyumba ya Mungu. Utoaji wake wa kikumi ulitokana na ufunuo wa ujenzi usiokuwa wa kawaida wa nguvu ya ndani ya Nyumba ya Mungu.

Kwa ajili ya utendeaji kazi eneo la kutoa ‘kikumi’ rejea kwenye mwongozo wangu unaosema utotaji zaidi ulio sahihi. Unaweza kuupakua kutoka tovuti yangu, www.randolfbarnwell.com Com AU kutoka www.thekingdomplatform.com]

Rudi kwa Isaya 2 na Mika 4

MATAIFA, WALIOVUTWA KWA NURU WATAPANDA JUU KWENYE NYUMBA YA BWANA KWENDA KUFUNDISHWA.

Isaya 2:3-*Na mataifa mengi watakwenda na kusema, njooni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake; maana katika Sayuni itatoka sheria na neno la BWANA katika Yerusalemu.*

Kitu ambacho mataifa watatafuta kutoka Nyumba ya Bwana ni NJIA za Mungu, ili waweze kutembea katika njia za Bwana. Neno la Mungu linafunua njia za Mungu na kurekebisha mienendo yetu tutembeapo katika njia Yake. Sheria ya Mungu na neno la Mungu hutoka katika Nyumba ya Mungu. Hatimaye kila mwana wa Mungu ndani ya Nyumba ya Mungu anafanyika kuwa Neno la Mungu yaani barua ya Kristo. Mwana anafanyika kuwa funzo la Mungu kwa ulimwengu. Kila wakati tutakuwa tunajihusisha na tendo la kufundisha, lakini lililo muhimu zaidi ni mwana kufanyika neno katika mtindo wake wa maisha na tabia; na hivi ndivyo mataifa wanavyo fundishwa njia za Mungu.

Isaya 54:13- *Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi.*

Wale ambao hawajamjua BWANA, watajiunga na kujishikiza wao wenyewe katika nyumba ya Bwana- kwa wana ambao wanazishikilia njia na Neno la Mungu.

114: Isaya- *Maana BWANA atamhurumia Yakobo atamchagua Israeli tena naye atawaweka katika nchi yao wenyewe , na mgeni atajiung nao, nao wataambatana na nyumba ya Yakobo.*

Kutakuwepo na kufurika kwa wingi kwa mataifa kuingia katika nyumba ya Mungu ambayo sasa inajengwakwa usahihi. Muktadha ambao unafanya hili litokee, ni kule kuwa na giza nene na machafuko ya kiulimwengu juu ya nchi. Watakutwa kuelekea NURU ya Mungu iliyomo ndani ya watu wa Mungu. Kama zilivyo siasa za ulimwengu , uchumi, uchafuzi wa hali ya

hewa unavyo zidi. Nyumba ya Mungu itaharakisha kufikia ukomavu wa hali ya juu na kuwa na utayari wa kuyapokea mataifa ya dunia.

Isaya 60:1-5

1. *Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia.*
2. *Maana, tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali Bwana atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako.*
3. *Na mataifa wataijilia nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako.*
4. *Inua macho yako, utazame pande zote, wote wanakusanyana; wanakujia, wewe, wana wako watakuja kutoka mbali, Na binti zako watabebwa nyongani*
5. *Ndipo utakapoona na kutiwa nuru, Na moyo wako utatetemeka na kukunjuka; kwa kuwa wingi wa bahari utageuzwa kukujia, utajiri wa mataifa utakuwasilia.*

Isaya 2:5-Enyi wa nyumba ya Israeli, *njooi, twenda katika nuru ya BWANA.*

**NENO LA MUNGU, ROHO YA MWANADAMU NA MUNGU KUUWEKA WAKFU
UONGOZI WA UBABA, VYOTE VINAFANANISHWA NA TAA/NURU.**

TAFAKARI MAANDIKO YAFUATAYO.

Mithali 20:27-Pumzi ya mwanadamu ni taa ya BWANA, hupeleleza yote yaliyomo ndani yake.

Zaburi 18:28-Kwa kuwa wewe unaiwasha taa yangu, BWANA Mungu wangu ananiangazia giza langu.

Zaburi 119:105-Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu

Mithali 6:23-Maana maagizo hayo ni taa, na sheria hiyo ni nuru. Na maonyo ya kuwaadilisha mtu ni njia ya uzima

Zaburi 19:8-Maagizo ya Bwana ni ya adili humfurahisha moyo Amri ya BWANA ni safi, Huyatia macho nuru.

Ayubu 29:3-Hapo taa yake ilipomulika juu yangu kichwani Nami nilitembea gizani kwa njia ya mwanga wako.

Zaburi 119:130- Kufafanusha maneno yako kuwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga.

2Sam 21:17b-Ndipo watu wa Daudi wakamwapia, wakasema, wewe hutatoka tena pamoja nasi kwenda vitani usije ukaizima taa ya Israel.

Neno la Mungu ni nuru, lakini nuru hii inapatikana tu wakati neno hili linapo kunjuliwa [funuliwa].

Funua/kunjua = pethach maana yake ni:-**uwazi, ingilio, njia ya mlango. Ni kiashiria cha mpenyo katika kitu fulani.**

Hata hivyo, tunahitaji kuwa na wababa wa kiroho waliounganishwa na chanzo cha neema ya kitume ambao wana uwezo wa kufafanua ile nuru ya Neno la Mungu, wakifunua ukweli wake kwa kina na matokeo yake ni kupata hekima na uelewa. Ukichunguza mistari iliyoorodheshwa hapo juu, utaona kuna aina mbili za ufafanuzi wa neno nuru yaani 'taa na mwanga. Ile 'taa' ya Neno ni agizo mahususi la Mungu linalotoa nuru na kuweka wazi mienendo yetu ya kila siku. [Linganisha na Zab 119:105 pamoja na Mith.6:23]. Nuru ya Neno ni kanuni au fundisho ambalo lina uwezo wa kuangazia njia zetu, na kutupa mwelekeo wa muda mrefu na wenye

uwazi kwa ajili ya safari iliyoko mbele yetu. Fundisho hubainisha njia na agizo hutoa mwanga kwa hatua zetu tunapokuwa njiani. Agizo la Bwana hufumbua macho yetu.

Yohana 1:1-4

1. *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu*
2. *Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.*
3. *Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.*
4. *Ndani yake ndimo mlimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.*

Uzima halisi wa mwana aliyejawa na Neno na ni mtiifu wa Neno ni NURU. Uzima wa mwana wa Mungu unafanyika kuwa nuru ya watu na inawavuta. Nuru inawakilisha ufunuo, mng'ao, uelewa, kuona kinabii n.k. Pia inaashiria utakatifu, uwazi, na uadilifu. Mataifa yatafutwa kwa sifa hizi katika Nyumba ya Mungu. Kitu wanachotafuta Mataifa ni kile tunacho kisherehekea sisi tulio katika Nyumba ya Mungu.

Mojawapo ya alama ya kuiwakilisha nuru ni upendo. Utamaduni wa Upendo usio na masharti katika Nyumba ya Mungu miongoni mwa wana wa Mungu utakuwa ni NURU yenye kuuvuta ulimwengu.

1Yohana 2:8-10

8. *Tena nawaandikia amri mpya, neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu, kwa kuwa giza linapita na ile nuru ya kweli imekwisha kung'aa.*
9. *Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa.*
10. *Yeye ampendaye ndugu yake, akaa katika nuru, wala ndani yake hamna kikwazo.*

Kazi zetu- tabia na utendaji wetu ulimwenguni – vitashawishi mataifa yaje katika Nyumba ya Mungu kufundishwa njia za Mungu.

Matayo 5:16-Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.

Kwa maombi, tafakari aya zifuatazo ambazo zaweza kutendewa kazi katika kanisa la leo.

Zakaria 8:20-23

20. *BWANA wa majeshi asema hivi, itatokea halafu ya kwamba watakuja mataifa na wenyeji wa miji mingi;*
21. *Wenyeji wa mji huu watauendea mji huu, wakisema, Haya! Twendeni zetu kwa haraka tuombe fadhili za BWANA, na kumtafuta BWANA wa majeshi. Mimi nami nitakwenda.*
22. *Naam, watu wa kabila nyingi na mataifa hodari watakuja Yerusalemu kumtafuta BWANA wa majeshi, na kuomba fadhili za BWANA.*
23. *BWANA wa majeshi asema hivi, siku hizo watu kumi, wa lugha zote za mataifa, wataushika upindo wa nguo yake yeye aliye Myahudi; naam, wataushika wakisema, Tutakwenda pamoja nanyi kwa maana tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi.*

‘Mataifa hodari-----inazungumzia kuhusu mataifa yenye nguvu ambayo yanashika nafasi za kimkakati katika masuala ya ki-ulimwengu.

Watu kumi-----labda inazungumzia kuhusu walengwa maalum kimkakati katika kila taifa.

‘Myahudi----inazungumzia kuhusu Mwana wa Mungu mkomavu au nyumba ya Mungu iliyokomaa hapa duniani.

‘Kanzu-----inazungumzia kuhusu ‘upindo wa neema au upako’ na pia inazungumzia kuhusu utayari na kuwekezewa kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya majukumu maalum.

Tutakwenda pamoja nanyi---- inaangazia kuhusu kilio cha mataifa, siyo tu kule kunyooshwa ili yawe sawa na Nyumba ya Bwana, lakini ni kule ku-ambukizwa kwa ku-ingizwa katika ujenzi wake halisi.

‘Utambuzi wa uwepo wa Mungu kwa mataifa na fadhila zake juu ya nyumba yake inayo jengwa utakua na kuwavuta waje waingie.

Yeremia 29:5-13

6. *Jengeni nyumba, mkakae ndani yake; kapandeni bustani, mkale matunda yake;*
7. *Oeni wake, mkazae wana na binti, kawaozeni wake wana wenu, mkawaoze waume binti zenu, wazae wana na binti; mkaongezeke huko wala msipungue.*
8. *Kautakieni amani mji ule, ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa BWANA; kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani.*
9. *Maana Bwana wa majeshi, Mungu wa Israel, asema hivi, Manabii walio kati yenu, na wabashiri wenu, wasiwadanganye ninyi, wala msisikilize ndoto zenu, mnazootesha.*
10. *Kwa maana kwa jina langu hutabiri maneno ya uongo kwenu; mimi sikuwatuma, asema BWANA.*
11. *Maana BWANA asema hivi, Babeli utakapotimiziwa miaka sabini, nitawajilia ninyi, na kulitimiza neno langu jema kwenu, kwa kuwarudisha mahali hapa.*
12. *Maana ninayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.*
13. *Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta, na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.*

Ndani ya mfumo wa Kibabeli wa ki-ulimwengu uliopo hivi sasa tunapaswa kujenga nyumba yaani kujenga NYUMBA YA MUNGU ambayo itakuwa na matokeo chanya juu ya ustawi wa jamii zinazo izunguka. Cha muhimu ni kwamba nyumba hii, ambayo ni familia ya Mungu-Mwili wa Kristo, iwe INAJENGWA’ kupitia fundisho sahihi la kitume. Neno lililomo katika nyumba hiyo, ndilo linalotafutwa na mataifa.

NYUMBA YA KWELI YA MUNGU INAPASWA KUKUA NA KUWA NA NGUVU ZAIDI NA ZAIDI.

Samwel 3:1-2

1. *Basi kulikuwa na vita siku nyingi kati ya nyumba ya Sauli na nyumba ya Daudi; Daudi akaendelea akastawi, lakini nyumba ya Sauli ikaendelea kudhoofika.*
2. *Naye Daudi akazaliwa, wana huko Hebroni;*

Kuna kasi ya mauti na kudhoofishwa kwa ‘NYUMBA’ [makanisa] sahihi na ongezeko la uimarishwaji sahihi wa NYUMBA. Daudi ni ufafanuzi wa kanisa la kweli na Sauli ni ufafanuzi wa kanisa lisilo sahihi. Kanisa la kweli linajengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, likitenda kazi kama kaya yaani familia ya Mungu. Kanisa hili lina wababa na wana wa kiroho, mahali ambapo msisitizo ni kuhusu ku-umbika kwa ukamilifu wa Kristo ndani ya kila mwana ambaye hatimaye anaonesha kwa vitendo asili ya Mungu na kutekeleza mapenzi Yake. Nyumba hii inakua na kuwa na NGUVU ZAIDI duniani hivi leo. Wakati makanisa ambayo ni taasisi za kidini [Sauli] yanaendelea kudhoofika. Neno la Bwana ndani ya nyumba zilizo sahihi litayavutia na ku-ambukizwa kwa mataifa, kama vile Yuda na Israel walivyokusanyika kwa

Daudi kule Hebroni [ikimaanisha ‘muungano’ shirikisho linalohusisha agano, upendo na mshikamano.]

BETHELI LAZIMA IFANYIKE KUWA EL-BETHELI

Yakobo alitoka Betheli [Nyumba ya Mungu] kwenda Remieli [uso wa Mungu] na kisha akaipa Betheli jina jipya yaani EL-Betheli [Mungu wa Nyumba ya Mungu au ‘Nyumba imara ya Mungu’ Mwanzo 28:19,32,35 - Pale Penuel baada ya kushikana mieleka na Bwana, asili yake ilibadilishwa na hili linaashiriwa na kubadilishwa kwa jina lake, kutoka Yakobo na kuitwa Israeli . Katika kuona USO au asili ya Mungu anabadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu. Kisha baadaye akapatana na ndugu yake waliokuwa wamefarakana yaani Esau. Wakati uso wa Mungu [asili na tabia ya Mungu] vinaposhudiwa katika Nyumba ya Mungu, Nyumba ya Mungu inafanyika kuwa yenye nguvu ya Mungu. Neno la Mungu linafunua uso na asili ya Mungu kama tulivyofundisha katika somo la 1 na 2 la mtiririko huu. Nyumba ya Mungu inakuwa na nguvu zaidi na zaidi wakati uwasilishaji wake wa uso wa Mungu unapongezeka. Wana wa kiroho katika nyumba ya Mungu watatii kila fursa kwa ajili ya mabadiliko na marekebisho binafsi katika tabia zao na pia wataanza kuishi kwa maelewano na upendo usio na masharti na ndugu wote katika mwili mkubwa wa Kristo.

Kisha Yakobo akaenda Bethlehemu –Nyumba ya Mikate [Mwanzo 35] ambayo inadokeza uwezo wa kugawa neema na Kristo kupitia Neno Lake. Makazi yake ya mwisho yalikuwa ni mnara wa **Ederi** wenye maana ya:- *’kundi’, kuhifadhi cheo, kutunza ili kwamba, kuto pungukiwa na chochote* [Mwz 35:21] .Hii ni nafasi ya kiserikali katika roho. Kuna mpango uliopangiliwa wa kundi la wana wa Mungu kwa neno la Mungu nahili huliwezesha kwa kumaanisha kama ndiyo ngome duniani. Neno hili Ederi lina maana sawa na neno mnara wa kundi katika kitabu cha Mika 4:8.

Mika 4:8-10a

8. *Na wewe, Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam,mamlaka ya kwanza yatakuja,ufalme wa binti Yerusalemu.*
9. *Sasa mbona unapiga kelele? Je hakuna mfalme kwako, mshauri wako amepotea, hata umeshikwa na utungu kama mwanamke wakati wa kuzaa?*
10. *Uwe na utungu, utaabike ili uzae, Ee binti Sayuni, kama mwanamke mwenye utungu ;*

MASWALI NA MASUALA YA REJEA BINAFSI NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Ni wakati gani kipindi katika historia ya mwanadamu kilielezwa Kama ni siku za mwisho zinaanza?
2. Kutokana na usomaji wako wa somo lililopo, kilichopo katika ufahamu wako, kita ainisha Nyumba ya Mungu kama ndiyo iliyo KUU juu ya milima mingine [mamlaka ya ushawishi] hapa duniani?
3. Ni nini kilio cha watu na mataifa kama wanavyokuja kukwea juu ya Nyumba ya Bwana?
4. Yakobo, katika ndoto yake iliyonukuliwa katika Mwanzo 28, ilikuwa na mwonekano wa michoro ambayo yeye aliita nyumba ya Mungu. Fafanua sehemu mbalimbali na nguvu zilizomo ndani ya nyumba hii iliyo onwa na Yakobo.
5. Pia Yakobo alielezea Nyumba ya Mungu kama Lango la Mbinguni. Hili lina maanisha nini?

WITO WA KUANGAZA KAMA MIANGA DUNIANI.

Lengo: Wito wa kuwa nuru.

Daniel 5:14: *Nimesikia habari zako, kwamba roho ya miungu imo ndani yako, na kwamba nuru na ufahamu na akili bora zimeonekana kwako [NASB].*

Daniel 5:14: *Hata nimesikia habari zako, kwamba roho ya miungu imo ndani yako, na nuru hiyo na ufahamu na hekima sahihi vimeonekana kwako [NKJV].*

YESU NI NURU

Yoh 8:12- *Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.*

Yoh 9:5- *Muda nilipo ulimwenguni mimi ni nuru ya ulimwengu.*

SISI NI NURU YA ULIMWENGU

Yoh 12:35-36 *Basi Yesu akawaambia, Nuru ingaliko pamoja nanyi muda kidogo, Enendeni maadamu mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza, maana aendaye gizani hajui aendako. Maadamu mnayo nuru, iaminini nuru hiyo, ili mpate kuwa wana wa nuru. Hayo aliyasema Yesu, akaenda zake, akajificha wasimwone.*

Matayo 5:14-16

14. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima
15. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani
16. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.

UZIMA = NURU=NENO

Yoh 1:1-5

1. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.
2. Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu.
3. Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.
4. Ndani yake ndimo mlimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.
5. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.

Yoh 1:14: *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa baba amejaa neema na kweli.*

Isaya 2:1-5

1. Hili ni neno aliloliona Isaya mwana wa Amози katika habari za Yuda na Yerusalemu.
2. Na itakuwa katika siku za mwisho mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima nao utainuliwa juu, juu ya vilima na mataifa yote watauendea makundi makundi.

3. *Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni twende juu mlimani kwa BWANA nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake nasi tutakwenda katika mapito yake, maana katika Sayuni itatokea sheria, na Neno la BWANA katika Yerusalemu.*
4. *Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi, nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu, taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe.*
5. *Enyi watu wa nyumba, njooni twende katika nuru ya BWANA.*

**NENO LA MUNGU, ROHO YA MWANADAMU NA UONGOZI WA UBABA
ULIOWEKWA WAKFU NA MUNGU, VYOTE VINAFAANANISHWA NA TAA/NURU.**

YATAFAKARI MAANDIKO YAFUATAYO:

Mithali 20:27 *Pumzi ya mwanadamu ni taa ya Bwana. Hupeleleza yote yaliyomo ndani yake.*

Zaburi 18:28 *Kwa kuwa wewe unaiwasha taa yangu, Bwana Mungu wangu aniangazia giza langu.*

Zaburi 119:105 *Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.*

Mithali 6:23 *Maana maagizo hayo ni taa, na sheria hiyo ni nuru, Na maonyo ya kumwadiisha mtu ni njia ya uzima.*

Zab 19:8 *Maagizo ya Bwana ni adili, Huufurahisha moyo. Amri ya Bwana ni safi, Huyatia macho nuru.*

Ayubu 29:3 *Hapo taa yake ilipomulika juu yangu kichwani, Nami nilitembea gizani kwa njia ya mwanga wake.*

Zab 119:130 *Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga.*

2 Sam 21:17b *Ndipo watu wa Daudi wakamwambia wakasema wewe hutatoka tena pamoja nasi kwenda vitani usije ukaizima taa ya Israeli.*

UPENDO KWA NENO= UPENDO KWA MUNGU NA KWA WATU WENGINE.

Amri kuu kabisa iliyotolewa na Bwana ni kumpenda Mungu na kupendana sisi kwa sisi.

Matayo 22:37-39

36. *Mwalimu katika torati ni amri ipi iliyo kuu?*
37. *Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.*
38. *Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.*
39. *Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.*

Yohana 13:34 *Amri mpya nawapa, mpendane, Kama nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.*

[Nukuu ya ziada: Amri inayohusu kupendana sisi kwa sisi inaendelezwa na:- kama nafsi yako [Matayo. 22:39] hadi kama nilivyowapenda ninyi? [Yoh 13:34]

Upendo wako kwa Mungu unathibitishwa kwa msimamo wako kwa Neno Lake, hususani kiwango chako, cha utii kwa Neno Lake. Yesu alisema kwamba, kama tunampenda Yeye, ni lazima tuzitende amri zake.

Yoh 14:15 *Mkinipenda mtazishika amri zangu*

Kwa kiwango kile kile ambacho wewe ni mtiifu kwa amri za Mungu ni kwa kiwango hicho hicho utampenda Yeye. Hakuna kipimo nyingine ambacho utatumia kupima upendo wako kwa Mungu, isipokuwa ni kwa kiasi gani unazitii amri zake katika Neno Lake.

Kumpenda Mungu kunakamilishwa ndani kwa wewe kulishika Neno Lake. Masuala haya ya kumpenda Mungu kwa mkono mmoja na kulishika Neno Lake kwa mkono wa pili, siyo masuala mawili tofauti, Lakini mkono mmoja unatoa uthibitisho kwa mkono wa pili.

1 Yoh 2:4-5

4. *Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.*
5. *Lakini yeye alishikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.*

Katika Yohana 14, Yesu alionesha kwamba ulimwengu hautamuona YEYE, lakini sisi, wanafunzi wake tutaweza kumwona. Kwa namna gani? Yeye na Baba Yake watafanya wenyewe wajulikane kupitia Neno Lake kwa wale wanao litii.

Yohana 14:19-26

19. *Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni, tena bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.*
20. *Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu,*
21. *Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*
22. *Yuda [siye Iskaariote] akamwambia, Bwana imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu?*
23. *Yesu akamwambia Mtu akinipenda atalishika neno langu na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*
24. *Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu' nalo neno mnalolisikia silo langu, ila lake Baba Aliyenipeleka.*
25. *Hayo ndiyo niliyo waambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu.*
26. *Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyo waambia.*

Kuwa na kuzishika amri za Mungu kunakuweka katika nafasi ya kufikia udhihirisho wa kipekee wa upendo wa Baba na Mwana, [mst wa 21] ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kushiriki baadhi ya mafunuo ya Mungu mwenyewe kwako.

Kushindwa kumpenda Mungu kwa kutolipenda na kulitii Neno Lake kunauweka hatarini msimamo wako kwa kaka na dada zako katika mwili wa Kristo.

1 Yohana 5:2-3

2. *Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake.*

3. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba twazishika amri zake, wala amri zake si nzito

Mstari wa pili unatoa wazo kwamba, ikiwa mtu haupendi Mwili wa Kristo- familia ya Mungu – Kaka na dada zako katika Kristo utakuwa unaonesha kwa vitendo ukosefu wa kutokumpenda Mungu kwa kuliasi Neno Lake. Kumpenda Mungu na Neno Lake siyo suala binafsi au la siri peke yake maadamu kutotii amri zake kunatoa uthibitisho wa kukosa upendo kwa Mungu, na kutotii huko kusikofaa huathiri jamii ya watakatifu ambayo na wewe ni miongoni mwao [angalia athari hasi kwamba dhambi ya Akani ilivyo athiri mafanikio ya Israeli katika uwanja wa vita – soma **Yoshua 7**]

Upendo kwa Mungu hauelezewi kama ni msisimko wa hisia chanya wa kimapenzi kwa Mungu. Inawezekana ni pamoja na hili, lakini hili halioneshi kuwepo kwa upendo kwa Mungu. Upendo kwa Mungu ni pale tu unapopimwa kwa njia moja nayo ni:- kwa kiwango cha utii kwa Neno lake.

2Yohana 1:6: *Na huu ndio upendo, tuenende kwa kuzifuata amri zake. Hii ndiyo ile amri, kama ulivyosikia tangu mwanzo kwamba mwenende katika hiyo.*

SHAUKU KALI NDANI NA KWA NENO LA MUNGU.

SHAUKU= Chephets maana yake ni *tamani, furaha , kuwa na mwelekeo kwa kitu au kuwa na hamu.*

Katika kulitii Neno Lake, kwanza mtu anapaswa AFURAHIE na kuwa na SHAUKU KALI kuhusu Neno Lake. Ili kulifurahia Neno Lake, ni lazima mtu auone ule uthamani wa Neno na kulipa kipaumbele cha hali ya juu sana. Kile ambacho unakiheshimu, utakipenda, na kile unachokipenda, utakitii.

BARAKA ZA KULIFURAHIA NA KULIPENDA NENO LA MUNGU

Shauku ‘Huwezesha kuwa na ‘utii’

Zab 119:35 *Uniendeshe katika mapito yako maaagizo yako, kwa maana nimependezwa nayo,*

Ayubu 23:12 *Sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake; Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu.*

Angalia sababu iliyomfanya Ayubu amtii Mungu na kumfanya asiachane na amri za kinywa cha Mungu, ni kwa sababu, alifanya maamuzi ya kuyathamini maneno ya Kinywa Chake-zaidi sana kuliko hata chakula muhimu cha mwili. Heshima yako kubwa kwa maneno yake kunauwezesha utii wako kwa ajili yake.

Amri Za Mungu siyo nzito kwa mtu ambaye anampenda Yeye na neno Lake.

1Yoh 5:3 *Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake, wala amri zake si nzito.*

Kumbukumbu la torati 30:8-20

8. Nawe utarudi, uitii sauti ya BWANA na kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo.

9. Na Bwana , Mungu wako atakufanya uwe na wingi wa uheri katika kazi yote ya mikono yako katika uzao wa tumbo lako na katika uzao wa ng’ombe wako na katika uzao wa

nchi yako kwa kuwa BWANA atafurahi tena juu yako kwa wema, kama alivyofurahi juu ya baba zako.

10. *Ukiwa utafuata sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa kuyashika maagizo yake, na amri zake zilizoandikwa katika chuo hiki cha torati, ukimwelekea BWANA Mungu wako, kwa moyo wako wote, Na Kwa roho yako yote.*
11. *Kwa maana maagizo haya nikuagizayo leo, si mazito mno kwako, wala si mbali.*
12. *Si mbinguni hata useme, Ni nani atakaye tupandia mbinguni akatuletee, aje atuambie, tusikie, tupate kuyafanya?*
13. *Wala si ng'ambo ya pili ya bahari hata useme, Ni nani atakaye tuvukia bahari, akatuletee, aje atuambie, tusikie tupate kuyafanya?*
14. *Lakini neno li karibu nawe sana, li katika kinywa chako na moyo wako, upate kulifanya.*
15. *Angalia nimekuwekea Leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya.*
16. *Kwa hivi nikuagizayo leo kumpenda BWANA MUNGU wako, kuenenda katika njia zake, na kushika maagizo yake, na amri zake, na hukumu zake, upate kuwa hai na kuongezeka, BWANA Mungu wako, apate kukubarikia katika nchi uingiayo kumiliki.*
17. *Lakini moyo wako, ukikengeuka, usipotaka kusikiliza, lakini ukavutwa kando kwenda kuabudu, miungu mingine, na kuitumikia.*
18. *Nawahubiri hivi leo hakika mtaamgamia, hamtaazifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi, uivukiayo Yordani, uingie kuimiliki.*
19. *Naishuhudia mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, Baraka na laana, basi chagua uzima ili uwe hai, wewe na uzao wako,*
20. *kumpenda Bwana, Mungu wako, kuitii sauti yake, na kushikamana naye, kwani hiyo ndiyo uzima wako, na wingi wa siku zako, upate kukaa katika nchi Bwana aliyo waapia baba zako, Ibrahimu , na Isaka , na Yakobo, kuwa atawapa.*

Angalia namna haya yafuatayo yote yalivyohusiana /mst wa 20]

Kumpenda Mungu – kuitii sauti Yake- kumshika Yeye kabisa. Kisha yanafuata maelezo yenye nguvu, 'Kwani huu ndio uzima wako.

- Baraka huambatana na utii- soma mistari ya 9,10 na 16 hapo juu
- Laana huambatana nakuto tii(uasi) soma mistari ya 15,17 na 18 hapo juu.

Shauku ndani ya Neno la Mungu Humwezesha mtu Kuvumilia Mateso.

Uwapo katikati ya taabu siku zote jiulize mwenyewe.

1. Je! Jaribu hili ni matokeo ya kutotii kwangu mimi? Jibu likiwa ndiyo tubu na tii. Wakati ambapo matokeo halisi ya kutotii kwetu yanaweza kutumiwa na Mungu ili kutufikisha mahali pa kuamini zaidi na kuwa na utiii thabiti kwa Neno Lake.

Zaburi 119:67- *Kabla sijateswa Mimi nalipoteta, Lakini sasa nimelitii neno lako.*

2. Je ! jaribu hili ni la kiulimwengu lililoanzishwa na Mungu katika kukusudia kukamilisha mitazamo ya kimkakati ya mapenzi Yake kwa taifa au kwa jamii fulani mahsusi? (K.v. kwa Elia alipokuwa katikati ya miaka 3 ya njaa; au Israeli katika mapigo yale kule Misri)
3. Je, hili ni jaribu langu kwa sababa ya kuruhusiwa Kiuungu na Mungu ili kukamilisha mambo fulani ndani ya maisha yangu? Inawezekana Mungu anataka kukamilisha utii wako kupitia jaribu lako. Ingawa Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu, ALIJIFUNZA utii kupitia mateso yaliyompata – soma **Waeb 5:8**.

Zaburi 119:71 *Ilikuwa vema kwangu kuwa naliteswa, Nipate kujifunza amari zako.*

Katika nyakati hizi za mateso na taabu ni lazima mtu kutokutilia mashaka ahadi za Mungu zinazo ambatana na utii na kuanza kupoteza nia na mapenzi ya kuendelea kumtii Mungu.

Ayubu 6:10= NASB- *Hapo ndipo ningefarijika hata sasa, Naamu, ningejikuza katika maumivu yanayoniacha kwa kuwa sijayakana maneno yake Mtakatifu.*

CEN-*Kisha ningefarijika hata sasa, nikijua kwamba katika maumivu yangu yote, sikuyakana maneno yake Mtakatifu.*

ERV:*Kisha ningefarijika kwa jambo hili moja, Hata kwa kupitia maumivu haya yote, kamwe sikukana kutii amri za aliye Mtakatifu.*

NrV- *Kisha bado Nina kitu kimoja cha kunifariji mimi Ingekuwa kwamba sijasema hapana kwa amri ya aliye Mtakatifu. Hivyo ingenipa mimi furaha pamoja na maumivu yangu yasiyokoma kamwe.*

Ikiwa ni kwa namna iwayo yote, unateswa na majaribu na matatizo **amuai kamwe** usiipoteze shauku yako kwa Neno la Mungu.

Zaburi 119:92-*Kama furaha yako isingelikuwa furaha yangu, Hapo ningalipotea katika taabu zangu.*

Zaburi 119:49-50- *Likumbuke neno ulilomwambia mtumishi wake kwa sababu umenitumainisha. Hii ndiyo faraja yangu katika taabu yangu, Ya kwamba ahadi yako imenihuisa.*

Ukumbusho: Rudia sehemu ya 3 katika mtiririko huu wa mafunzo. Kila Neno au ahadi ambayo mtu aliitoa itajaribiwa katika maisha yake. Utapitia majaribu mengi mpaka Neno lifanyike mwili ndani ya maisha yako .Yusufu alikuwa mhanga wa kujaribiwa mengi na Mungu, na yote haya yalikuwa ni sehemu ya mchakato wa Mungu wa kumtengeneza na kumuandaa ili awe tayari kukamilisha hatima ya wito wake. Elewa kwamba kujaribiwa kwako ni kwa sababu ya Neno unalosikia.

Zaburi 105:19- *Hata wakati wakuwadia Neno Lake. Ahadi ya Bwana ilimjaribu.*

Ufunuo 1:9- *Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu , na ushuhuda wa Yesu.*

Mwiba wa Paulo ndani ya mwili, iwe ni kitu gani hiki kilikuwa kiliruhusiwa na Mungu ili kumfanya awe mnyenyekevu kwa mtazamo wa wingi wa mafunuo aliyopewa yeye.

2Wakorintho 12:7-10

7. *Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nilipewa mwiba katika mwili mjumbe wa shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi*
8. *Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke.*
9. *Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.*
10. *Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana ninapokuwa dhaifu ndipo nilipo na nguvu.*

SHAUKU KATIKA NENO NA KWA NURU YAKE UTaweza KUTEMBEA KUPITIA NYAKATI ZA GIZA.

Zaburi 18:28-*Kwa kuwa wewe unaiwasha taa yangu, BWANA Mungu wangu aniangazia giza langu.*

Mithali 20:27- *Pumzi ya mwanadamu ni taa ya BWANA hupelekea yote yaliyomo ndani yake..*

Zaburi 119:105:*Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.*

Mithali 6:23-*Maana maagizo, hayo ni taa na sheria hiyo ni nuru, Na maonyo ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima.*

Zab 19:8-*Maagizo ya BWANA ni ya adili. Huufurahisha moyo. Amri ya Bwana ni safi huyatia macho nuru.*

Ayubu 29:3- *Hapo taa yake ilipomulika juu yangu kichwani, Nami nilitembea gizani kwa njia ya mwanga wake.*

Kwa kutilia maanani Maandiko yote hapo juu, tunaweza kuhitimisha ifuatavyo:-

Roho ya Mungu huwasiliana na roho ya mwanadamu. Mungu aliwasiliana na Adamu wakati wa jua kupunga au Ruach-roho wa siku. Roho yako ndipo mahali pa mapokezi ya vitu vya kiroho au vitu vya Roho. Maneno ambayo Mungu ananena ni roho na ni uzima. Intelijensia ya kiroho ni utendaji wa nia ya roho na siyo nia ya nafsi. Nia ya nafsi isiyofanywa kuwa mpya ambayo iko nje ya kupatanishwa na roho iliyofanywa upya, inashindwa kutambua vitu vya kiroho. Nia ya nafsi ni lazima ifikishwe kwenye ulinganifu na nia ya roho.

Lango au kufafanuliwa kwa Neno huleta nuru na uelewa kwa roho zetu. Neno hili, yaani amri za Mungu hufumbua macho na kuleta mwangaza kwa vipindi vifupi vya kila siku. Taa hii ya BWANA pia ndiyo roho ya mwanadamu. Kitu ambacho mwanadamu anakitaka ni Mungu kuangazia roho yake. Mungu anafanya hivyo kwa kulituma Neno lake kwako kupitia watu anaowatuma na kuwaweka katika maisha yako kama wababa wa kiroho. Huwa wananena Neno, wanafasiri siri zake, wanafunua maana yake na hivyokutoa mlango wa kuingia katika mapenzi na njia za Mungu kwa ajili yako. Taa hii-ni roho iliyong'arishwa kwa neno lazima iwe juu ya kichwa chako, yaani juu na kuingia katika nia ya nafsi ili kushawishi na kurekebisha fahamu zetu, mitazamo, maamuzi na tabia.

Lakini pia Neno HUANGAZA njia zetu, mwelekeo wa muda, mrefu, Funzo au fundisho ndiyo nuru kwa nuru hii tunaweza kutembea kupitia gizani.

- **Kushaukia kanuni za Neno ni kupata njia ya kuzirithi.**

Zaburi 119:111-Shuhuda zako nimezifanya urithi wa milele, maana ndizo chanagamko la moyo wangu.

Urithi wako wote katika Mungu, umefungiwa ndani ya Neno Lake.

Mdo 20:32-Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa.

- **Kushaukia katika Neno kutasababisha kutokea kwa hali ambayo ndani yake kutakuwa na hali ya kutawaliwa katika mawazo na tafakari yako**

Zab 119:97- Sheria yako naipenda mno ajabu , Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.

- **Kushaukia Neno Lake kunashuhudiwa kwa kuingizwa ndani ya maisha Yote ya mtu na hili hutoa uthitbitiskwamba wewe umekuwa kiumbe kipya kufuatia Asili ya Mungu.**

Yeremia 15:16- Maneno yako yalionekana , nami nikayala , na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu, maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana Mungu wa majeshi.

“Jina” hapa linazungumzia ‘asili’

BBE:Lakini kwangu mimi neno lako ni shangwe kuufanya moyo wangu ufurahi, kwa sababu nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana Mungu wa majeshi.

- **Kuwa na shauku katika Neno ni utoshelevu halisi na wenye ujuzi wa kufurahikia.**

Zab 19:10- ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali.

Ezekieli 3:1-3

1. *Akaniambia, Mwanadamu, kula uonacho, kula gombo hili , kisha enenda ukaseme na wana wa Israeli*
2. *Basi nikafunua kinywa changu, naye akanilisha lile gombo.*
3. *Akaniambia, Mwanadamu, lisha tumbo lako, ulijaze tumbo lako kwa hili gombo nikupalo, Ndipo nikalila, nalo kinywani mwangu lilikuwa tamu, kama utamu wa asali.*

Neno linaweza kuwa tamu kwa ladha yake lakini mchakato wa kuliingiza ndani na kuruhusu utu ufanane nalo kabisa, kwa kulifanya liwe sehemu muhimu ya jinsi wewe ulivyo ni mchungu.

Hili linahitaji utii kwa kadri unavyopitia mchakato wa kulitii Neno la Mungu.

Ufunuo 10:9-10

9. *Nikamwendea malaika Yule nikamwambia kwamba anipe kile kitabu kidogo. Akaniambia, kitwae, ukile, nacho kitakutia uchungu tumboni mwako, Bali katika kinywa chako kitakuwa kitamu kama asali.*
10. *Nikakitwaa kile kitabu kidogo katika mkono wa malaika Yule, nikakila, nacho kikawa kitamu kama asali kinywani mwangu, na nilipokwisha kukila tumbo langu likatiwa uchungu.*

Ufunuo na ukweli vinaweza vikawa vinafurahisha mdomoni – vina hali ya kuvutia. Tunavutiwa navyo. Lakini inavyofikia wakati wa kutendea kazi vinaweza vikawa ni ujuzi wenye uchungu katika kuufisha mwili na mapenzi yako katika kutafuta kumpendeza Mungu.

- Furahia KUYATENDA mapenzi YAKE kwa sababu umelitunza Neno na mapenzi Yake kama ndiyo furaha iliyomo ndani ya moyo wako.

Andika Neno lake juu ya moyo wako.

Yeremia 31:33- *Basi agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israel, baada ya siku zile asema BWANA; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.*

Zab. 37:31- *Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake, Hatua zake hazitelezi*

2Kor. 3:1-3: *Je! Tunaanza tena kujisifu wenyewe au tunahitaji Kama wengine, barua zenye sifa kuja kwenu, au kutoka kwenu? Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote, mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai, si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.*

Zaburi 40:7-8

7. *Ndipo niliposema, Tazama nimekuja, [katika gombo la chuo nimeandikwa]*
8. *Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu, Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.*

Mapenzi ya Mungu ndani ya maisha ya kila mmoja wetu yamo ndani ya Neno Lake-“Katika gombo la chuo nimeandikiwa.” Kwa kadri tunavyolipenda Neno Lake na kutunza sheria na maagizo Yake ndani ya mioyo yetu, kutatokea kuwepo na KUFURAHIA katika kuyahitaji makusudi na dhamira Yake.

Pia Kama vile Yesu alivyogundua maandiko ya kiunabii yaliyomhusu Yeye katika Neno la Mungu-sisi pia- tutapata uthibitisho wa maelekezo mahususi yanayohusu njia mbalimbali za utii ambazo Mungu anatutaka tutembe ndani yake. Soma Luka 4 hapo chini.

Luka 4:15-22

15. *Naye alikuwa akifundisha katika masinagogi yao, akitukuzwa na watu wote.*
16. *Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake akasimama ili asome.*
17. *Akapewa chuo cha nabii Isaya akakifungua chuo, akatafuta mahai palipoandikwa,*
18. *ROHO WA BWANA YU JUU YANGU, KWA MAANA AMENITIA MAFUTA KUWAHUBIRI MASKINI HABARI NJEMA. AMENITUMA KUWATANGAZIA WAFUNGWA KUFUNGULIWA KWAO, NA VIPOFU KUPATA KUONA TENA, KUWAACHA HURU WALIOSETWA.*
19. *NA KUTANGAZA MWAKA WA BWANA ULIOKUBALIWA.*
20. *Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi, na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho.*
21. *Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu*
22. *Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake, wakasema, Huyu siye mwana wa Yusufu?*

Yohana 4:34- *Yesu akawaambia, Chakula changu, ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake.*

Yeremia 6:10:*Niseme na nani na kushuhudia, wapate kusikia Tazama sikio lao halikutahiriwa, wala hawawezi kuisikiliza tazama, neno la BWANA limekuwa matukano kwako, halifurahii.*

KAMWE USIPOTEZE UPENDO WAKO KWA NENO LA MUNGU.

Zaburi 119:47-48

47. *Nami nitajifurahisha Sana kwa maagizo yako, Ambayo nimeyapenda.*

48. *Na mikono yangu nitayainulia maagizo yako, niliyoyapenda, Nami nitazitafakari amri zako.*

Zab 119:96-97

96. *Nimeona ukamilifu wote kuwa na mwisho, Bali giza lako ni pana mno.*

97. *Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa,*

Zab 119:127-131

127. *Ndiyo maana nimeyapenda maagizo yako, kuliko dhahabu naam, dhahabu iliyo safi*

128. *Maana nayaona mausia yako yote kuwa ya adili, kila njia ya uongo naichukia.*

129. *Shuhuda zako ni za ajabu, Ndiyo maana roho yangu imezishika.*

130. *Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga.*

131. *Nalifunua kinywa changu nikatweta, Maana naliyatamani maagizo yako.*

Zab 119:159-160

159. *Uangalie niyapendayo mausia yako, Ee Bwana, unihuishe sawa sawa na fadhili zako.*

160. *Jumla ya neno lako ni kweli, Na kila hukumu ya haki yako ni ya milele.*

Hebu sasa tuhitimisha kwa kumnukuu Derek Prince

---- ni vigumu kukadiria kupita kiasi , au kusisitiza kupita kiasi ule umuhimu wa nafasi ya Neno la Mungu katika maisha ya Mkristo aaminiye .

Niruhusu niwasilishe kweli hizi moja kwa moja na kwa njia binafsi: Kulishika Neno la Mungu ndiyo sura yenye heshima ya hali ya juu kabisa inayo tutofautisha wewe kutoka ulimwenguni ili uwe mwanafunzi wa Kristo, Huo ndio mtihani wa upendo wako kwa Mungu , Ndicho kinachosababisha upendo wa Mungu na upendeleo Wake kukuelekea wewe. Ndiyo njia ambayo Mungu Baba na Mungu Mwana watakuja maishani mwako na kufanya makao pamoja nawe [Yoh 14:23]

Hebu niyaweke kwako kwa namna hii: Msimamo wako kwa Neno la Mungu ndio msimamo wako kumwelekea Mungu mwenyewe. Huwezi kumpenda, Mungu zaidi ya unavyolipenda Neno lake. Huwezi kumpa heshima Mungu kuliko unavyoliheshimu Neno Lake. Huweza ukatenga nafasi kubwa zaidi kwa ajili ya Mungu katika moyo wako na katika maisha kuliko unavyo fanya hivyo kwa ajili ya Neno Lake.

Unataka kujua Mungu ana maanisha nini kwako? Ni rahisi tu!

Unaweza kujua kwa kujiuliza wewe mwenyewe swali hili: Ni kwa kiasi gani Neno la Mungu linakuwa na maana katika maisha yako? Jibu la swali la pili ndilo pia jibu la swali la kwanza. Mungu anamaanisha mengi kwako Kama Neno Lake linavyo maanisha kwako. Ni kwa kiasi hicho tu, hakuna zaidi.

[Chanzo: Prince D [1986] Founation Seris- Volume one, Thomas Nelson Publishers; page 27-28].

**MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA
KIKUNDI.**

1. Upendo wako Kwa Mungu unajulikanaje au unapimwaje?
2. Tilia maanani namna upendo na shauku yako kwa Neno la Mungu unavyowezesha utii wako kwa Neno.
3. Ni kwa namna gani tunaweza kutambua nyakati za mateso kwa kuzingatia upendo na uelewa wetu kwa Neno au ahadi za Mungu kwetu?
4. Ni nini baadhi ya visababishi vya Baraka vinavyo ambatana na kulipenda Neno la Mungu?
5. Yesu aligundua sura za mapenzi ya Baba Yake Kwa ajili ya uzima Wake kupitia kusoma na kujifunza Neno la Mungu. Fafanua maelezo haya kwa kutumia maandiko.

Lengo: Kumpenda Mungu kunaakisiwa kwa Upendo wa Neno lake.

Shughuli muhimu ya nyumba ya Mungu ni Neno la Mungu- soma (**Isaya 2: 1-5, Mika 4: 1-4**). Upendo wa kwanza wa mtu kibibilia ni Upendo kwa Neno la Mungu (Tutaonesha hili katika kipindi kitakachofuata).

Amri kuu zaidi iliyoagizwa na Bwana ni Kumpenda Mungu na kupendana sisi kwa sisi.

Mathayo 22:36-39

36. *Mwalimu, katika torati ni amri gani iliyo kuu?*

37. *Akamwambia, MPENDE BWANA MUNGU KWA MOYO WAKO WOTE NA KWA ROHO YAKO YOTE NA KWA AKILI ZAKO ZOTE.*

38. *Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.*

39. *Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO.*

Yohana 13:34: *“Amri mpya nawapa, Mpendane kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.*

Nukuu ya ziada: Ile amri ya kupendana inaendelezwa kutokana na maneno “kama nafsi yako” (**Mathayo 22:39**) hadi “kama nilivyowapenda ninyi” (**Yohana 13:34**)

Upendo kwa Mungu unashuhudiwa kwa msimamo wako kulielekea Neno lake, Mahsusi kiwango chako cha utii kwa neno lake. Yesu alisema kwamba, Kama tunampenda yeye tunalazimika kuzitenda amri zake. (**Yohana 14:15:** “ *Mkinipenda, mtazishika amri zangu*”)

Kiwango ambacho wewe unakuwa mtii kwa amri za Mungu ni kwa kiwango hicho hicho unapaswa kumpenda yeye. Hakuna kipimo kingine ambacho kinaweza kutumiwa kupima Upendo wako Kwa Mungu, isipokuwa ni kwa kiasi gani unazitii amri zake zilizoko katika Neno Lake.

Upendo wa Mungu umekamilishwa kwa Neno lake kwa wewe kulishika. Masuala ya kumpenda Mungu kwa mkono mmoja, na kulishika Neno lake kwa mkono wa pili siyo masuala mawili tofauti, isipokuwa moja hutoa ushahidi kwa jingine.

1Yohana 2:4-5

4. *Yeye asemaye nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo wala kweli haimo ndani mwake.*

5. *Lakini yeye ashikaye Neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.*

Katika Yohana 14, Yesu anaonesha kwamba Ulimwengu hautamwona YEYE ila sisi tulio wanafunzi wake. Kwa namna gani? Yeye na Baba watafanya wenyewe wajulikane kupitia Neno lake kwa wale wanaolitii.

Yohana 14:19-23

19. *Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu mimi ni hai na ninyi mtakuwa hai.*
20. *Siku ile ninyi mtatambua yakua mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.*
21. *Yeye aliye Na amri zangu Na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*
22. *Yuda (siye Iskariote), akamwambia, Bwana, Imekuwaje kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu?*
23. *Yesu akajibu akamwambia, Mtu akinipenda atalishika Neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.*

Kuwa” na “kuzishika” amri za Mungu kutakupa wewe nafasi za kupokea dhihirisho za Upendo wa Baba na mwana (Mst. 21), ikiwa ni pamoja na kujua siri fulani za kujifunua kwa Mungu mwenyewe kwako.

Kwa kushindwa kumpenda Mungu kwa kuto kupenda na kulitii Neno lake kunauweka msimamo wako katika hatari kubwa kuhusu ndugu zako wa kiume na wa kike katika mwili wa Kristo.

1Yohana 5:2-3

2. *Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake.*
3. *Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.*

Mstari wa 2 unatoa ushauri (Rai) kwamba mtu hataupenda mwili wa Kristo – Familia ya Mungu- kaka zako na dada zako ndani ya Kristo wakati anaonesha kutokuwa na upendo kwa ajili ya Mungu kwa kutolitii Neno lake. Kumpenda Mungu na Neno lake sio jambo binafsi au la siri peke yake. Wakati uasi kwa amri zake ushahidi wa kutokuwa na upendo kwa Mungu, na uasi huu unaathiri vibaya jamii ya watakatifu ambayo wewe unahusika(dhambi ya Akani iliisababishia Israel athari hasa katika mpango wao wa kivita- (soma *Joshua 7*).

Upendo kwa Mungu haufafanuliwi kama ni hisia za misisimko chanya ya kimapenzi kumwelekea Mungu. Inawezekana na likawemo ndani, lakini huu si ushahidi wa kugombewa wa upendo wako kwa Mungu. Upendo kwa Mungu unapimwa tu kwa njia moja, nayo ni kile kiwango chako cha utii kwa Neno lake.

2Yohana 1:6 *Na huu ndio upendo: tuenende kwa kuzifuata amri zake. Hii ndiyo ile amri, kama mlivyosikia tangu mwanzo kwamba mwenende katika hiyo.*

Upendo siyo katika KU-UZUNGUMZIA isipokuwa ni katika KU-UISHI.

Unaweza kusema unampenda Mungu lakini ukawa huoneshi huo Upendo na wala kutoa kipaumbele kwa Neno lake kwa kulisikiliza, kulisoma, kujifunza, kulitafakari na zaidi sana KULITII. Kibibilia humpendi Mungu kabisa.

Na iwe kwetu sote tuwe na ustadi (uhodari) wa kumpenda Mungu zaidi kwa kushawishika KULITII Neno lake zaidi kwa matendo ya hiari.

KUWA NA SHAUKU KALI NDANI NA KWA NENO LA MUNGU.

SHAUKU= chephets maana yake ni *tamani, furaha, kuwa na mwelekeo kwa kitu au kuwa na hamu.*

KULITII Neno la Mungu ni lazima kuwe na SHAUKU ndani ya mtu na pia AWE NA HISIA KALI kuhusu Neno lake. Katika kuwa na SHAUKU ya Neno lake, mtu anapaswa kuona uthamani wa Neno na kulipa kipaumbele cha hali ya juu. Kile ambacho unakiheshimu, Utakipenda na kile ambacho unakipenda, utakitii.

BARAKA ZA KUWA NA SHAUKU NDANI NA KULIPENDA NENO LA MUNGU.

“SHAUKU” huwezesha kuwa na “UTII”

***Zaburi 119:35-**Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako, Kwa maana nimependezwa nayo.*

***Ayubu 23:12-** Sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake; Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu,*

Angalia sababu iliyomfanya Ayubu amtii Mungu kwa kutorudi nyuma na kuiacha amri ya midomo ya Mungu. Ilikwa ni kwasababu alikuwa ameamua kuyapa uthamani maneno ya kinywa cha Mungu, zaidi sana kuliko chakula muhimu cha mwili. Heshima yako ya hali ya juu kwa maneno yake, itakuwezesha wewe kuwa na utii kwa ajili yake.

Amri za Mungu siyo nzito kwa mtu anayempenda Yeye na maneno Yake.

***IYohana 5:3-** Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.*

Kumbukumbu la Torati 30:8-20

8. *Nawe utarudi, uitii sauti ya Bwana, na kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo.*
9. *Na Bwana, Mungu wako, atakufanya uwe na wingi wa uheri katika kazi yote ya mkono wako, katika uzao wa tumbo lako, na katika uzao wa ng'ombe wako, na katika uzao wa nchi yako; kwa kuwa Bwana atafurahi tena juu yako kwa wema, kama alivyofurahi juu ya baba zako;*
10. *ukiwa utaifuata sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa kuyashika maagizo yake, na amri zake zilizoandikwa katika chuo hiki cha torati; ukimwelekea Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote.*
11. *Kwa maana maagizo haya nikuagizayo leo, si mazito mno kwako, wala si mbali.*
12. *Si mbinguni, hata useme, Ni nani atakayetupandia mbinguni akatuletee, aje atuambie tusikie, tupate kuyafanya?*
13. *Wala si ng'ambo ya pili ya bahari, hata useme, Ni nani atakayetuvukia bahari, akatuletee, aje atuambie, tusikie, tupate kuyafanya?*
14. *Lakini neno li karibu nawe Sana, li katika kinywa chako Na moyo wako, upate kulifanya.*
15. *Angalia, nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya;*
16. *wa hivi nikuagizavyo leo kumpenda Bwana, Mungu wako, kuenenda katika njia zake, na kushika maagizo yake, na amri zake, na hukumu zake, upate kuwa hai na kuongezeka; Bwana, Mungu wako, apate kukubarikia katika nchi uingiayo kuimiliki.*
17. *Lakini moyo wako ukikengeuka, usipotaka kusikiza, lakini ukavutwa kando kwenda kuabudu miungu mingine, na kuitumikia;*

18. *Nawahubiri hivi leo hakika mtaangamia; hamtazifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi, uivukiayo Yordani, uingie kuimiliki.*
19. *Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako;*
20. *kumpenda Bwana, Mungu wako, ku*

Chunguza namna haya yafuatayo yanavyohusiana: (mst. 20) kumpenda Mungu- kuitii sauti yake, kushikamana naye, kisha yanafuata maelezo yenye nguvu: Huo ndio Uzima wako.

- Baraka huambatana na utii-soma mistari ya 9,10 na 16 hapo juu.
- Laana huambatana na kutotii (uasi)-soma mistari ya 15,17 na 18 hapo juu.

Kuwa na shauku katika Neno la Mungu kunamwezesha mtu kuvumilia Mateso.

Uwapo katikati ya shida/taabu siku zote jiulize;-

1. **Jaribu hili ni matokeo ya kuasi kwangu?** Jibu likiwa ndiyo, tubu na tii. Kuna nyakati ambazo matokeo halisi ya kutotii kwetu yanaweza kutumiwa na Mungu kutupeleka mahali pa kutufanya tuamue na kusimama imara zaidi katika utii wa Neno lake.
***Zaburi 119:67-** Kabla sijateswa Mimi nalipotea, Lakini sasa nimelitii neno lako.*
2. **Jaribu hili ni la kiulimwengu lililoanzishwa na Mungu katika kutafuta kukamilisha mwelekeo mkakati wa mapenzi yake kwaajili ya taifa au jamii mahsusii ya watu?** (kama vile Eliya alipokuwa katikati ya njaa kwa miaka mitatu).
3. **Je, jaribu hili ni la binafsi lililoruhusiwa ki-uungu na Mungu kwasababu ya kutukuka kuruhusiwa Ki-Uungu na Mungu ili kukamilisha mambo fulani yaliyo ndani ya maisha yangu?**, Mungu anaweza kuwa anataka kukamilisha utii wako kupitia jaribu. Ingawa Yesu alikuwa ni mwana wa Mungu, alijifunza utii kupitia yale mambo yaliyomtesa. (soma Waebrania 5:8)

***Zaburi 119:71-**Ilikuwa vema kwangu kuwa naliteswa, Nipate kujifunza amri zako.*

Katika nyakati hizi za taabu na mateso, mtu hapaswi kuzitilia shaka ahadi za Mungu ambazo zinaambatana na utii. Kwasababu hiyo, mtu anaweza kupoteza azma na mapenzi yakuendelea kumtii Mungu.

Ayubu 6:10

***NASB:** “Lakini bado ningali ninafarijiwa, na ninafarijika katika maumivu yasiyoniacha kwa kuwa sikuyakana maneno yake Matakatifu.*

***CEV:** Kisha nitafarijiwa, nikijua kwamba katika maumivu yangu yote kamwe sikuacha kumtii Mungu.*

***ERV:** Kisha nitafarijiwa kwa kitu hiki kimoja, Ingawa kwa kupitia maumivu haya yote sijakata tama kamwe kuzitii amri zake Takatifu.*

***NirV:** Kisha nitaendelea kuwa na kitu kimoja cha kunifariji, Itakuwa kwamba sijawahi kusema hapanakwa amri za Mtakatifu. Hilo litanipa faraja pamoja na maumivu ambayo hayana mwisho.*

Iwe ni kwa sababu ya aina yoyote unateswa katika majaribu na magumu anuwai/mbalimbali, usipoteze shauku yako kwa ajili ya Neno la Mungu.

Zaburi 119:92- *Kama sheria yako isingalikuwa furaha yangu, Hapo ningalipoteka katika taabu zangu.*

Zaburi 119: 49-50 *Likumbuke neno ulilomwambia mtumishi wako, Kwa sababu umenitumainisha. Hii ndiyo faraja yangu katika taabu yangu, Ya kwamba ahadi yako imenihuiisha.*

UKUMBUSHO:

Lifanyie mazoezi somo la 3 katika mfuatano huu wa mafunzo. Kila neno au ahadi ambayo mtu atafunuliwa, itajaribiwa katika maisha yako. Utapitia majaribu mengi mpaka lile Neno lifanyike kuwa mwili/ halisia katika maisha yako. Yusufu alikuwa mhanga wa majaribu ya aina nyingi kutoka kwa Mungu; na yote haya yalikuwa ni kwaajili ya utayari ya kukamilisha hatima ya wito wake.

Elewa kwamba jaribu lako ni kwaajili ya Neno unalosikia.

Zaburi 105:19 *Hata wakati wa kuwadia neno lake, Ahadi ya Bwana ilimjaribu.*

Ufunuo 1:9 *Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.*

Mwiba wa Paulo katika mwili? Chochote ambacho hiki kilikuwa, kiliruhusiwa na Mungu ili kumfanya awe mnyenyekevu kwa sababu ya wingi wa mafunuo aliyopewa yeye.

2Wakorinto 12: 7-10

- 7. Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi.*
- 8. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke.*
- 9. Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.*
- 10. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.*

SHAUKU ndani ya NENO na kwa NURU yake unaweza KUENENDA hata katika nyakati za GIZA.

Zaburi 18:28 *Kwa kuwa Wewe unaiwasha taa yangu; Bwana Mungu wangu aniangazia giza langu.*

Mithali 20:27 *Pumzi ya mwanadamu ni taa ya Bwana; Hupeleleza yote yaliyomo ndani yake.*

Zaburi 119:105 *Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.*

Mithali 6:23 *Maana maagizo hayo ni taa, na sheria hiyo ni nuru, Na maonyo ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima.*

Zaburi 19:8 *Maagizo ya Bwana ni ya adili, Huufurahisha moyo. Amri ya Bwana ni safi, Huyatia macho nuru.*

Ayubu 29:3 Hapo taa yake ilipomulika juu yangu kichwani, Nami nilitembea gizani kwa njia ya mwanga wake;

Kwa kutilia maanani maandiko yote hapo juu, tunaweza kuhitimisha yafuatayo:-

Roho wa Mungu huwasiliana na roho ya mwanadamu. Mungu aliwasiliana na Adamu wakati wa jua kupunga au Ruachi – Roho wa siku. Roho yako ndipo mahali pa mapokezi ya vitu vya kiroho au vitu vya Roho. Maneno anayonena Mungu ni Roho na ni Uzima. Uwezo wa akili wa kiroho ni utendaji wa ile nia ya Roho na siyo nia ya nafsi. Nia ya nafsi ambayo haijafanywa upya iko nje ya ku-patanishwa na Roho iliyofanywa upya, kwani inashindwa kutambua vitu vya Kiroho. Nia ya nafsi ni lazima ipelekwe kwenye kushika manishwa na nia ya roho.

Lile ingilio au kule kufunuliwa kwa Neno kunaleta nuru na uelewa kwa roho zetu. Neno hili, yaani “amri za Mungu” hufumbua macho na kutuletea mng’ao kila siku kwa vipindi vifupi vifupi vya hatua zetu. Taa hii ya BWANA pia ndiyo roho ya mwanadamu. Kitu anachokihitaji mwanadamu ni Mungu kuipa Nuru roho yake. Mungu anafanya hivyo kwa kulitunza Neno lake kwako kupitia kwa wale anaowatuma na kuwaweka katika maisha yako kama wababa wa kiroho. Wanalinena Neno, kufasiri siri zake, kufunua maana yake na hivyo kutoa lango la kuingia katika mapenzi ya Mungu na njia zake kwa ajili yako. Taa hii – Roho iliyonururishwa kwa Neno ni lazima iwe yenye kutawala fikra, mitazamo, maamuzi na tabia zetu.

Lakini pia Neno HUANGAZIA njia yetu- katika kuwa na mwelekeo wa muda mrefu. Funzo au fundisho ni Nuru. Kwa nuru hii tunaweza hata kuenenda penye giza.

Zaburi 43:3 Niletewe nuru yako Na kweli yako ziniongoze, Zinifikishe kwenye mlima wako mtakatifu hata maskani yako.

Mafanikio na urithi humjia yeye ambaye ana shauku katika Neno.

Zaburi 1:1-3

- 1. Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.*
- 2. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*
- 3. Naye atakuwa Kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzao matunda yake Kwa majira yake, Wala jani Lake Halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.*

Katika mstari wa kwanza, istilahi “KWENDA”, “SIMAMA” na “KETI” zinaelezea maisha yote ya mtu. Mtu aliyebarikiwa ni ambaye hatendi baadhi ya mambo fulani, (mst. wa 1) kwa sababu tu anafanya jambo jingine kwa kulishaukia Neno la Mungu.

Uwezo wake wa kushinda dhidi ya mashauri maovu, mienendo miovu na mabaraza ya wenye mizaha unawezeshwa kwa masharti na mtazamo wa shauku yake ambayo vimo katika NENO LA MUNGU. Kile ambacho unakishaukia kinaweza kuwa ndio uwezo wako wa kushinda kilicho andaliwa kukushinda wewe.

“Shauku” inashuhudiwa kwa zingatiao thabiti. Mtu ambaye ana shauku sana katika Neno anafananishwa na mti uliopandwa kando ya vijito vya maji. Mfanano huu ulikusudiwa kueleza athari/ matokeo yenye nguvu na faida za kuwa na shauku katika Neno.

Faida ni za aina tatu:-

1. Kuwa na matunda- huhusika na majira yoyote katika Mungu.
2. Hakuna utasa- Jani halinyauki. Majani yananyauka katika kipindi cha kiangazi au wakati jani linapo dhoofika. Jani katika muktadha huu ni alama ya dhiki katikati ya mafanikio. Anaishi akiwa sugu lakini kwa nje akiwa hana kitu (hasi) katika mazingira ya kawaida. Hakwepi matatizo yaliyopo pale alipowekwa, lakini anaimarishwa na Mungu katika kuyapitia hayo.
3. Na kila alitendalo litafanikiwa.

- ❖ Kuwa na shauku katika neno lake ni udhihirisho wa wewe kuwa na HOFU na Unyenyekevu kwa Mungu.

Kumhofu Mungu kwako kunashuhudiwa kwa kuwa na shauku katika Neno lake.

Zaburi 112:1 Haleluya. Heri mtu yule amchaye Bwana, Apendezwaye sana na maagizo yake.

- ❖ Kuwa na shauku katika Neno lake kama ambavyo ungefanya ikiwa ungekuwa na njia ya kupata utajiri wa kifedha usio pimika.

Zaburi 119:14 Nimeifurahia njia ya shuhuda zako Kana kwamba ni mali mengi.

Zaburi 119:162 Naifurahia ahadi yako, Kama apataye mateka mengi.

Zaburi 19:10 Ni za kutamanika kuliko dhahabu, Kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali Kuliko sega la asali,

Zaburi 119:72 Sheria ya kinywa chako Ni njema kwangu, Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.

- ❖ Kwa kuwa na shauku katika Neno Lake, kunakuhakikishia wewe kutosahau. Neno lake linasahaulika ikiwa huziungi mkono kanuni zake katika maisha yako, kama ndizo kanuni unazopaswa kuzifuata katika kuishi kwako.

Zaburi 119:16 Nitajifurahisha sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako.

- ❖ Kuwa na shauku katika kanuni za Neno hufungua mlango wa kuzirithi.

Zaburi 119:111-Shuhuda zako nimezifanya urithi wa milele, Maana ndizo changamko la moyo wangu.

Urithi wako kamili katika Mungu umefungiwa katika Neno Lake.

Matendo 20:32 Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo la Kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa.

- ❖ Kuwa na shauku katika Neno kwa asili kunasababisha ndani yake kuwe na kutawala mawazo na kutafakari kwako.

Zaburi 119:97 Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.

Zaburi 1:2 *Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*

- ❖ Kuwa na shauku katika Neno lake kunashuhudiwa kuwa Neno hilo limekuwa mfanano kwa maisha yote ya mtu na hili hutoa uthibitsho kwamba unapata asili kutokana na asili ya Mungu.

Yeremia 15:16 *Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana, Mungu majeshi.*

“Jina” hapa linazungumzia asili.

BBE: Lakini kwangu mimi Neno lako ni furaha, likiufanya moyo wangu ufurahi, kwa maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana Mungu wa majeshi.

- ❖ Kuwa na shauku katika neno ni Utoshelevu kamili na ni ujuzi wa kufurahisha.

Zaburi 19:10 *Ni za kutamanika kuliko dhahabu, Kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, Kuliko sega la asali.*

Ezekiel 3 :1-3

1. *Akaniambia, Mwanadamu, kula uonacho; kula gombo hili, kisha enenda ukaseme na wana wa Israeli.*
2. *Basi nikafunua kinywa changu, naye akanilisha lile gombo.*
3. *Akaniambia, Mwanadamu, lisha tumbo lako, ulijaze tumbo lako kwa hili gombo nikupalo. Ndipo nikalila, nalo kinywani mwangu lilikuwa tamu, kama utamu wa asali.*

Neno linaweza kuwa tamu kwa ladha yak, lakini ni mchakato mgumu kuliingiza katika vitendo na kulifanya lifanane kikamilifu na utu wa binadamu, na kulifanya liwe ndiyo sehemu muhimu ya jinsi wewe ulivyo. **Hili linahitaji utiifu kwa kadri unavyopitia katika mchakato huu wa kulitii Neno la Mungu.**

Ufunuo 10:9-10

9. *Nikamwendea malaika yule nikamwambia kwamba anipe kile kitabu kidogo. Akaniambia, Kitwae, ukile, nacho kitakutia uchungu tumboni mwako, bali katika kinywa chako kitakuwa kitamu kama asali.*
10. *Nikakitwaa kile kitabu kidogo katika mkono wa malaika yule, nikakila; nacho kikawa kitamu Kama asali kinywani mwangu, na nilipokwisha kukila tumbo langu likatiwa uchungu.*

Ufunuo na ukweli vinaweza kufurahisha mdomoni. Vinavutia na tunavutwa kuviendea. Lakini inapofikia wakati wa kuvitendea kazi, vinaweza kuwa ujuzi mchungu kwa kadri unavyoendelea kuufisha mwili wako na matakwa yako katika kutaka kumpendeza Mungu.

- ❖ Shauku ya KUTENDA mapenzi yake kwa sababu umelitunza NENO LAKE na mapenzi yake kama ndiyo shauku ndani ya moyo wako. Andika Neno lake juu ya Moyo wako.

Yeremia 31:33 *Bali agano hili ndilo nitakalofanya Na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani Yao, Na katika mioyo Yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.*

Zaburi 37:31 *Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake. Hatua zake hazitelezi.*

2Wakorinto 3:1-3

Je! Tunaanza tena kujisifu wenyewe? Au tunahitaji, kama wengine, barua zenye sifa kuja kwenu, au kutoka kwenu? Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, Inajulikana na kusomwa na watu wote; mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai;/katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.

Zaburi 40:7-8

7. *Ndipo niliposema, Tazama nimekuja, (Katika gombo la chuo nimeandikiwa,)*
8. *Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.*

Mapenzi ya Mungu ndani ya maisha ya kila mmoja wetu yamo ndani ya Neno lake-“katika gombo la chuo nimeandikwa” kwa kadri tunavyolipenda neno lake na kuzitunza sheria na amri zake ndani ya mioyo yetu, Kutatokezea SHAUKU katika kutii makusudi na malengo yake.

Pia kama vile Yesu alivyogundua maandiko ya kinabii yaliyomhusu yeye katika Neno la Mungu, sisi pia tunapaswa kupata uthibitisho wa maelekezo mahsusni ya njia mbalimbali za utii ambazo Mungu anatutaka tuenende katika hizo (soma Luka 4 hapo chini).

LUKA 4:15-22

15. *Naye alikuwa akifundisha katika masinagogi yao, akitukuzwa na watu wote.*
16. *Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.*
17. *Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa,*
18. *Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,*
19. *Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.*
20. *Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho.*
21. *Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.*
22. *Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake, wakasema, Huyu siye mwana wa Yusufu?*

Yohana 4:34 *Yesu akawaambia, Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, Nikaimalize kazi yake.*

KAMWE USIUPOTEZE UPENDO WAKO KWA NENO LA MUNGU

Zaburi 119:47-48

47. *Nami nitajifurahisha Sana Kwa maagizo yako, Ambayo nimeyapenda.*
48. *Na mikono yangu nitayainulia maagizo yako niliyoyapenda, Nami nitazitafakari amri zako.*

Zaburi 119:127-131

127. *Ndiyo maana nimeyapenda maagizo yako, Kuliko dhahabu, naam, dhahabu iliyo safi.*
128. *Maana nayaona mausia yako yote kuwa ya adili, Kila njia ya uongo naichukia.*
129. *Shuhuda zako ni za ajabu, Ndiyo maana roho yangu imezishika.*

130. *Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga.*

131. *Nalifunua kinywa changu nikatweta, Maana naliyatamani maagizo yako.*

Zaburi 119:159-160

159. *Uangalie niyapendavyo mausia yako, Ee Bwana, unihuishe sawasawa na fadhili zako.*

160. *Jumla ya neno lako ni kweli, Na kila hukumu ya haki yako ni ya milele.*

Tuhitimishe kwa kumnukuu Derek Prince

..... ---- ni vigumu kukadiria kupita kiasi , au kusisitiza kupita kiasi ule umuhimu wa nafasi ya Neno la Mungu katika maisha ya Mkristo aaminiye .

Niruhusu niwasilishe kweli hizi moja kwa moja na kwa njia binafsi: Kulishika Neno la Mungu ndiyo sura yenye heshima ya hali ya juu kabisa inayo tutofautisha wewe kutoka ulimwenguni ili uwe mwanafunzi wa Kristo, Huo ndio mtihani wa upendo wako kwa Mungu , Ndicho kinachosababisha upendo wa Mungu na upendeleo Wake kukuelekea wewe. Ndiyo njia ambayo Mungu Baba na Mungu Mwana watakuja maishani mwako na kufanya makao pamoja nawe [Yoh 14:23]

Hebu niyaweke kwako kwa namna hii: Msimamo wako kwa Neno la Mungu ndio msimamo wako kumwelekea Mungu mwenyewe. Huwezi kumpenda, Mungu zaidi ya unavyolipenda Neno lake. Huwezi kumpa heshima Mungu kuliko unavyoliheshimu Neno Lake. Huweza ukatenga nafasi kubwa zaidi kwa ajili ya Mungu katika moyo wako na katika maisha kuliko unavyo fanya hivyo kwa ajili ya Neno Lake.

Unataka kujua Mungu ana maanisha nini kwako? Ni rahisi tu!

Unaweza kujua kwa kujiuliza wewe mwenyewe swali hili: Ni kwa kiasi gani Neno la Mungu linakuwa na maana katika maisha yako? Jibu la swali la pili ndilo pia jibu la swali la kwanza. Mungu anamaanisha mengi kwako Kama Neno Lake linavyo maanisha kwako. Ni kwa kiasi hicho tu, hakuna zaidi.

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA REJEA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Ni kwa namna gani Upendo wako kwa Mungu unaweza kutambuliwa na kupimwa?
2. Zingatia namna shauku yako kali katika Neno la Mungu inavyo kuwezesha kulitii Neno la Mungu.
3. Ni kwa namna gani tunaweza kutambua nyakati za mateso huku tukizingatia upendo na uelewa wetu wa Neno la Mungu au ahadi zake kwetu?
4. Ni vitu gani baadhi vinavyofuatana na Baraka pamoja na kushaukia Neno la Mungu?
5. Yesu aligundua vipengele vya mapenzi ya Baba yake kwa maisha yake kupitia kusoma na kujifunza Neno la Mungu. Fafanua sentensi hii kwa kutumia maandiko.

Lengo:Uchunguzi kifani kuhusu Waefeso.

Katika sehemu hii tunachunguza dhana ya kibiblia kuhusu ‘upendo wa kwanza, ambayo ndani yake tutaonesha kwamba inatupelekea kutoa kipaumbele cha hali ya juu, heshima na upendo kwa Neno la Mungu.

Hili ni pamoja na:- Msimamo wa mtu kulielekea Neno.

- Heshima na staha kwa wale wanaotuletea neno.
- Mtu mwenyewe kujiweka katika nafsi hai ya kuli sikia Neno.
- Uhusika endelevu wa mara kwa mara na kukutana na Neno.
- Utii kwa kile ulicho kwisha sikia kama ushahidi wa upendo wako kwa Mungu na Neno Lake.

Ufunuo 1:9-20

9. *Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso ya ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patimo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.*
10. *Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu.*
11. *Ikisema, haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke katika hayo makanisa saba: Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadefia, na Laodikia.*
12. *Nikageuka nione ile sauti iliyosema nami; na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu,*
13. *Na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.*
14. *Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji, na macho yake kama mwali wa moto,*
15. *Na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru, na sauti yake kama sauti ya maji mengi.*
16. *Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking’aa kwa nguvu zake.*
17. *Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, usiogope, mimi ni wa kwanza na wa mwisho,*
18. *Na aliye hai, nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.*
19. *Basi uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayo kuwa baada ya hayo.*

20. Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, ni ya vile vinara saba vya dhahabu. Zile nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba, na vile vinara saba ni makanisa saba.

SAUTI YAKE ILIKUWA UVUMI/MLIO WA MAJI MENGI.

Maji ni alama ya Neno la Mungu [soma Yoh 15:3; Efes 5:25-27; Yoh 3:5; 1Petr1:22-23; Yoh 17:17] sauti ya Bwana ili fananishwa na **MAJI MENGI**. Hili linatupeleka kwenye ukubwa wenye sehemu nyingi za kule kunena kwa Mungu au zile namna nyingi tofauti za kujidhihirisha kwa sauti yake au misisitizo tofauti ya neno lake. Ukamilifu wa ‘**SAUTI YAKE**’ inaweza kuonekana katika udhihirisho wa pamoja wa ‘**maji mengi**’. Hakuna kikundi hata kimoja mahususi/kanisa/mtandao n.k chenye uelewa wote wa ujumla wote wa kusudi lote au shauri lote la Mungu’ [soma Mdo 20:27]

Amri ya kisheria ‘**SIKIA**’ iliyotangaziwa kwa kila kanisa katika ufunuo sura ya 2 na 3 ni mahususi kwa kile anachosema Roho kwa yale makanisa [ni wingi-siyo umoja] kwa makanisa yote kwa pamoja.

Ezek 43:2. Na tazama. Huo utukufu wa Mungu wa Israel ulitokea kwa njia ya mashariki; na sauti yake ilikuwa kama mshindo wa maji mengi, nayo nchi iling’aa kwa utukufu wake.

Ufunuo 14:2a. Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu.

Zaburi 46:4. Kuna mto, vijito vyake vya ufurahisha mji wa Mungu, patakatifupa maskani yake aliye juu.

Zabur 36:8. Watashibishwa kwa unono wa nyumba yako, nawe utawanyweshwa mto wa furaha zako.

Zaburi 65:9. Umejia nchi na kustawisha, umeitajirisha sana, mto wa Mungu umejaa maji, wawaruzuku watu nafaka, maana ndiwe utengenezaye ardhi.

Hivyo kuwa kando ya vijito vya maji kunamgusia mtu ambaye kusikia kwake kumeongezeka hadi kufikia kuwa na msimamo mkali na uwezo wa kuupokea ukweli wote bila ya kuukataa mkondo wake mahususi au kanuni ya ukweli. Katika kitabu cha Zaburi 1, miti mingine inaweza kuteseka kutokana na athari za ukame kwa sababu haikupandwa kando ya vijito vingi vya kweli vya Neno la Mungu. Hali zao ni za njaa na ukame—ambazo ni sura za kutoweza kuusikia ukweli [Amosi 8:11] ‘**Angalia, siku zinakuja, asema Bwana Mungu, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula wala kiu ya kukosa maji, bali yakukosa kuyasikia maneno ya Bwana.**

Kinyume na hili, mti uliopandwa kando ya maji hatimaye unakuwa na uwezo wa ku-usikia ukamilifu wote wa Neno la Mungu. Sharti hapa ni kusikia fundisho kamili na siyo kuchagua ni kipi cha kusikia. Hili ni pamoja na kupokea na kushikilia [kukumbatia] kila Neno kutoka kwa baba yako wa kiroho katika Bwana- maneno yote sahihi na ya kujenga [2Tim 4:2” Lihubiri

neni, uwe tayari, wakati ukufaa na wakati usiokufaa; karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho].

Pembeni: Ona pia, ‘maji mengi’ katika Ezekiel 43:1-2 mahali yanapozalisha utukufu uingiao duniani; Ufunuo 14:21].

**VINARA VYA TAA SABA NI MAKANISA YALIYO JIKITA KATIKA NENO
AMBALO KWA PAMOJA YANAWAKILISHA FUNDISHO LA KITUME LISILO NA
KASORO LINALO LETA NURU- MNG’AU- UFUNUO.**

Vile vinara saba ni makanisa saba, yanayo wakilisha sehemu pana ya ndani ya mwili wa Kristo ki-ulimwengu. Kila moja lina sifa ya kuwa na vitu anwai na vinavyo tofautiana. Tarakimu [namba] saba lina ashiria ukamilifu kwa ushirika. Makanisa haya kwa pamoja kama yanavyo jieleza yanawakilisha utimilifu katika eneo ambalo kwa hilo yanatukuzwa [sifiwa]. Pia, wakati ‘kinara cha taa’ ni picha ya fundisho la kitume, haya makanisa saba kwa ujumla wake yaliwakilisha fundisho lililokuwa kamili (sahihi). Tulifundisha wakati uliopita kwamba **NENO la MUNGU** ni lazima liumbe tabia ya **NYUMBA ya MUNGU** [Isaya 2:1-5, Mika 4:1-4; **rejea somo la 9 na la 10 pia**]. Vijito vingi vya kitume kwa pamoja vinaanzisha mto wa sauti ya Mungu. Mvinyo mpya uko katika kishada cha kichala cha zabibu na siyo umewekwa katika zabibu moja maalum. Sisi tulio kanisa moja, tunayo nia ya Kristo.

Isay 65:8a: Bwana asema hivi, kama vile divai mpya ipatikanayo katika kichala, na mtu mmoja husema, usikiharibu kwa maana mna Baraka ndani yake;

Mvinyo ni picha ya Ufunuo wa Neno. Katika ile harusi ya Kana, Yesu aligeuza maji yakawa mvinyo. Kialama maji ni kiwakilishi cha Neno la Mungu katika kusafisha na katika tendo la kutakasa. Mvinyo nao una liwakilisha Neno, lakini ni katika tabia yake ya ufunuo katika kuongoa (Kutaalamisha) na kung’arishafahamu zetu. Katika unabii uliohusu Yuda ulioandikwa katika Mwanzo 49:8-12, inasemekana kwamba macho yake yangukuwa mekundu kwa mvinyo [mst 12] kuonesha kwamba matumaini yake yangufanywa kuwa mekundu kwa ufunuo kutokana na Neno la Mungu. Ufunuo na mng’ao hutusababisha sisi tu-enende tukiwa na ufahamu, uelewa, na kuwa na uhakika. Mahali pasipo na ufahamu na uelewa, ujinga na giza hutawala na hivyo kutufanya tuenende pasipokuwa na uhakika (Yoh. 12:35). Mahali penye maarifa na uelewa pana nuru inayoangaza juu ya namna tunavyoweza kuongoza maisha yetu katika giza la dunia hii. Uelewa uliokamilika kabisa na wa uhakika wa Neno la Mungu na mapenzi yake unawezekana kuwepo wakati mikondo anuwai ya kitume inapokutana katika jito moja la ukweli.

**NYOTA SABA= MALAIKA SABA= UTIMILIFU NDANI YA WABABA WA KITUME
WA KIROHO/ WAJUMBE .**

Zile nyota saba ndio wale malaika saba au wajumbe [ufun 1:20]- walio wababa wa kiroho wanao ongoza kila kanisa. Hawa huleta nuru kutoka katika Neno kwa ajili ya wale walio chini ya uangamizi wao. Ile tabia ya Neno la Mungu kama mwanga katika njia yetu na taa ya miguu yetu, inatambuliwa na kuwa tendaji wakati wababa wa kiroho wanapo unganika na neema halali ya kweli ya ubaba wa kitume, inayotoa mlango wa kuingia katika neno la Mungu. Viongozi hawa, ambao kwa kweli wanaishi kile wanachofundisha, wao wenyewe wanatumika na kuiwakilisha nuru ya Neno la Mungu kwa watu wao. Daudi alionwa na watu wake kama ni taa ya Bwana kwao.

2Samwel21:17b-*Ndipo watu wa Daudi wakamwapia,wakasema,Wewe hutatoka tena pamoja nasi kwenda vitani,usije ukaizima taa ya Israeli.*

Wababa wa kweli wa kiroho hu-wakilisha MWANGA kwa watu wao.Nuru yao ni Neno la Mungu ambalo wanafundisha na kunena.

Ufun 1:16.*Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali wenye makali kuwili ukitoka katika kinywa chake, na uso wake kama jua likang'aa kwa nguvu zake.*

Nyota hizi au wababa wa kiroho wameinuliwa katika mkono wa kuume wa Mungu.

‘**Mkono wa kuume**’ unawakilisha: Nafasi ya nguvu ya uweza na mamlaka ya kuamua.

Uwezo wenye nguvu wa kutekeleza na kufanya mapenzi ya Bwana.

Mpango au mkakati wa mapenzi ya Mungu unafanya kazi hasa kupitia vipawa na wababa wa kitume wa kiroho wenye neema, ambao wamewezeshwa kutoa msukumo kwa makusudi yake makubwa mno kwa ajili ya kanisa kwa utangazaji wao wa neno lake lenye nguvu kwa wale walio chini ya uangalizi na usimamizi wao.

Upanga mkali ukatao kuwili kutoka katika kinywa chake.

Mkali=Oxus maana yake ni *mkali, mwepesi.*

Neno hili chimbuko lake ni kutokana na Neno lenye maana ya ‘tindikali (asidi).’Tindikali ina athari za uchanguaji au kuyeyusha inapotumiwa juu ya kitu. Hili lina turejesha kwenye nguvu ya Neno ambalo hatua kwa hatua linayeyusha kile chenye makosa.

KUUACHA UPENDO WAKO WA KWANZA: UCHUNGUZI KIFANI KUHUSU WAEFESO.


Jina Efeso linamaanisha yafuatayo:

Kutamanisha; Kuto ruhusiwa; Legeza, Makusudi kamili; Tupia kwa.

Ufunuo 2:1-7

- 1. Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika: Haya ndiyo anenayo yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu.*
- 2.Nayajua matendo yako, na taabu yako na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo.*
- 3. Tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka.*
- 4. Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.*
- 5. Basi, kumbuka ni wapi uliko anguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.*
- 6. Lakini unalo neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo na mimi nayachukia.*
- 7. Yeye aliye na sikio na asikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.*

RAMANI INAYOONYESHA SEHEMU ZA KIJIOGRAFIA ZA YALE MAKANISA SABA NDANI TA ASIA.



Kati ya yale makanisa saba, Efeso limeorodheshwa la kwanza. ‘Nafasi ya kwanza’ ni nafasi ya kitume. Hii ni nafasi ya kwanza ambayo inaongoza njia kuingia kwenye utimilifu wa makusudi ya Mungu.

Chunguza namna ambavyo kila herufi kwa yale makanisa saba, Kristo anatambulishwa kwa namna mahsusi.

Efeso: *Haya ndiyo anenayo yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu [Ufun 2:1b]*

Smirna. *Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa mwisho, aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai. [Ufun 2:8b]*

Pergamo. *Haya ndiyo anenayo yeye aliye na huo upanga mkali, wenye makali kuwili [Ufun 2:12b]*

Thiatira. *Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, yeye aliye na macho yake kama mwali wa moto, na miguu yake mfano wa shaba iliyosuguliwa sana [Ufun 2:18b]*

Sardi. *Haya ndiyo anenayo yeye aliye na hizo Roho saba za Mungu, na zile nyota saba [Ufun 3:1b]*

Filadofia. *Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye [Ufun 3:7b.]*

Laodikia. *Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu [Ufun 3:14b]*

Hizi funuo binafsi za Kristo katika kila kanisa zinawakilisha sura mahsusi za Uungu ambazo zimefunuliwa kwa wazi kwa kila kanisa. Zinaangazia sehemu ya kipekee ya Asili ya Mungu

iliyo tiliwa mkazo katika muktadha huo mahsusi na una kumbukumbu imara kwa yaliyomo katika ujumbe uliofunuliwa kwa kila kanisa.

Kwa kanisa la Efeso, Kristo anatambulishwa kama ‘yeye azishikaye nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu’. Hili linaashiria kwamba lile kanisa la Efeso lilikuwa linamuona Kristo kama mmoja ambaye ana uwezo na kuzithibiti zile nyota zote saba- au viongozi waliokuwa juu ya kila kanisa; na yeye, Kristo akitembea katikati ya kila kanisa [kinara cha taa]- akikagua na kuwaeleza kuhusu utendaji kazi wao wanavyo wakilisha yeye mwenyewe. Kanisa hili linaelewa matendo ya yale makanisa mengine yote, ikiwa ni pamoja na nguvu, na udhaifu wao. Kanisa hili si tu kwamba linaelewa ufunuo na ujumbe wa Kristo kwa ajili yake, lakini pia kwa ajili ya mpangilio wote wa kanisa, na linajua kwa uhakika kila kanisa limefikia wapi mpaka sasa kwa kuzingatia lilipaswa kuwa wapi.

Kwa ufahamu huu, kanisa la Efeso linatupa picha ya kuwa na kanuni za kitume, ambalo miongoni mwa yale mengine linashikilia ile kanuni ya kuwekwa daraja la kwanza- siyo kwa sifa ya ubora, lakini ni kwa sifa ya utendaji wenye matokeo [Efes 2:20; 3:5; 4:11; 1Kor 12:28]. Moja kati ya misisitizo mikuu ya kitume ni kuhusu kila kanisa kuwa na kujikita katika Ukristo na ya jengwe na kutenda kwa usahihi [bila hitilafu].

Kanisa la Efeso lina ona picha kamili. Kwa hiyo haliwezi kustahimili uovu- halina kuvumilia. Linachukia roho ya Wanikolai (Nikolai=mharibu) anaye wakamata watu; wanikolai lilikuwa nidhehebu liloshikilia mafundisho ya Balaam- ambayo yana athari ya [miongoni mwa mambo mengi] kuharibu usafi [utakatifu] wa watu wa Mungu kupitia mahusiano yasiyo sahihi; yana haribu nguvu ya watu wa Mungu katika kuwakilisha sura yake kwa usahihi; yanataka kuwakamata watu nakuwageuza ili waingie katika utamaduni wa wakati wao. Kanisa la Efeso lina upendo na mapenzi makali ya kitume- na linatoa changamoto kwa watu na kwa mifumo ambayo siyo sahihi.

Kanisa la Efeso linasifika kwa bidii na uvumilivu wao katika kazi, kutovumilia kwao uovu, utambuzi wao kwa mitume wa uongo na mafundisho potofu ya kitume, moyo wao wa kutokata tamaa, uvumilivu ambao ni wa lazima kwa wajibu wao na utendaji kama kiongozi miongoni mwa yale makanisa saba, kwamba wameuacha upendo wao wa kwanza.

Hatimaye kanisa hili linapewa maelekezo: “Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi **kumbuka ni wapi ulipoanguka**; ukatubu, **ukayafanye matendo ya kwanza**” [Ufun 2:4, 5].

Lugha iliyotumika ku-elezea kosa lao ilikuwa ‘**kuacha upendo** wao wa **kwanza**’ na ‘**kuanguka**’.

Umeacha=aphiemi maana yake niacha, weka pembeni, ondoa, ruka, dharau n.k kuachilia kiondoke kufuatitangazo kutoka kwa mwenyewe, jali, mahudhurio, shughuli, kuondoka au kuacha peke yake.

Ulipo anguka= pipto peto maana yake ni kuanguka kutoka mahali pa juu kwenda mahali pa chini, kushindwa.

Kanisa la Efeso **waliuacha** upendo wao wa kwanza na hili linaelezewa kama ndipo mahali walipotoka na kuanguka. Wakati unapoanguka, unapoteza upeo ambao ungekusaidia kuwa na uwezo mkubwa wa kuona. Wakati unapoondoka taratibu au kidogo kidogo kutoka katika **UPENDO WAKO** wa **KWANZA**[ambao ni upendo kwa neno la Mungu] unapoteza

mwinuko wa kiroho; hivyo mtazamo na tathimini ya matukio na watu kwako vinakuwa na makosa.

Chunguza jambo hili: Waliondoka au waliuacha upendo wao wa kwanza kwa sababu ‘waliacha kutenda matendo’ waliyotenda hapo kwanza. ‘Wameanguka’ kutoka mahali hapa-inaashiria kwamba walipoteza upeo wao wa juu uliowawezesha kujiona na kujitambua wao wenyewe kwa usahihi na hali ya makanisa mengine. Swali la maana la kujiuliza ni: Matendo ya kwanza ya kanisa la Efeso yalikuwa yapi? Ili kuweza kupata jibu la swali hili, tunahitaji kuchunguza historia ya kanisa hili na msisitizo wake mahsusi kuhusu usahihi wa NENO LA MUNGU LA MUNGU lililokuwa linawajia kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

KULIELEWA KANISA LA WAEFESO

Efeso ulikuwa ni mji mashuhuri ulioko upande wa pwani ya magharibi ya mkoa wa Rumi katika Asia Ndogo. Ulikuwa unajulikana kwa kumwabudu Mungu mke aliyeitwa Diana. Ulikuwa ndio makao makuu ya mkoa na ulijipatia ushawishi mkubwa katika eneo lote. Chunguza mwanzo wa shughuli za kiroho ndani ya Efeso:

Mdo 18:19-28

- 19. Wakafika Efeso, akawaacha huko. Yeye mwenyewe akaingia katika sinagogi, akahojiana na Wayahudi.*
- 20. Walipomtaka akae wakati mwingi zaidi, hakukubali;*
- 21. bali aliagana nao, akisema, Nitarejea kwenu tena, Mungu akinijalia akatweka, akatoka Efeso.*
- 22. Na alipokwisha kushuka Kaisaria, akapanda juu, akawasalimu kanisa, kisha akatelemkia Antiokia.*
- 23. Hata akiisha kukaa huko siku kadha wa kadha akaondoka, akapita kati ya nchi ya Galatia na Frigia, mji kwa mji, akiwathibitisha wanafunzi.*
- 24. Basi Myahudi mmoja, jina lake Apolo, mzaliwa wa Iskanderia mtu wa elimu, akafika Efes; naye alikuwa hodari katika maandiko.*
- 25. Mtu huyo alikuwa amefundishwa njia ya Bwana; na kwa kuwa roho yake ilikuwa ikimwaka, alianza kunena na kufundisha kwa usahihi habari za Yesu; naye alijua ubatizo wa Yohana tu.*
- 26. Akaanza kunena kwa ujasiri katika Sinagogi; hata Priskila na Akila walipomsikia wakamchukua kwao, wakamweleza njia ya Bwana kwa usahihi zaidi.*
- 27. Na alipotaka kuvuka bahari aende mpaka Akaya, ndugu wakamhimiza, wakawaandikia wale wanafunzi wamkaribishe, naye alipofika akawasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Mungu.*
- 28. Kwa maana aliwashinda Wayahudi kabisa kabisa mbele ya watu wote akionesha kwa maneno ya maandiko ya kuwa Yesu ni Kristo.*

Matendo ya kwanza ya kanisa la Efeso yameandikwa katika Matendo 19. Yanaweka nafasi ya uthamani wa juu kabisa katika Neno la Mungu.

Mdo 19:1-20

1. *Ikawa Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko;*
2. *Akawauliza, je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlopoamini? Wakamjibu, la, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukumsikia.*
3. *Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema kwa ubatizo wa Yohana.*
4. *Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakaye kuja nyuma yake, yaani Yesu.*
5. *Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu.*
6. *Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri.*
7. *Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili.*
8. *Akaingia ndani ya Sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta kwa mambo ya Ufalme wa Mungu.*
9. *Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile njia mbele ya mkutano, basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina laje Tirano.*
10. *Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wyunani.*
11. *Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida;*
12. *Hata wagonjwa wakaletwa lesu na nguo zilizotoka mwilini mwake magonjwa yao yakawaondokea, na pepo wachafu wakatoka.*
13. *Baadhi ya Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu, wakisema, nawaapisha kwa Yesu yule anaye hubiriwa na Paulo.*
14. *Walikuwako wana saba wa mtu mmoja Skewa, Myahudi, kuhani mkuu waliofanya hivyo.*
15. *Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani?*
16. *Na Yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa.*
17. *Habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawaingia wote, na jina la Bwana Yesu likatukuzwa.*
18. *Na wengi wa walio amini wakaja wakaungama, wakidhihirisha matendo yao.*
19. *Na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote; wakafanya hesabu ya thamani yake wakaona ya kwamba yapata fedha hamsini elfu.*
20. *Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu.*

Mambo ya kuzingatiwa kuhusu matukio na shughuli ndani ya Efeso.

1. Efeso, mahali pa ku-inuliwa na pa mpito [kupitia]

Kule Efeso, wanafunzi wa Yohana wanapiga hatua kuingia katika msisitizo uliopo hivi sasa au katika majira ya Mungu. Paulo alikutana na wanafunzi kumi na wawili wa Yohana mahali hapa na kuwaelezea kuhusu ubatizo katika Roho Mtakatifu. Ujuzi ambao kamwe hata hawakujua ulikuwepo.

Walikuwa hawaujui ujuzi huu kwa sababu ya fundisho walilokuwa wamejiunga nalo. Mafundisho ya Yohana yalisisitiza tu kuhusu toba na ubatizo wa maji mengi. Katika sura iliyopita, Apolo, ambaye alikuwa amefunzwa vema katika mafunzo ya Yohana, alikubali yeye mwenyewe ku-inuliwa na Akila na Priskila, wana wawili wa Paulo katika Bwana. Aliendelea kutoka njia sahihi hadi kwenye njia iliyo sahihi zaidi. Hata hivyo, hawa wanafunzi kumi na wawili wa Yohana, ambao kwa sasa pengine ni wanafunzi wa Apolo, walikuwa hawajasikia fundisho la kitume lililokuwepo mpaka walipokutana na Paulo, ambaye kwa haraka aliwapa fursa ya kuingia katika awamu mpya ya Mungu ya kushughulikia kanisa.

Jambo ninalotaka kulitilia mkazo hapa, ni kwamba, yote haya yalitokea kule Efeso. Efeso ni mahali pa kuinuliwa na pa kupitia kuingia katika kunena kwa sasa kwa Mungu. Sehemu ya maana ya 'Efeso' ni 'ya kuatamanisha' na 'kukusudiwa kikamilifu.' Efeso linawakilisha mahali pa kutamanisha katika roho, pa kufikia, mahali ambapo utimilifu wa kusudi la Ki-Uungu linaweza kutambuliwa kwa sababu ya uamuzi wa mtu kushikamana na majira mapya katika Mungu.

Skewa, ambaye alikuwa kuhani Mkuu wa Kiyahudi na wana wake saba, walikataa kuinuliwa na kupitishwa katika msisitizo uliopo sasa. Kifo cha Yesu kiliashiria tamati ya utaratibu wa Agano la Kale la Kikuhani wa Kilawi, na bado mwanamme huyu alikuwa anaendelea kutenda kama Kuhani Mkuu. Shughuli zake za kiroho zilikuwa hazipasi kuwepo. Alikuwa na wana saba [kiashiria cha uwana uliokamili katika mazingira yasiyo sahihi] na hata hivyo alitimiza majukumu ya kuwa baba wa kiroho. Ubaba wake haukuwa sahihi. Ubaba wa kiroho peke yake haukuhakikishii usahihi. Kuwa baba ni kupaswa kuwepo katika unenaji wa sasa wa Bwana. Skewa ambaye jina lake lina maanisha '**mkono wa kushoto**' hakuwa na mamlaka ya mkono wa *kulia* au mamlaka yaliyo *tambuliwa katika ulimwengu wa roho*. Yeye na wanawe walijaribu kutumia mamlaka ya kiroho wakitarajia kupata matokeo kama yale yaliyotokea katika huduma ya Paulo. Mamlaka ya kimapepo ikaonesha kuto watambua na waka teswa na kudhalilishwa. Yote haya yalitukia kule Efeso. Wale waliokataa kuhamia katika yanayo nenwa na Mungu hivi sasa, yakawekwa wazi katika jaribio lao la kutaka kupata mafanikio na matokeo ya majira haya yaliyopo ya kitume, na wakapoteza msimamo wa kiroho, mamlaka na kutambuliwa.

Tafadhali weka kwenye ufahamu wako kwamba Efeso palikuwa ni mahali ambapo Neno la Mungu lilipewa uthamani na kipaumbele cha hali ya juu sana. Katika Ufunuo 2:2, wanasifika kwa uwezo wao wa kutambua maelezo potofu ya kitume. Tunaiona ishara ya awali ya uwezo huu hapa, kwamba utaratibu potofu wa kitume ulio wakilishwa na Skewa uliwekwa wazi. Msingi wa kufichuliwa kwao ulitokana na kushindwa kwao kuhamia katika Neno linahubiriwa na Paulo kwa sasa. Neno ambalo kama wao wangelitii, lingeweza kuwapa uzito na akili katika ulimwengu wa roho.

2. Efeso, Mahali pa Kufikiria na Kushawishi kuhusu Ufalme wa Mungu

Mdo 19:8-9

8. *Akaingia ndani ya sinagoga, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu.*
9. *Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile njia mbele ya makutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa la mtu mmoja jina lake Tirano.*

Paulo alinena kijasiri kwa miezi mitatu katika sinagoga kuhusu Ufalme wa Mungu, mbinu yake ya utendaji ilikuwa ni moja ya: -**KUHOJI NA KUSHAWISHI** kuhusu Ufalme wa Mungu. Baadhi hawakujihusisha na mafundisho yake, na wakawa ‘wagumu’ na ‘wasiotii’ na wakaanza kukashifu ile ‘njia’ kwa kutoa maelezo ya kutunga yaliyotafsiriwa kama mafundisho mapya ya kidini ya siku yao, kitu kilicho kuwa tofauti na kile kilichokuwepo. Kila muondoko mpya wa Mungu utasumbuliwa na wale wasiouelewa kikamilifu.

Paulo aliacha kulitumia sinagoga kama mahali pa kutangaza mafundisho yake na akaenda kutumia shule ya Tirano kwa miaka mingine miwili. Hapa pia, mbinu aliyotumia kufikisha ujumbe wake ilikuwa ni moja: -**kuhojiana**.

KUHOJIANA

Kuhojiana= dialegomai maana yake ni *kuzungumza kwa kijibizana au kinyume chake, kuzungumza na, hoja, kuwasilisha hotuba ya kisomi, kusema sawa sawa, ndivyo ilivyo, jadili [kwa kubishana au kushawishi], kuzungumza, kuongea, kuhutubiana, bisha, jadili.*

Kushawishi=peitho maana yake ni *kumshawishi mwingine ili aipokee Imani; Kugusa kwa maneno ya huruma au hamasa; Kushawishi.*

Mbinu hii ya kuhojiana na kushawishi ilihitaji Paulo awe amefunzwa vema katika kile alichotaka kufundisha na kuhubiri. Lipo hitaji muhimu kwa wakati tulio nao hivi sasa, kwa ajili yetu kuwa ni wenye kufunzwa vema maandiko, na haswa katika kile ambacho anakisisitiza Mungu hivi sasa. Apolo alikuwa na ‘uwezo mkubwa katika maandiko’ na ‘ali-lelewa katika njia za Bwana’ na kwasababu hiyo, alinena ‘kwa ujasiri katika sinagoga’. Usomaji wa kutupia macho wa hotuba ya Petro katika Mdo. 2 na kujitetea kwa Stefano katika Mdo. 7 inaonesha kwamba wote wawili walikuwa na maarifa kamili ya maandiko. Katika kipindi kijachokatika mfululizo huu, tutaangalia hitaji la kujifunza kwa bidii Neno, ili kwamba tuweze KUHOJI NA KUSHAWISHI watu kiupelelezi, kuhusu Neno la Mungu lililopo kwa majira yoyote tunayoishi hivi sasa.

3. Efeso Mahali Makini pa Kukutana na Neno la Mungu kutoka Chanzo cha Kweli cha Kitume.

Baada ya miezi yake mitatu ya kujibana ya mafundisho kidogo ndani ya sinagoga, Paulo alifundisha **kila siku** kwa miaka 2 katika shule ya Tirano. Kulikuwepo na **kukutana** na Neno la Mungu kwa miaka miwili kamili- bila kupumzika. Jambo hili linawezekana liliendelea kwa miaka mitatu [soma Mdo 28:31]. Kulikuwa na kuabudu kupita kiasi na upendo kwa Neno la Mungu na hasa kwa msisitizo mpya na uelewa ambao Paulo aliwapelekea.

Katika Biblia yenye maelezo ya ziada [Amplified Bible] inadokeza kwamba kwa miaka miwili kila siku kuanzia saa 4 asubuhi mpaka saa tisa alasiri, Paulo alifundisha katika shule ya Tirano. Kulikuwepo na njaa kali kwa ajili ya Neno la Mungu.

Mdo 19:9b ...”*akaondoka akawaacha akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja jina kale Tirano kutoka kama saa nne kamili mpaka saa tisa [Amplified Bible].*

Leo sisi tunakuwa na mtazamo finyu na ulio mdogo sana wa kusikia Neno la Mungu. Tunadharau kitu halisi kilicho andaliwa kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika miji yetu. Kwa waaminio wengi kujitoa kwao kwa neno la Mungu kumepungua hadi kufikia dakika thelathini za kusikiliza Neno siku ya Jumapili asubuhi. Inapaswa kuwepo na utamaduni wa kuli tumaini Neno zaidi katika kanisa la sasa. Kanisa la kwanza liliendelea kusimama imara katika fundisho la Kitume – soma Mdo 2:42.

Baada ya muda wakati Paulo akiwa anaondoka Efeso, wakati akiwa Mileto, aliwaita wazee wa kanisa la Efeso na kuwapa maelezo ya mwisho.

Mdo 20:15-31

15. *Tukatweka kutoka huko na siku ya pili tukafika mahali panapokabili Kio; siku ya tatu tukawasili Sarmo, tukakaa Trogilio, siku ya nne tukafika Mileto.*
16. *Kwa sababu Paulo anakusudia kupita Efeso merikebuni, asije akakawia katika Asia, kwa maana alikuwa na haraka akitaka kuwahi Yerusalemu siku ya Pentekoste, kama ikiwezekana.*
17. *Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa.*
18. *Walipofika kwake akawaambia, ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote,*
19. *Nilimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote, na kwa machozi, na majaribu yaliyo nipata kwa hila za Wayahudi;*
20. *Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lolote liwezalo kuwafaa, bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba,*
21. *Niliwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo.*
22. *Basi sasa, angalieni, nashika njia kwenda Yerusalemu hali nimefungwa rohoni, nisiyajue mambo yatakayonikuta huko;*
23. *Isipokuwa Roho Mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia akisema, ya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja.*
24. *Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia habari njema ya neema ya Mungu.*
25. *Na sasa, tazameni, mimi najuwa ya kuwa ninyi nyote niliwahubiria Ufalme wa Mungu, nikienda huko na huko, hamtaniona uso tena.*
26. *Kwa hiyo nawashuhudia wote siku hii ya leo, ya kuwa mimi sina hatia kwa damu ya mtu yeyote,*
27. *Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*
28. *Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*

29. *Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu Mbwa mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi,*
30. *Tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.*
31. *Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka yakwamba miaka mitatu usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi.*

Baadaye kutokana na mbinu yake ya kuhoji na kushawishi, Paulo anaweka wazi pia kwamba ali ‘tangaza’, shuhudia’ na ‘kufundisha’,

Tangaza= anaggello maana yake ni *kutoa tangazo [kinaga naga], kutangaza, simulia,toa taarifa,onesha, nena, ambia.*

Shuhudia= diamarturomai maana yake ni *kushuhudia au kupinga kwa dhati, kidini ni kushitaki, kuthibitisha kitu kwa ushuhuda, kushuhudia, kusababisha kiaminiwe.*

Fundisha=didasko maana yake nikuwa na *mazungumzo na wengine ili kuwapa maelekezo, kutoa elimu mihadhara; kuota maekezo; kuingiza fundisho ndani ya mtu; kufafanua au kuelezea kinaga naga.*

Paulo alisambaza Neno hadharani na nyumba hadi nyumba. ‘Nyumba kwa nyumba yaani, Neno kwa Neno lilisomwa kutoka familia moja hadi familia nyingine’.

Hili halizungumzii nyumbani mahali halisi pa kuishi ila kwa kanisa ambalo wanakutana kama familia- kaya ya Imani. Mahali walipokutana siyo suala muhimu. Baadhi labda zilikuwa kubwa na baadhi ndogo. Kitu cha muhimu katika jiji lote la Efeso kilikuwa, Paulo alijongea kutoka nyumba moja hadi nyingine.

Lakini pia alifundisha wazi wazi ndani ya sinagogi na katika shule ya Tirano. Mahali hapa labda wazee au wababa wa kiroho wa kaya hizi za imani walikuwa wana kutana kwa lengo la kupokea fundisho la Kitume kutoka kwa mtume Paulo. Kisha baadaye wanarudi kwenye kaya zao na kuyagawa haya kwa watu wao. Hili linatuonesha kuwa,kuna uhitaji kwa kila kanisa la mahali au kaya ya imani ndani ya jiji au mkoa kuunganika na neema ya ubaba wa kitume ulio halali na wa uhakika, ambayo kutokana na hiyo watakuwa wanapokea fundisho.

4. Efeso, Mahali Ambapo Mataifa Yanakutana Kulisikia Neno la Mungu, Mahali Ambapo Neno la Mungu Linakua kwa Nguvu na Kudumu.

Matokeo ya mtazamo mkali sana kuhusu neno la Mungu kule Efeso ulikuwa kwamba, Asia yote ili sikie Neno la Mungu. Kutokana na hili tunaona kwamba Efeso lilikuwa ni jiji la kimkakati wa hali ya juu kwa ajili ya kueneza Injili. Ilikuwa ni jiji ‘lango’. Ilikuwa ndio kitovu ambacho Neno la Mungu lilipata mseleleko mkubwa na wa kasi kuingia katika maeneo yaliyoiuzunguka. Miji inayofanana na Efeso inapaswa kuibuka leo- mahali ambapo kutoka hapo Mungu anaweza kuanzisha hali zenye maana za malengo yake ya ki-ulimwengu ambayo yataenda mbali na kufikia kuleta matokeo katika ulimwengu wa kiroho.

5. Efeso, ni mahali ambapo Itikadi za Kibinadamu na mifumo ya Dini potofu zilizopingana na mapenzi ya Mungu zili haribiwa kwa sababu ya Neno la Mungu.

Matokeo ya mwisho ya mtazamo mkali wa Paulo katika kufundisha Neno la Mungu kule Efeso, ni kuchomwa kwa wastani vipande 50,000 vya fedha, vitabu vya thamani vya uchawi, na

kuhamisha ibada za mungu mke Diana [Artemi]. Hili lilishuhudiwa kuwa hasara kubwa yamapato yaliyotokana na kuuza vibanda vya fedha vya mungu mke katika jiji. Mhunzi wa fedha ambaye alikuwa akitengeneza vibanda hivi, Demetrio, na watu wengine wa namna yake, walipinga lakini haikusaidia.

Vitabu vyenye thamani ya vipande 50,000 vya fedha vilichomwa. Hizi ni sawa na fedha ya Kiyunani iitwayo ‘**drachma**’ 50,000. **Drachma** moja ni sawa na kisio la malipo ya kazi ya siku moja. Hivyo **drachma** 50,000 ni kwa makisio ya mshahara wa miaka 137 wa kazi ya kila siku. Kufundisha kwa Paulo na mtazamo mkali wa kila siku hasa kuhusu Neno la Mungu kuliathiri uchumi wa eneo husika. Kulikuwa hakuna tena kazi za ibilisi zilizokuwa zinafadhiliwa kwa fedha.

Kwa kuingiza kanuni za Neno la Mungu ndani ya watu wa Efeso, siku zote Paulo aliziimarisha na kuzifanya madhubuti tunu au kanuni za ufalme wa Mungu. Diana mungu mke alikuwa ni mamlaka ovu ya kimapepo iliyotawala juu ya Efeso. Mamlaka ovu inakuwa imepewa uwezo wa kutawala juu ya ardhi ya eneo fulani na kuwa na mamlaka ya kisheria kwa kadri watu wa milki hiyo wanavyo jiunga nayo na kutenda sawa sawa na kanuni fulani zinazohusiana nayo. Ili kuvunja nguvu ya mamlaka hiyo, ni rahisi. Haribu kanuni zake inazotumia katika kutenda, kwa kuiondoa kupitia uwasilishaji fundisho na uwekezaji katika moyo au nia za watu, kanuni za ufalme wa Mungu. Hili lilifanyika kupitia Neno la Mungu. Kule Efeso, jiji lote na jimbo lote la Asia kulikuwa na mguso chanya wa kujazwa njia za Mungu na tunu zake kupitia misisitizo ya kila siku na utangazaji wa Neno la Mungu. Neno la Mungu linahitaji kupendwa na kupewa kipaumbele hadi kufikia upeo maalum ikiwa tunataka kubadilisha tamaduni za majiji yetu ili zifanane na ule wa ufalme wa Mungu. Pia lile Neno ambalo tunataka lihubiriwe linapaswa kuwa na uhusiano na fundisho la kitume lililopokelewa kupitia Mtume wa kweli mwenye kuaminika, na mwenye kustahili wa Kristo.

HITIMISHO. Ule upendo wa kwanza ambao kanisa la Efeso LILIUACHA – na ile nafasi walioiacha na KUANGUKA- ilikuwa ni upendo wao kwa ajili ya Neno na bidii kwa NENO LA MUNGU. Kwa sababu tusizojua sisi, walikaa mbali kutoka ubora na kipaumbele cha NENO LA MUNGU. Hivyo wakapoteza uthamani wao. sura nyingine za maana ya ‘Efeso’ ni pamoja na, kuacha kutoa, kupumzika, kuzembea. Labda walifanya kupumzika na wakapoteza msimamo wao katika neno la Mungu; walilegeza mshikamano wao mkali wa kulipenda neno, na hivyo kupoteza wepesi wao. Isije kutokea nasi tuka**anguka** kutoka nafasi zetu za kipaumbele cha juu na kule kujitoa kwetu kulitii Neno la Mungu linalo endelea kutujia. Mamlaka yakanisa la kitume ni kwa uhalisia ku-unganika na ubora unaopatikana katika Neno la Mungu. Mahali ambapo Neno linapopewa nafasi ya pili, mamlaka ya kitume yatakuwa yameporomoshwa.

Tendo mkakati la Paulo la mwisho kuhusu kanisa la Efeso lilikuwa ni kuukabidhi uongozi wake, yaani wazee wa Efeso, katika neema ya Neno la Mungu.

Mdo 19:32. *“Basi wengine walikuwa hivi na wengine hivi na wengine hivi; kwa maana ule mkutano ulikuwa umechafuka-chafuka, na wengi wao hawakujua sababu ya kukusanyika kwao pamoja.*

Paulo **aliwakabidhi** katika **nen**o la **neema** yake. Neno ‘**kabidhi**’ [**poratithemi**] linamaanisha *kuwekwa karibu*. Paulo aliwatia moyo, kamwe wasije wakapoteza kule kuwa karibu na Neno la Mungu- na Paulo analitaja kama ni **nen**o la **neema** yake. Kimsingi neema inagawiwa kupitia Neno la Mungu. Kuwa na upungufu wa neno ni kuwa na upungufu wa neema ambayo kwa

ukweli ndiyo inayopangilia utambulisho ndani ya Mungu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu yako katika ufalme. Paulo aliendelea kusema kwamba **Neno la Mungu** lina uwezo wa **kujenga** na kutupa njia ya kuingia katika urithi wetu ulio ndani ya Mungu.

Paulo alimchukua mwana wake bora Timotheo na akamweka yeye awe kiongozi kule Efeso. Timoteo naye alipaswa kuwa weka wazee mahali pale na kuzuia mafundisho mengine [soma 1Tim 1:3] Mistari inayo zungumzia nguvu ya **kanisa lenye mtazamo** wa **nen**o kama Efeso. Ipo katika Mdo 19:20 na 9:10.

Mdo 19:20. *Hivi ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu.*

Mdo 19:10b. *Wote waliokaa Asia wakalisikia Neno la Bwana.*

Zingatia pia:

Mdo 6:7. *Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu, jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani.*

Mdo 12:24 *Neno la Bwana likazidi na kuenea.*

Mdo 5:42. *Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.*

Mdo 13:5. *Na walipokuwa katika salami wakalihubiri neno la Mungu katika masinagogi ya Wayahudi nao walikuwa naye Yohana kuwa mtumishi wao.*

Mdo 13:48-49. *Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana, nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini.*

MASWALI NA MASUALA BINAFSI YA JEREA NA MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI.

1. Fafanua maana ya kialama, kadhalika maana muhimu ya zile nyota saba na vinara vya taa saba katika Ufunuo sura ya kwanza?
2. Elezea maana muhimu ya kuliweka kanisa la Efeso katika nafasi ya kwanza miongoni mwa yale saba. Hili lina matumizi gani kwa wakati wetu katika kanisa la leo?
3. Kibibilia, **upendo wa kwanza** inazungumzia nini? Onesha jibu lako kwa kutumia kanisa la Efeso kama mfano.
4. Ni mbinu gani aliyotumia Paulo kueneza Neno la Mungu kule Efeso? Alipenda kutumia utaratibu gani katika kuelezea ujumbe wake? Katika majibu yako kwa hili, jadili kwa pamoja mbinu zake katika upeo wa mkazo na ukawaida.
5. Ni athari zipi na matokeo yapi viliambatana na mtazamo mkali wa Paulo juu ya Neno la Mungu kule Efeso?
6. Je! ‘Umeuacha’ ‘upendo wako’ wa ‘kwanza?’

